

**MATUMIZI YA NGELI MIONGONI MWA WANAFUNZI WA KISWAHILI WA  
CHUO KIKUU CHA MASENO, NCHINI KENYA**

**NA**

**MARY LUKAMIKA KIBIGO**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA  
SHAHADA YA UZAMILI KATIKA KISWAHILI  
YA CHUO KIKUU CHA MASENO**

**IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA NYINGINE ZA KIAFRIKA**

**KITIVO CHA SANAA NA SAYANSI JAMII  
CHUO KIKUU CHA MASENO**

**OKTOBA**

**2015**

## UNGAMO NA IDHINI

Tasnifu hii ni kazi yangu asilia na haijawahi kuwasilishwa kwa minajili ya shahada katika Chuo Kikuu kingine.

.....

**Mary Lukamika Kibigo**

.....

Tarehe

PG/MA/098/2011

Idhini imetolewa kwa minajili ya kutahiniwa tukiwa wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Maseno.

.....

**1. Prof. Florence Indede**

.....

Tarehe

Idara ya Kiswahili na

Lugha Nyingine za Kiafrika

Chuo Kikuu cha Maseno

.....

**2. Prof. Sangai Mohochi**

.....

Tarehe

Shule ya Sanaa na Sayansi Jamii

Chuo Kikuu Kishiriki cha Rongo

## **HATILINZI**

Hakuna ruhusa ya kunakili kazi hii ama kuihifadhi kwa mfumo wowote bila ruhusa kutoka kwangu au Chuo Kikuu cha Maseno.

## SHUKRANI

Kwanza kabisa ningependa kumshukuru Rabana kwa kunijalia kuishi, kunipa siha njema na kuniwezesha kusoma hadi kiwango cha uzamili. Kama siye Mola, bila shaka hakuna lolote zuri ambalo ningeweza kulitekeleza. Ahsante sana Maulana!

Ninakishukuru sana Chuo Kikuu cha Maseno kwa kunisajili kuendelea na masomo yangu na pia kwa kunipatia wasimamizi walio wakwasi katika taaluma ya Kiswahili.

Shukrani zangu za dhati ziwaendee wasimamizi wangu weledi Prof. Florence Indede na Prof. Sangai Mohochi. Ahsanteni kwa kujitolea kwa hali na mali kunielekeza ipasavyo mkanihimiza na kunipa mawaidha mwafaka yaliyoipelekea tasnifu hii kukamilika. Mungu awakirimie baraka zake zisizo kifani. Aidha, ninatoa shukrani tele kwa Prof. Inyani Simala kwa kunishauri, kunipa ari ya kukipenda Kiswahili na kunikuza kiakademia.

Vilevile, Dkt. David Ongarora ulinipa ushauri uliufaa utafiti wangu hasa kinadharia, ahsante sana Daktari! Pongezi zisizo kifani ziwaendee wahadhiri wangu wapendwa Dkt. Asiko Beverline, Dkt. Amukowa Deborah, Bw. Lumwamu Philip, Bw. Mulwale Martin, Bw. Okal Benard, Dkt. Kasomo, Bw. Masila James, Dkt. Ojwang' Benard na Bw. Muga. Ahsanteni kwa kunipa ari ya kuendelea na utafiti wangu. Ukwasi wenu wa lugha ya Kiswahili ulinipa mshawasha wa kuiboresha tasnifu hii. Mterehemezi awajalie hekima na maarifa teletele.

Ninakushukuru sana marehemu babangu mpendwa Kibigo Musa kwa kunilea na kunihimiza licha ya kuwa dua yako kuu kwangu ilikuwa niwe tabibu. Hata hivyo, ninaazimia kuwa Daktari wa lugha ya Kiswahili ili niweze kuwatibu wengi wanaotarajia kuwa weledi katika taaluma hii. Kwa marehemu mamangu mpenzi Agnetta Kasaya, kaka zangu Elphas Ukiru na Saul Onzere, ahsanteni sana kwa kuyafadhili masomo yangu. Kwa dada zangu Priscilla Imali na Esther Nyangasi, ahsanteni kwa kunihimiza na kunisaidia kwa hali na mali.

Shukrani nyingine ziwaendee wazamili wenzangu: Enock Mokuu, Philemon Etole, Frida Miruka na Roseline Odongo. Ahsanteni kwa kunitia shime tulipokuwa tukipiga mbizi pamoja katika bahari ya masomo. Mbarikiwe sana. Aidha, sehemu hii isingekamilika bila kuwashukuru wafuatao: Mume wangu mpenzi bwana Peter Lisero; ulinipa utulivu na kunifaa kifedha bila kuwa hoi, ahsante sana mpendwa wangu! Isitoshe, watoto wetu wapendwa Fanana Wilbroda, Musa Gentle, Josephat Chichi, Flavian Oyolo na Florian Kutswa kwa ustahimilivu wenu nilipokuwa nikizamia masomo yangu. Ahsanteni!

Kwa wanafunzi wote wa Chuo Kikuu cha Maseno mlioshiriki katika utafiti huu, ninawashukuru sana.

Kwa Moses Oswago, Linda Namude, Benard Khayumbi na Bellah Atieno, ahsanteni sana kwa uvumilivu wenu wa kuipiga chapa kazi hii. Mola awabariki nyote ambao sikuweza kuwataja na mliweza kuuchangia ufanisi huu kwa njia moja au nyingine. Asanteni sana na Mungu awabariki nyote. Shabash!

## **TABARUKU**

Kwa marehemu babangu mpendwa Zakayo Musa Kibigo, marehemu mamangu kipenzi Agnetta Kasaya, kwa mume wangu mpenzi Peter Abraham Lisero na wanangu wpendwa watano; ninyi ndio mlionipa kiu cha kuyaenzi masomo. Kwa hivyo, kwa heshima, taadhima na unyenyekevu, ninawatabarukia kazi hii!

## IKISIRI

Utafiti huu unachunguza matumizi ya ngeli miongoni mwa wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno. Sura ya kwanza imeshughulikia ngeli kama msingi muhimu wa usarufi wa lugha za KiBantu hususan lugha ya Kiswahili. Dhana ya ngeli ni pana na tata kiasi cha kuwakanganya watumizi wengi wa Kiswahili wakiwemo wanafunzi. Mtazamo huu umechochewa na mkondo wa fikra unaotambua ngeli kama mojawapo ya vipengele muhimu vya sarufi ya Kiswahili. Licha ya kutekeleza wajibu huu, bado kuna ngeli ambazo hutatiza na kuzua changamoto kwa watumizi wa Kiswahili hasa wanafunzi, pengo ambalo utafiti huu unadhamiria kuliziba. Madhumuni mahsusi yalikuwa: Kubaini makosa yanayotokea wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno wanapotumia ngeli, kujadili changamoto zinazotokea wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno wanapotumia ngeli, na kupendekeza mikakati ya kukabiliana na matatizo hayo ya kisarufi na kuweza kuinua umilisi wa kiisimu katika Kiswahili miongoni mwao. Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya Uchanganuzi wa Makosa kulingana na Corder (1974). Mihimili mitano ya nadharia iliyotumiwa ni; Kukusanya sampuli ya lugha ya wanafunzi, kutambua, kuainisha, kuelezea na kutathmini makosa. Sura ya pili imefafanua tahakiki ya maandishi. Sura ya tatu imejikita katika kufafanua muundo mseto wa kitathmini na kitakwimu na njia na mbinu za utafiti zilizohusu uchunguzi maktabani na nyanjani. Ukusanyaji data nyanjani ulifanywa kwa kuwarekodi wanafunzi wakijadiliana katika vikundi maalum vya Kiswahili kuhusu mada za kozi zinazohusu ngeli, kurekodi usaili pamoja na kuwapa mada za insha kuandikia na kuzisahihisha ili kupata data, baina ya mwezi wa Februari na Aprili, 2013. Uthibitishaji na uhakikishaji wa vifaa ulifanyiwa majaribio awali na wataalam katika Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika pamoja na utafiti wa awali. Usampulishaji mahuluti ulitumiwa ambapo uteuzi sampuli wa mtabakisho, uteuzi sahili usioratibiwa na usampulishaji maksudi zilitumiwa kuwateua wanafunzi 54 wa Kiswahili wanaochukua shahada ya kwanza kutoka kwa idadi ya jumla ya wanafunzi 540 kuanzia mwaka wa kwanza hadi wa nne. Sura ya nne imeshughulikia uchanganuzi wa data uliojikita katika kusikiza na kunukuu rekodi za majadiliano na usaili na kuchanganua insha zilizoandikwa na kusahihishwa ili kulifikia lengo. Aidha, data zilichanganuliwa na kuwasilishwa kimaelezo na kijedwali. Utafiti huu umeonyesha bayana kuwa ngeli ni kipengele muhimu cha sarufi kinachodhihirisha umilisi na utendaji wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili. Vilevile, utafiti umebaini ngeli za ziada na zinazotatiza hususan LI-YA, PA-KU-MU na KI-VI pamoja na changamoto zake zinazohusu vivumishi tata kama, jingine na lingine; zingine na nyingine katika ngeli za LI-YA na I-ZI mtawalia. Mikakati kama uzingativu wa maana na sarufi ilipendekezwa, ili kukabiliana na matatizo hayo ya sarufi na kuinua umilisi wa kiisimu katika Kiswahili miongoni mwao. Uchunguzi huu uliwezesha utafiti kufikia malengo yake na kujibu maswali yote ya utafiti. Matokeo ya utafiti huu yalikusudia kutoa mwanga zaidi uelewa wa matumizi ya ngeli katika Chuo Kikuu cha Maseno, Vyuo Vikuu na lugha ya Kiswahili kwa jumla. Hata hivyo, utafiti huu ulidhihirisha kuwa dhana ya ngeli bado ilikuwa tatizo kwa wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno hasa wa viwango vya chini kwani baadhi yao hawakuelewa msingi wake. Kwa hivyo, utafiti huu unapendekeza kuwa kuna haja ya dharura kwa wapangaji sera wa Kiswahili kuandaa semina, warsha na kongamano ili kuhamasisha wanafunzi wa Kiswahili kuhusu umuhimu wa dhana ya ngeli katika Chuo Kikuu cha Maseno, lugha ya Kiswahili na isimu kwa jumla.

## ABSTRACT

The main purpose of this research was to investigate the use of noun classes among Maseno University Kiswahili students. The first chapter has dealt with Noun classification as a basis of grammar that is very vital in creating linguistic competence and performance of words in most Bantu languages especially Kiswahili. The concept of Noun classes is wide in scope in the sense that it brings contrast among most Kiswahili users including the students. This approach recognizes Noun classification as one of the important aspects of Kiswahili Grammar. Despite this accomplishment, some Noun classes are still problematic and challenging among Kiswahili users especially students. This research aimed at filling this gap. The specific objectives were to establish the errors observed as the Kiswahili students used the noun classes, discuss the challenges facing them as they used the noun classes and recommend the strategies to be undertaken in order to deal with these grammatical errors hence creating linguistic competence in Kiswahili language. The study adopted Corder's Error Analysis theory (1974) whose five tenets include; the collection of a sample of learner language, identification, explanation, description and evaluation of errors. The research used mixed design; evaluative and quantitative. Data collection in the field was done through tape-recording of Kiswahili undergraduate students as they discussed in their focus Kiswahili groups, interview and they also wrote compositions which were marked for data output. These tools were pretested and piloted by experts in Kiswahili and Other African Languages (KOAL) department to enhance their reliability and validity. The research used the multistage sampling technique whereby stratified sampling, simple random sampling and purposive sampling techniques were used to cater for the different categories of informants that the study had targeted. The total population of 540 Kiswahili students was sampled which gave us a sample of 54. The research used primary and secondary data collection techniques based on extensive library research and fieldwork. The data collected was transcribed, analyzed and presented through discussions and tables. The study revealed how Kiswahili students used the Noun classes, the extra noun classes and the specific challenges facing them like the use of adjectives in noun class 'LI - YA' and 'I-ZI' and the problematic noun classes such as 'LI-YA', 'PA-KU-MU' and 'KI-VI' and the strategies that were undertaken to deal with the grammatical errors like the use of meaning and the value of grammar hence creating linguistic competence Maseno University, Universities and Kiswahili in general. However, the study revealed that the concept of Noun classes was still an issue to be ironed out by the Kiswahili University students especially the lower years (1<sup>st</sup> and 2<sup>nd</sup>). Therefore this research recommends that there is an urgent need by the Kiswahili policy makers to hold seminars, workshops and conferences so as to sensitize the Kiswahili learners about the importance of Noun classes and aspects of Kiswahili grammar in Maseno University and grammar in general.

## VIFUPISHO NA AKRONIMU

**KOAL:** Kiswahili and Other African Languages\_Kiswahili na Lugha Nyingine  
za Kiafrika.

**K :** Konsonanti

**V :** Vokali

**N:** Nomino

**TUKI:** Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili

**T:** Vitenzi



## MCHORO

<b>Mchoro 1.</b> Chati ya duara ya kiwango cha umilisi wa lugha ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Maseno .....	82
--------------------------------------------------------------------------------------------------------------------	----

## **JEDWALI**

<b>Jed. 1.</b> Uteuzi sampuli wa mtabakisho na uteuzi sampuli usioratibiwa .....	53
<b>Jed. 2.</b> Usampulishaji maksudi.....	54
<b>Jed. 3.</b> Data iliyotokana na mijadala iliyoleta kosa .....	65
<b>Jed. 4.</b> Makosa kutokana na insha.....	68
<b>Jed. 5.</b> Sheng' katika chuo kikuu cha Maseno .....	72
<b>Jed. 6.</b> Matumizi ya vivumishi vinavyotatanisha .....	75
<b>Jed. 7.</b> Mikakati kulingana na maoni ya wanafunzi .....	79

## YALIYOMO

UNGAMO NA IDHINI .....	i
HATILINZI .....	ii
SHUKRANI.....	iii
TABARUKU .....	iv
IKISIRI.....	v
ABSTRACT .....	vi
VIFUPISHO NA AKRONIMU.....	vii
MCHORO.....	viii
JEDWALI.....	ix
YALIYOMO.....	x
<b>SURA YA KWANZA.....</b>	<b>1</b>
<b>UTANGULIZI.....</b>	<b>1</b>
1.1 Utangulizi .....	1
1.2 Usuli wa mada.....	1
1.3 Suala la Utafiti .....	7
1.4 Maswali ya utafiti.....	7
1.5 Madhumuni ya utafiti .....	8
1.6 Upeo wa utafiti.....	8
1.7 Misingi ya uteuzi wa mada ya utafiti .....	9
1.8 Misingi ya kinadharia.....	10
1.8.1 Nadharia ya Uchanganuzi wa Makosa .....	10
1.9 Hitimisho .....	15
<b>SURA YA PILI.....</b>	<b>16</b>
<b>TAHAKIKI YA MAANDISHI.....</b>	<b>16</b>
2.1 Utangulizi .....	16
2.2 Dhana ya Ngeli.....	16

2.2.1 Uainishaji wa Ngeli .....	19
2.2.1.1 Uainishaji Kimofolojia .....	20
2.2.1.2 Uainishaji Kisintaksia.....	22
2.2.1.3 Uainishaji Kisemantiki .....	28
2.3 Namna makosa yanavyodhihirika katika matini .....	30
2.3.1 Dhana ya Makosa .....	31
2.3.2 Nadharia ya Uchanganuzi wa Makosa .....	34
2.3.3 Uhakiki wa kazi mbalimbali zilizotumia nadharia ya Uchanganuzi wa Makosa .....	37
2.4 Changamoto za matumizi ya Ngeli katika lugha mbalimbali.....	38
2.5 Mikakati ya kukabiliana na matatizo ya kisarufi .....	39
2.5.1 Uzingativu wa Sarufi.....	40
2.5.2 Mkakati wa kutambua nomino ambazo hupatikana katika ngeli husika .....	41
2.5.3 Mkakati wa kuzingatia maana ya nomino husika .....	41
2.5.4 Mkakati wa kubaini kikundi cha nomino pamoja na sheria zake .....	42
2.5.5 Mkakati wa kuzingatia wingi wa maneno ya ngeli tofautitofauti.....	42
2.6 Nafasi ya Ngeli katika kuonyesha umilisi wa kiisimu wa lugha ya Kiswahili.....	42
2.6.1 Umilisi na utendaji wa kiisimu .....	43
2.7 Hitimisho .....	49
<b>SURA YA TATU.....</b>	<b>50</b>
<b>NJIA NA MBINU ZA UTAFITI .....</b>	<b>50</b>
3.1 Utangulizi .....	50
3.2 Muundo wa Utafiti .....	50
3.3 Eneo la utafiti.....	51
3.4 Kundi Lengwa.....	52
3.5 Usampulishaji .....	52
3.6 Ukusanyaji data.....	54
3.6.1 Muda wa ukusanyaji data .....	54

3.6.2 Utaratibu wa ukusanyaji data.....	55
3.6.3 Uthabiti na utegemezi wa vifaa vya utafiti. ....	55
3.7 Mbinu za ukusanyaji data.....	56
3.7.1 Utafiti wa Maktabani.....	56
3.7.2 Utafiti wa Nyanjani .....	57
3.7.2.1 Majadiliano katika vikundi maalum vya Kiswahili .....	57
3.7.2.2 Usaili / Dodoso.....	57
3.7.2.3 Uandishi wa Insha .....	58
3.8 Uchanganuzi na uwasilishaji wa data.....	60
3.8.1 Uchanganuzi wa kitathmini .....	60
3.8.2 Uchanganuzi wa kitakwimu.....	61
3.9 Changamoto za utafiti .....	62
3.10 Maadili ya utafiti .....	62
3.11 Hitimisho .....	63
<b>SURA YA NNE .....</b>	<b>64</b>
<b>UCHANGANUZI NA UWASILISHAJI WA DATA.....</b>	<b>64</b>
4.1 Utangulizi .....	64
4.2 Makosa yaliyodhihirika wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno walipotumia ngeli.....	64
4.2.1 Data iliyotokana na mijadala iliyoleta kosa.....	65
4.2.2 Makosa ya ngeli kutokana na insha.....	68
4.3 Changamoto za matumizi ya ngeli.....	72
4.3.1 Athari ya lugha ya Sheng’ .....	72
4.3.2 Changamoto ya vivumishi vinavyotatanisha .....	75
4.4 Mikakati ya kukabiliana na makosa ya kisarufi.....	78
4.5 Umilisi. ....	82
4.6 Hitimisho .....	83

<b>SURA YA TANO .....</b>	<b>85</b>
<b>MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO.....</b>	<b>85</b>
5.1 Utangulizi .....	85
5.2 Muhtasari wa Utafiti.....	85
5.3 Hitimisho la utafiti .....	87
5.4 Mapendekezo ya utafiti .....	88
5.5 Mawanda mapya ya utafiti.....	89
5.6 Taamuli.....	89
<b>MAREJELEO .....</b>	<b>90</b>
<b>VIAMBATISHO .....</b>	<b>100</b>
Kiambatisho 1: Barua kwa Mkuu wa Idara.....	100
Kiambatisho 2: Kibali cha Utafiti.....	101
Kiambatisho 3: Mwongozo wa Usahihishaji wa Insha:Alama za insha kutegemea idadi ya makosa.....	102
Kiambatisho 4: Mifano ya insha zilizosahihishwa katika Chuo Kikuu cha Maseno.....	103
Kiambatisho 5: Usaili: Mpangilio wa usaili kwa wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno .....	123
Kiambatisho 6: Mada za majadiliano ya vikundi maalum vya Kiswahili iliyorekodiwa kwa kila mwaka katika Chuo Kikuu cha Maseno.....	126
Kiambatisho 7: Idhini kutoka kwa mwanafunzi.....	127
Kiambatisho 8: Orodha ya uchunzaji.....	128

## **SURA YA KWANZA**

### **UTANGULIZI**

#### **1.1 Utangulizi**

Utafiti huu unachunguza matumizi ya ngeli miongoni mwa wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno. Sura ya kwanza imeshughulikia usuli wa mada, suala la utafiti, maswali ya utafiti, madhumuni ya utafiti, upeo, misingi ya uteuzi na nadharia ya utafiti. Usuli wa mada umegusia muumano katika lugha kwa jumla, chimbuko la sarufi na suala la ngeli kama kipengele muhimu cha sarufi kijumla na katika lugha za Kibantu, makosa yanayodhihirika, changamoto zinazojiri na kupendekeza mikakati ya kukabiliana na matatizo hayo ya kisarufi na umilisi wa lugha ya Kiswahili kwa jumla. Tahakiki ya maandishi imeonyesha mapengo yaliyopo katika utafiti wa awali na umuhimu wa kulishughulikia suala hili katika utafiti huu. Madhumuni ya utafiti huu yamewekwa wazi kwa mujibu wa kuonyesha na kudhihirisha vipengele vilivyoshughulikiwa kuufanikisha utafiti. Aidha, maswali ya utafiti yametoa msingi na mwelekeo wa kuchunguza matumizi ya ngeli miongoni mwa wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno. Upeo wa utafiti umeonyesha sehemu ambayo utafiti huu unajikita au mipaka yake. Nadharia ya Corder (1974) imetumiwa kama usukani wa kuuendesha utafiti huu. Kwa jumla, sura hii imetoa mwelekeo wa utafiti huu.

#### **1.2 Usuli wa mada**

Kitamaduni, muundo kimatini kuhusu maelezo ya muumano umejitokeza katika mifano iliyotolewa na wataalam anuwai kwa kurejelea muumano wa vivumishi kwenye nomino katika uana, nambari, muumano wa vitenzi na lugha zilizorejelewa ni Kilatini, Kiingereza na Kiswahili, Jespersen (1922), Broomfield (1933) na Lyons (1968). Masuala ya lugha na sarufi kwa jumla yana historia ndefu na mkufu huu tunaweza kuufuatilia kuanzia Ugiriki ya kale ambapo Plato na Aristotle walichangia pakubwa kwa mfumo wa mtaala na kuanzisha njia

bora ya uandishi wa sarufi, Howart (1999). Nao Ferguson (1964) na Barlow (1986) wakichangia maelezo hayo wanazungumzia kuhusu muumano katika baadhi ya lugha kama vile Kiarabu, Kiingereza na Kiswahili. Kwa mfano, wataalam hawa wanaeleza kuwa lazima kuwe na muumano kati ya kiwakilishi cha swali katika Kiingereza na nomino husika. Mawazo hayo yanauweka wazi msingi na mwanya wa kulitafitia suala la ngeli katika Chuo Kikuu cha Maseno kwa vile dhana ya ngeli haipatikani katika ombwe tupu bali ni kipengele cha sarufi kinacholeta muumano katika baadhi ya lugha za KiBantu hususan Kiswahili. Corder (1974) anakinzana na mawazo hayo kwa kupeana hatua ya kwanza ya kuchanganua makosa ya wanafunzi kwa kueleza kuwa ni muhimu kupata sampuli ya lugha ya wanafunzi husika. Kwa hivyo, wataalam hao wa awali walishughulikia dhana ya ngeli katika matini ya vitabu ilhali utafiti huu ni wa kipekee kwa vile unakusudia kuchunguza matumizi ya ngeli za Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Maseno, kwa kushughulikia lugha halisi ya wanafunzi, jambo ambalo halijafanywa na mtaalam yeyote yule.

Kila lugha ina njia yake ya kuyaainisha maneno ili kuuweka wazi usarufi wa lugha husika, kwa mfano kuna lugha zinazozingatia uana kama vile Kiingereza, Kifaransa na Kimaasai, Mukuria (1987). Ngeli ni msingi muhimu wa usarufi wa lugha za KiBantu hususan lugha ya Kiswahili. Kimsingi, nomino za KiBantu huhusu jozi nyingi za umoja na wingi. Ngeli hurejelea makundi au mpangilio wa maneno kimakundi kutegemea upatanisho wa kisarufi. Kila ngeli huwa na upatanishi wa kisarufi kulingana na kundi fulani la nomino, (Chomi, 2001). Ngeli katika lugha ya Kiswahili ni mojawapo ya vipengele vya lugha vinavyodhihirisha umilisi na utendaji wa kiisimu. Watumizi wa lugha huonyesha umilisi huu kupitia kwa stadi nne za lugha ambazo hudhihirisha utendaji, nazo ni; kusikiza, kusoma, kuzungumza na kuandika. Ngeli ni muhimu kwani ni njia mojawapo ya kuonyesha umilisi na utendaji wa lugha, Chomsky, (1957,1965). Kwa mujibu wa TUKI (1981), ngeli ni neno la Kihaya mojawapo ya lugha za Kibantu nchini Tanzania. Neno hili lina maana ya jinsi ya



kupanga aina za nomino au majina katika makundi kwa mfano KI-VI-, JI-MA- na kadhalika. TUKI (1990) wanawiana na maelezo haya na kueleza kuwa ngeli ni kundi moja la majina yaliyo na upatanisho wa kisarufi unaofanana na viambishi vya umoja na wingi. Jinsi anavyoshauri Chomi (2001), dhana ya ngeli inarejelea makundi ambamo nomino za Kiswahili hugawanywa. Kwa hivyo, kutafitia matumizi ya ngeli katika Chuo Kikuu cha Maseno kutauwezesha utafiti huu kubaini iwapo watafitiwa husika wamemakinika kwa kufanya makosa machache au ni hafifu kwa kufanya makosa mengi. Jambo ambalo litauwezesha utafiti kupima hali yao ya umilisi na utendaji wa kiisimu wa lugha ya Kiswahili.

Matumizi ya Kiswahili yana asili katika upwa wa Afrika Mashariki. Lugha hii imepata ufanisi wa kipekee miongoni mwa lugha za Kiafrika. Kama anavyodokeza Mohochi (2002), hivi karibuni kumekuwa na haja ya dharura ya kutumia Kiswahili sanifu katika teknolojia. Anaongezea kuwa:

“Hii imetokana na utetezi kwamba lugha ya Kiswahili kama lugha sambazi kote ulimwenguni inaaminika kuwa na upekee katika ufanikishaji wa mawasiliano, ubadilishaji wa maarifa, ujuzi na Teknolojia”.

Kwa hivyo, kuwa na umilisi na utendaji mwafaka wa sarufi ya lugha ya Kiswahili kunasaidia kuwasiliana kwa ufasaha na kuimudu lugha barabara.

Kuhusu dhana ya makosa, Lee (1957) anatoa uchanganuzi wa baadhi ya makosa ambayo yanapatikana katika kazi iliyoandikwa na wanafunzi wa Kislovaki. Kazi hiyo inajumuisha makosa ya uakifishaji, kuongezea au kuondoa vibainishi, hijai miongoni mwa mengine. Selinker (1972) akimwunga mkono Norrish (1987) anadokeza kuwa chanzo cha makosa katika lugha ya Kiingereza ni kutooana kwa nomino na viwakilishi vyake, nyakati zisizofaa; wingi na mpangilio usiofaa miongoni mwa mambo mengine. Ingawa makosa yanaweza kuwa ya aina moja, hali hii inatoa pengo kwa utafiti huu kwa vile muundo wa lugha ya Kiingereza

ni tofauti na wa Kiswahili ambao utafiti huu unakusudia kuangazia. Kwa hivyo, kimsingi, makosa huweza kuathiri hali ya umilisi na utendaji wa mtumizi wa lugha husika.

Dhana ya ngeli ni pana na tata kiasi cha kuwakanganya watumizi wengi wa Kiswahili. Hali hii imetokana na uainishaji wa ngeli ambao umezua matatizo miongoni mwa wanafunzi na walimu. Ngeli kama kipengele muhimu cha sarufi iliyo uti wa mgongo wa lugha ya Kiswahili bado ni suala nyeti katika viwango vyote vya elimu. Licha ya utata huo, hakujawahi kuwa na makubaliano kuhusu jinsi ngeli za Kiswahili zinavyofaa kuainishwa, Gromova (2008). Kwa hivyo ni dhahiri kuwa suala la ngeli lingali tatizo kuu kwa watumizi wengi wa lugha ya Kiswahili wakiwemo wanafunzi. Hata hivyo, mawazo ya Gromova (mtaje) yanakinzana na wataalam wengine kama Obuchi na Mukhwana (2010) ambao wanatoa suluhu kwa hali kama hiyo. Hivyo basi, huu ndio msingi wa utafiti huu unaonua kubainisha kosa ni lipi katika matumizi ya ngeli.

Changamoto hudhihirika pale ambapo tunaangazia sera, vitabu, programu na miradi mbalimbali. Kwa mfano nchini Malawi, shule za msingi hutumia vipindi katika redio vilivyoandaliwa katika lugha maalum za kienyeji. Haya huzua changamoto kwa watumizi wa Kiswahili kwa vile wanafunzi wengi huathiriwa na dhana ya ujumlishi pamoja na athari ya lugha ya kwanza asemavyo Selinker (1972). Pia nchini Kenya, sera ya serikali iliifanya lugha ya Kiswahili kutotumika sana, haya yalisababisha udunishaji wa lugha na kufanya watumizi wengi wa lugha hii kutoitilia maanani na vilevile hawakuweza kuzingatia vipengele muhimu vya sarufi kama vile viwakilishi vya ngeli. Hata hivyo, mnamo mwaka wa 1974, Rais wa kwanza wa Kenya hayati Mzee Jomo Kenyatta aliamrisha matumizi ya lugha ya Kiswahili katika bunge.

Kufikia mwaka wa 1981, tume ya Mackay ilipendekeza lugha ya Kiswahili ifundishwe na kutahiniwa kama somo katika mfumo wa elimu kuanzia shule za upili hadi Vyuho Vikuu.

Somo hili halikuwa la lazima hadi kufikia mwaka wa 1985 ambapo Kiswahili kilifanywa somo la lazima katika shule za msingi na za upili (Mbaabu, 1996). Ni wakati huo ambapo lugha hii ilitahiniwa kwa mara ya kwanza katika mtihani wa (K.C.P.E)- Kenya Certificate of Primary Education, katika mfumo wa 8-4-4.

Hatua zifuatazo zinaimarisha matumizi ya ngeli katika mazingira ya kielimu: Kwanza kabisa, silabasi mpya ya mwaka wa 2002 (KIE) imependekeza matumizi mapya ya ngeli kwa kuegemea kwa upatanisho wa kisarufi na kuonelea kuwepo kwa makundi kumi na mawili (12) ya ngeli. Aidha, silabasi hii inatusaidia kutambua usahihi na makosa ya ngeli. Isitoshe, programu mbalimbali kama mafundisho ya redio kupitia idhaa ya K.B.C kuhusu somo la Kiswahili kwa shule za msingi ni mojawapo ya hatua ambazo zimesaidia katika kuimarisha matumizi ya ngeli katika mazingira ya elimu. Katika Vyuvo Vikuu, kuna programu zinazofunzwa kama vile za Mofolojia, Sintaksia na Semantiki ambazo zinahusu masuala ya ngeli.

Radford (1997) anaeleza uhamisho dhima na kutuelekeza katika upatanisho wa kisarufi unaojikita katika ngeli. Kulingana na Massamba, Kihore na Hokororo (1999), ngeli huhusika na upangaji wa nomino kutegemea dhima ya hizo nomino.

Momanyi (2001), alitafitia lugha ya Sheng' na kueleza kuwa lugha ya Kiswahili imefika kwenye njia panda kwa vile watu hawawezi kupambanua matumizi bora ya lugha ni yapi. Hali hii ni muhimu kwa utafiti huu kwa maana maneno mengi ya Sheng' hayana makundi maalum ya nomino, jambo linalowatatiza watumizi wa lugha ya Kiswahili. Maoni ya Miguda (2002) na Ng'ong'a (2002) yanachangia hoja hii wanapoeleza kuwa wanafunzi wengi chuoni huwa na matatizo ya mazungumzo na maandishi huku wakitumia Sheng' zaidi kuliko lugha nyingine. Kulingana na Mirikau (2008), ngeli huainishwa kwa kuzingatia sifa za kimofolojia, kisemantiki, kisintaksia na kinambari. Hali hii ni muhimu katika utafiti huu kwa vile

huchangia utata wa dhana ya ngeli. Aidha, mawazo haya yanawiana na lengo la utafiti huu kwa vile ngeli ni kiungo muhimu kinachohitajika na kila mwanafunzi wa lugha ya Kiswahili kuanzia viwango vya chini vya elimu hadi vya juu ili kumpa usarufi na umilisi wa lugha hii. Wataalam hawa wanaongezea kuwa, wasioelewa ngeli hufanya makosa mengi ya kisarufi.

King'ori (2005) na Ambuyo (2007) wameshughulikia uhamisho dhima katika sentensi za Kiswahili na Luloogoli mtawalia. Kwa mfano Ambuyo (mtaje) anaelezea muumano wa viambishi vya ngeli kisintaksia ila alishughulikia lugha ya Kimaragoli, hata hivyo, mwelekeo wake wa upatanisho wa kisarufi kisintaksia ni muhimu sana kwa utafiti huu. Aidha, Lwidiko (2008) ameshughulikia uainishaji wa ngeli za Kihehe na Emmanuel (2009) amezichunguza ngeli za Kipangwa. Tafiti zao ni msingi muhimu kwa utafiti huu. Kulingana nao, dhana ya upatanisho wa kisarufi ni muhimu kwa vile walizingatia kigezo cha Mofu-Sintaksia. Opunde (2010) naye ameshughulikia matumizi ya riwaya katika ufundishaji wa ngeli za Kiswahili katika Shule za Upili Nchini Kenya, miongoni mwa wengine. Maoni ya Opunde (mtaje) ni kwamba riwaya za Kiswahili zitumike katika kufunza mada za sarufi. Tafiti za wataalam hawa kwa ujumla ni mikakati ya kukabiliana na matatizo yanayowakumba watumizi wa lugha husika. Hata hivyo, utafiti huu unatofautiana na tafiti za awali kwa vile unalenga Chuo Kikuu cha Maseno ilhali kwa mfano utafiti wa King'ori (2005) ulifanywa katika Chuo Kikuu cha Nairobi, Ambuyo (2007) naye alifanya katika Chuo Kikuu cha Kenyatta huku Opunde (2010) akiufanya utafiti wake katika Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro. Kwa hivyo, tofauti na hao, utafiti huu unachunguza matumizi ya ngeli miongoni mwa wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno kwa misingi kuwa, dhana ya ngeli ni pana na tata. Aidha, kuna ngeli nyingine ambazo hutatiza na kuzua changamoto kwa watumizi wa lugha ya Kiswahili. Chuo Kikuu cha Maseno kilitumika kama kiwakilishi cha kiwango cha juu cha elimu.

Kwa hivyo, inakisiwa kuwa wanafunzi wengi hujiunga na Vyuo Vikuu huku matumizi ya ngeli yakisalia kuwa hafifu. Licha ya juhudi na mikakati ambayo imewekwa na wataalam anuwai, bado kuna changamoto kadhaa ambazo huizingira dhana hii ya ngeli, pengo ambalo utafiti huu unanua kuliziba. Utafiti huu unanua kuchunguza matumizi ya ngeli za Kiswahili kwa kubaini makosa, kujadili changamoto na kupendekeza mikakati ya kukabiliana na matatizo hayo ya kisarufi na kuinua umilisi wa lugha ya Kiswahili kwa kuangazia wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno kama kiwakilishi cha Vyuo Vikuu nchini.

### **1.3 Suala la Utafiti**

Msingi muhimu wa usarufi wa lugha za Kibantu ni ngeli kwa vile ni nguzo kuu katika kubainisha umilisi na utendaji wa kiisimu katika baadhi ya lugha za Kibantu hususan Kiswahili. Ngeli ni makundi ambamo nomino za Kiswahili hugawanywa. Ngeli zisipotumiwa sahihi huzua dosari kisarufi. Maumbo ya ngeli za Kiswahili yamewekwa tofauti kulingana na wataalam mbalimbali. Jambo hili huzua utata na matatizo kwa watumizi wengi wa Kiswahili wakiwemo wanafunzi. Wanafunzi wengi wa lugha ya Kiswahili hutatizika na matumizi ya ngeli kwa sababu ya upana na utata wake. Juhudi tele na mikakati imewekwa ili kutatua tatizo hili lakini bado kuna vikwazo ambavyo vinazuia matumizi mwafaka ya ngeli na kudunisha umuhimu wa kipengele hiki cha sarufi. Licha ya umuhimu huo, watumizi wengi wa lugha ya Kiswahili hasa wanafunzi wangali wanatatizika kimawasiliano. Kimahsusuni, utafiti huu unalenga katika kuzichunguza ngeli ambazo hutatiza na changamoto zake kwa kuangazia lugha halisi ya wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno.

### **1.4 Maswali ya utafiti**

Maswali yafuatayo ndiyo yaliyouongoza utafiti huu;

- (i) Ni makosa gani yanayotokea katika matumizi ya ngeli miongoni mwa wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno?

(ii) Ni changamoto gani zinazowakumba wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno wanapotumia ngeli?

(iii) Ni kwa namna gani matatizo haya ya matumizi ya ngeli yanaweza kukabiliwa miongoni mwa wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno na kuinua umilisi wao wa kiisimu wa lugha ya Kiswahili?

### **1.5 Madhumuni ya utafiti**

Utafiti ulichunguza matumizi ya ngeli miongoni mwa wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno nchini Kenya. Ili kufikia azma hii, utafiti ulizingatia madhumuni mahsusi yafuatayo:

- i) Kubaini makosa yanayotokea wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno wanapotumia ngeli.
- ii) Kujadili changamoto zinazotokea wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno wanapotumia ngeli.
- iii) Kupendekeza mikakati ya kukabiliana na matatizo haya ya kisarufi miongoni mwa wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno na kuinua umilisi wao wa kiisimu wa lugha ya Kiswahili.

### **1.6 Upeo wa utafiti**

Utafiti unalenga kuchunguza matumizi ya ngeli miongoni mwa wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno. Chuo hiki kiliteuliwa kimaksudi kulingana na ile hali ya mtafiti kuweza kutangamana na wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo hicho. Ni katika harakati hizo za kuwasiliana nao ambapo mtafiti aliweza kutambua pengo kuhusu suala la utafiti ambalo ni dhana ya ngeli. Aidha, wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno wamechaguliwa kama kiwakilishi cha kiwango cha juu cha elimu. Sababu kuu ikiwa kwamba hapa ndipo mahali ambapo walimu wa lugha hii huandaliwa na inatarajiwa wawe wameimudu ngeli

barabara, kisintaksia, kimofolojia na kisemantiki. Upeo kinadharia unajikita katika mihimili mitano ya uchanganuzi wa makosa kwa mujibu wa (Corder 1974). Mihimili hiyo ni kukusanya sampuli ya lugha ya wanafunzi, kutambua, kuainisha, kuelezea na kutathmini makosa. Upeo kulingana na ukusanyaji wa data utajikita katika uandishi wa insha, majadiliano na usaili.

### **1.7 Misingi ya uteuzi wa mada ya utafiti**

Utafiti huu ulikuwa na lengo la kuchunguza jinsi wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno wanavyotumia ngeli, changamoto zinazotokea, makosa wanayoyafanya na mikakati ya kukabiliana na matatizo hayo ya kisarufi. Hii ni kwa sababu ngeli ni mojawapo ya vipengele muhimu katika kuimilisi lugha ya Kiswahili. Umilisi wa ngeli ni muhimu sana katika ufahamu wa sarufi kwa jumla. Ukosefu wa ngeli katika lugha ya Kiswahili ni mithili ya jifya moja kukosekana wakati wa mapishi. Ngeli huhusika na upangaji wa nomino kutegemea dhima ya hizo nomino kama wanavyodokeza Massamba, Kihore na Hokororo na (1999). Aidha, kwa vile ngeli ni suala tata na pana, suala hili lilituuliwa kwa misingi kuwa mtafiti aliweza kuwasiliana na kutagusana na wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno. Tajriba za mtafiti na kule kutagusana nao ndiko kuliipelekea ari ya kulitafitia suala la ngeli. Isitoshe, Gromova (2008) anaeleza kwamba hakujawahi kuwa na makubaliano jinsi nomino za Kiswahili zinavyofaa kuainishwa. Hata hivyo, utafiti huu unanua kutoa suluhu kwa hali kama hii.

Matokeo ya utafiti huu yalikuwa muhimu kwa vile yamedhihirisha kwamba suala la utafiti lilifaa kutafitiwa. Utafiti umedhihirisha bayana kuwa dhana ya ngeli ni muhimu kwa vile ni mojawapo ya vipengele muhimu vinavyoweza kuzua umilisi na utendaji wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili. Pia, utafiti umeonyesha hali ya umilisi na utendaji wa lugha ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi hao ijapo kulikuwa na makosa ya hapa na pale. Aidha,

changamoto zimedhihirika wazi. Matokeo ya utafiti huu huenda yakawasaidia wanafunzi wa viwango mbalimbali kwa vile yameweka wazi namna ya kutumia ngeli katika kuonyesha umilisi na utendaji wa kiisimu wa lugha ya Kiswahili. Mwisho, utafiti umependekeza mikakati ambayo inaweza kutumiwa kukabiliana na matatizo haya ya kisarufi katika lugha ya Kiswahili kwa jumla.

## **1.8 Misingi ya kinadharia**

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Uchanganuzi wa Makosa, Corder (1974) ambayo inajikita katika muumano katika uasili wa lugha kisarufi. Nadharia hii ndiyo iliyokuwa mwafaka zaidi kwa vile inaegemea katika kuchanganua makosa.

### **1.8.1 Nadharia ya Uchanganuzi wa Makosa**

Nadharia hii iliasisiwa na Corder (1967) na kuendelezwa naye mwenyewe mnamo mwaka wa 1974. Kimsingi, nadharia hii ina historia ndefu lakini kimatumizi kama chombo kuhusu kujifunza lugha, ilianza kutumiwa mnamo miaka ya sitini. Nadharia hii ni muhimu kwa utafiti huu kwa vile inajikita katika kuchanganua makosa kisarufi. Nadharia ya Uchanganuzi wa Makosa imetumiwa na wataalam wengi kama vile; Richards (1974), Taylor (1980), Felix (1981), Pavesi (1986), Santos (1987), Bardovi – Harlig na Bofman (1989), Roos (1990), Lennon (1991) na Selinker (1992) miongoni mwa wengine. Maoni ya wataalam hawa ni muhimu kwa utafiti huu kwa maana yanaangazia makosa ya wanafunzi. Kwa mfano, Bardovi-Harlig na Bofman (1989) walichunguza wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Indiana waliopita na waliofeli mtihani mmojawapo wa mingine ya kuandika insha. Walitambua kuwa, kundi la waliopita lilikuwa na makosa machache kijumla katika kiwango cha kimofolojia kuliko katika kiwango cha kisintaksia. Kimsingi, maoni ya wataalam hawa ni kwamba wanafunzi hufanya makosa kimaongezi na kimaandishi lakini katika viwango tofauti tofauti vya sarufi. Mawazo haya yanaafikiana na utafiti huu kwa vile unalenga kimahususi,



kubaini makosa yanayofanywa na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Maseno wanapotumia ngeli miongoni mwa malengo mengine. Kimsingi, kulingana na Corder (1974), hatua zifuatazo ndiyo mihimili ya nadharia hii:

- 1.) Kukusanya sampuli ya lugha ya wanafunzi.
- 2.) Kutambua makosa.
- 3.) Kuainisha makosa.
- 4.) Kuelezea makosa.
- 5.) Kutathmini makosa.

Hii ni nadharia inayochunguza makosa katika sentensi. Bloom (1970) kwa mfano anaeleza kuwa si wanafunzi wanaojifunza lugha ya pili pekee ambao hufanya makosa bali, watoto wadogo wanaojifunza lugha ya kwanza pia hufanya makosa. Inadaiwa kwamba kuna baadhi ya wanafunzi ambao hufanya makosa katika maongezi na wala si katika maandishi, (Rod, 1995). Hata hivyo, nadharia hii inadai kuwa wanafunzi hufanya makosa katika ufahamu na kimatumizi. Hivyo basi, utafiti huu uliwahusisha wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno kwa kuwarekodi wakijadiliana katika vikundi maalum vya Kiswahili, kuwanasa huku wakisailiwa na uandishi wa insha. Haya yalikuwa muhimu kwa maana utafiti ulikusudia kupata data ya kimaongezi na kimaandishi. Nadharia hii imekuwa muhimu katika utafiti huu kwa vile uliazimia kubaini makosa yanayofanywa na wanafunzi hao wanapotumia ngeli. Nadharia hii ni faafu kwa vile hujumuisha hatua tano ambazo ni teneti au mihimili yake. Nayo ni ; kukusanya sampuli ya lugha ya wanafunzi, kutambua, kuainisha, kuelezea na kufafanua makosa katika lugha ya mwanafunzi, (Corder 1974).

Hatua ya kwanza katika Uchanganuzi wa Makosa kulingana na Corder (1974) ni kuamua ni sampuli zipi za lugha ya wanafunzi zitakazotumiwa kwa uchanganuzi na jinsi ya kuzikusanya sampuli hizi. Mhimili huu ulikuwa muhimu kwa utafiti huu kwa vile uliwezesha kupata

sampuli mahususi ya 54 kutoka kwa jumla ya wanafunzi 540 wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno. Kwa kutumia usampulishaji wa vikoa, usampulishaji sahili usioratibiwa na usampulishaji kimfumo, utafiti uliweza kupata sampuli faafu ya kurekodi na kuandika insha. Mhimili huu uliufaa sana utafiti huu kwa vile data ilikusanywa kwa kurekodi kwa tepurekoda majadiliano ya vikundi maalum vya Kiswahili pamoja na usaili, kisha mada za insha zikapeanwa kulingana na kila mwaka na mwishowe zikasahihishwa.

Sampuli hizi zilikusanywa kwa wakati mmoja ili kuweza kulinganisha umilisi na utendaji wa kiisimu wa wanafunzi wa mwaka wa kwanza, wa pili, wa tatu na wa nne wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno. Hiki kilikuwa kiwakilishi cha Vyuo Vikuu vingine. Mtaalamu huyu (Corder, mtaje) katika makala yake ya 1981, anadai kuwa kuna mambo mengi yanayofaa kutiliwa maanani na ambayo husababisha utofauti katika lugha ya wanafunzi. Nayo ni; yaliyomo katika mada, mazingira ya kujifunza lugha, chombo cha kuwasilisha lugha-mazungumzo au maandishi miongoni mwa mengine. Kwa hivyo, katika muktadha huu, utafiti wetu ulijikita katika lugha ya mazungumzo (usaili na mijadala ya mihadhara) na maandishi (insha) ili kupata data kutokana na sampuli faafu.

Mhimili wa pili ni wa kutambua makosa. Mhimili huu unadai kuwa, lugha ya wanafunzi ikishakusanywa, makosa yanafaa kudondolewa. Kwa hivyo, ni muhimu kuamua ‘makosa’ ni yapi na kutambua mpangilio mwafaka wa kuyatambua makosa hayo. Kwa mujibu wa Corder (1974) makosa yanafafanuliwa kama kupotoka kutoka kwa hali sanifu au kutozingatia kaida za lugha husika. Katika muktadha huu, utafiti wetu ulikusanya data kwa kuwapa wanafunzi mada za insha kuandikia na kuzisahihisha ili kuyadondoa makosa ya ngeli. Vilevile, tepurekodi za usaili na mihadhara ya kawaida ya Kiswahili zilisikizwa na kunukuliwa ili kuweza kuyadondoa makosa. Haya yalitekelezwa kwa kulinganisha data iliyokusanywa na ngeli za Kiswahili sanifu kwa mujibu wa ngeli zilizopendekezwa na silabasi mpya (KIE,

2002), pamoja na zile za wataalam kama Mgullu (1995, 1999) na Habwe na Karanja (2004). Kwa hivyo, lugha Sanifu ya Kiswahili ndicho kigezo : vigezo vya usanifu wa lugha vikiwa kimofolojia, kisintaksia na kisemantiki miongoni mwa vingine.

Mhimili wa tatu wa kuainisha makosa unahusu kulinganisha makosa ya wanafunzi. Mhimili huu unajikita katika kupima umilisi wa kiisimu kwa vile tuliweza kulinganisha makosa yaliyofanywa na wanafunzi wa viwango vya chini na vya juu miongoni mwa wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno. Mhimili huu unadai kuwa makosa huweza kuainishwa kwa kuacha au kuongezea kiambishi fulani katika maandishi au matamshi miongoni mwa mengine. Hatua hii ilikuwa muhimu kwa utafiti huu kwa vile wanafunzi waliweza kuacha au kuongezea viambishi fulani vya ngeli katika maandishi pamoja na kutozingatia upatanisho wa kisarufi kimaongezi na kimaandishi. Kwa mfano ;

\*1.Msamiati mpya ya Kiswahili.

√2. Msamiati mpya wa Kiswahili.

Mfano huu unatodokezea waziwazi kuwa wanafunzi walikuwa na viwango vya umilisi vilivyotofautiana kutegemea idadi ya makosa.

Mhimili wa nne ni wa kuelezea makosa. Mhimili huu unadai kuwa baada ya kutambua na kuainisha makosa, ni bora kuchukua hatua ya kujaribu kuyaeleza makosa hayo. Kuelezea makosa ni kule kutambua asili ya kosa na kwa nini kosa hilo lilifanywa. Mhimili huu ulikuwa muhimu kwa utafiti huu kwa vile ulituongoza katika kuelezea jinsi ya kutambua hali zinazosababisha kuweza kuielewa lugha ya pili husika ambayo katika muktadha huu ni Kiswahili. Wataalam kama Richards (1971), Selinker (1972) na Corder (1974), wanadai kuwa chanzo cha makosa huweza kuwa ; ujumlishaji, athari ya lugha ya kwanza, kutozingatia kanuni mwafaka, kutokamilisha kanuni na mielekeo ya uongo au mibaya kuhusu lugha

husika. Haya ni muhimu kwa utafiti huu kwa vile yanasaidia kutambua asili ya makosa ya ngeli na kwa nini yalikuwa yakifanywa, kisha kuusaidia utafiti kupendekeza mikakati ya kukabiliana na matatizo hayo ya kisarufi. Akiongezea mawazo ya wataalam hao, Taylor (1986) anadai kwamba chimbuko la kosa huweza kuwa la kiisimujamii, kisaikolojiaisimu, kiasili sentensi ilivyoundwa na mtumizi wa lugha. Mathalan, makosa ya kiisimujamii huhusu uwezo wa mwanafunzi kuweza kukabili lugha yake kulingana na muktadha wa jamii ambapo lugha ya Sheng' inaweza kuwa kama mfano hapa.

Mhimili wa tano unahusu kutathmini makosa. Kulingana na Corder (1974), mhimili huu hujikita katika kutathmini makosa na kutambua makosa haya yana athari zipi kwa watu husika. Athari hizi ndizo ambazo zilitufaa sana wakati wa kutoa mapendekezo yetu. Tukiangazia kwa mfano data ya uandishi wa insha, mhimili huu ulikuwa muhimu kwa vile ulitusaidia kupata mikakati ya kuwasaidia wanafunzi kuepukana na makosa hayo ya kisarufi mintaarafu ngeli. Aidha, makosa ya wanafunzi, kimatamshi na kimaandishi ndiyo yaliyotwezesha kupata kigezo cha kupimia kiwango cha umilisi na utendaji wao wa kiisimu wa lugha ya Kiswahili.

Kulingana na Richards (1986) nadharia ya uchanganuzi wa makosa imetumiwa kutambua mikakati ambayo wanafunzi hutumia katika kujifunza lugha, kufuatilia sababu za makosa ya wanafunzi, kupata mambo kuhusu makosa ya kawaida katika kujifunza lugha au kutayarisha nyenzo za kufunzia. Aidha, Michaelides (1990) anaeleza kuwa nadharia ya uchanganuzi wa makosa ni utaratibu maalum wa kuchanganua makosa ya wanafunzi ambao ni wa thamani sana kwa walimu, wanafunzi na watafiti. Anaongezea kuwa kwa walimu, ni njia mwafaka ya kuweza kutoa picha faafu ya uelewa na umilisi na utendaji wa wanafunzi katika lugha husika.

Kimukhtasari, nadharia ya Uchanganuzi wa Makosa imependekezwa na baadhi ya wataalam huku wengine wakidai kuwa imepoteza mashiko kwa sababu ya udhaifu wake wa

kuyaangazia makosa. Kwa mujibu wa utafiti huu, mihimili hii inatosheleza kazi hii na kwa hivyo udhaifu huo haujitokezi hapa

## **1.9 Hitimisho**

Kwa jumla sura hii ilijikita katika utangulizi ulioweka msingi wa utafiti wote kwa mapana na marefu. Ilishughulikia usuli wa utafiti kwa kutalii dhana ya ngeli kama kipengele muhimu cha sarufi katika lugha za Kibantu, kikiwemo Kiswahili. Suala la utafiti limeonyesha bayana umuhimu wa ngeli za Kiswahili kama mojawapo wa vipengele muhimu vya sarufi vinavyoonyesha umilisi na utendaji wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili. Maswali ya utafiti yalikuwa kama haipotesia yetu ya kutambua changamoto, makosa ya ngeli na kupendekeza mikakati ya kukabiliana na matatizo hayo ya kisarufi. Nayo madhumuni ya utafiti yalichangia pakubwa katika kutuwekea ngazi imara ya mchango wa ngeli kama kipengele muhimu cha kudhihirisha muktadha wa umilisi na utendaji wa Kiswahili kwa kulenga wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno, misingi ya uteuzi wa mada ilisimama wima na kudhihirisha kuwa utafiti ulikuwa ukifanywa kwa nia ya kuweza kulijaza pengo kuhusu matumizi ya ngeli kwa kuangazia umilisi na utendaji wa wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno. Mipaka ya utafiti iliwekwa wazi na upeo wa utafiti huku nadharia ya Uchanganuzi wa makosa ikitumiwa kama dau letu la usafiri, kudhihirisha ngeli zinazotatiza na changamoto zake katika Chuo Kikuu cha Maseno.

## SURA YA PILI

### TAHAKIKI YA MAANDISHI

#### 2.1 Utangulizi

Sura hii inatoa tahakiki mbalimbali kuhusu mada ya utafiti pamoja na msingi wa madhumuni ya utafiti kwa kurejelea na kujadili changamoto za matumizi ya ngeli katika lugha mbalimbali, dhana ya ngeli, uainishaji wa ngeli, namna makosa yanavyodhihirika katika kazi mbalimbali, nadharia ya Uchanganuzi wa Makosa, mikakati mbalimbali ya kukabiliana na makosa haya ya kisarufi na nafasi ya ngeli katika kuonyesha umilisi wa lugha ya Kiswahili. Tahakiki hizi zimechunguzwa kama njia ya kubainisha pengo lililoko katika utafiti wa awali.

#### 2.2 Dhana ya Ngeli

Sehemu hii imetoa maoni ya wataalam mbalimbali kuhusu dhana ya ngeli kama njia ya kuelewa suala la utafiti na kudhihirisha wazi umuhimu wake katika utafiti huu. Dhana ya ngeli imezishughulisha kalamu nyingi. Dhana hii inajikita katika muumano katika lugha anuwai za binadamu kama vile Kilatini, Kifaransa, Kiingereza na Kiswahili miongoni mwa lugha nyingine (Jespersen 1922 ; Bloomfield, 1933 ; Lyons, 1968). Ngeli ni dhana ambayo haipatikani katika ombwe tupu bali hujikita katika sarufi iliyowekewa msingi na wataalam wakongwe kama Aristotle na Plato katika Ugiriki ya kale, Howart (1999). Kimsingi, Guthrie (1967) anaihusisha dhana ya ngeli na uhusiano uliopo kati ya lugha ya Kiswahili na lugha nyingine za KiBantu. Anasema kuwa lugha za KiBantu zina mpangilio wa majina katika makundi au ‘ngeli’. Istilahi ngeli imechukuliwa kutoka lugha ya Kihaya (Tanzania). Katika lugha ya Kihaya neno **ngeli** lina maana ya aina ya kitu. Kulingana na *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (1981 uk. 213), ngeli ni:

“Utaratibu wa taaluma ya Sarufi ya lugha katika kupanga aina za majina (nomino) katika makundi kutegemea sifa mahsusi kwa mfano Ki-Vi-, Ji-Ma na kadhalika”

Mukuria (1987) anaafikiana na Guthrie (1967) katika tasnifu yake anapoulinganisha mpangilio wa ngeli za Kiswahili sanifu na Kikuyu cha Kiambu. Ametambua kuwa kuna uwiano wa karibu sana baina ya lugha hizo kwa sababu ya upatanisho wa kisarufi. Hata hivyo, hakuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya lugha mbili. Kwani hutofautiana katika matumizi ya ngeli kutegemea nomino husika. Mawazo ya wataalam hao yanawiana na ya Ferguson na Barlow (1988). Aidha, *Kamusi ya Isimu na Lugha* (1990) inachangia mawazo hayo kwa kueleza kuwa ngeli ni kundi moja la majina yaliyo na upatanisho wa kisarufi unaofanana na viambishi vya umoja na wingi vinavyofanana. Ujuzi wa ngeli ni muhimu kwa mwanafunzi yeyote yule wa Kiswahili kwa sababu ni nguzo kuu katika kutambua umilisi na utendaji wa maneno katika lugha husika kama anavyoshauri Mbaabu (1995).

Kwa mujibu wa Chomi (2001), dhana ya ngeli inarejelea makundi ambamo nomino za Kiswahili hugawanywa. Massamba, Kihore na Hokororo(2001) wanatilia mkazo mawazo haya kwa kueleza umuhimu wa dhana ya sentensi kuwa na upatanisho wa kisarufi mintaarafu ngeli. Mukuria (2002), anaeleza kuwa nomino katika Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu huainishwa kwa kuzingatia mfumo wa ngeli. Mtaalam huyo anaendelea kusema kuwa huwezi kushughulika sarufi bila kurejelea ngeli katika lugha hizo.

*Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2004 uk. 304) inaeleza ngeli kama “kundi la nomino katika baadhi ya lugha lenye sifa zinazofanana kisarufi”

Habwe na Karanja (2004), wanaeleza kuwa ngeli ni namna ya kuweka nomino katika makundi yanayofanana au yanayowiana. Kulingana nao, ngeli ni jamii ya nomino zenye mabadiliko ya aina moja kwenye vitenzi, vivumishi na pia viwakilishi. Ingawa maoni haya ni ya kweli kwa namna fulani lakini tunatofautiana nao kwa upande mwingine kwa vile kuna nomino fulani ambazo zinaweza kuwa na viambishi vinavyofanana ilhali si za kikundi

kimoja. Kwa mfano kiboko (**mjeledi**) huwekwa katika ngeli ya KI-VI ilhali kiboko (**mnyama**) huwekwa katika ngeli ya A-WA.

Upatanisho wa kisintaksia huwa hasa wa vitenzi kwa sababu kitenzi ni kipashio cha lazima katika sentensi ya Kiswahili. Kazi za wataalam kama vile King'ori (2005) zinasititiza uhamishaji wa maumbo. Kwa mfano, ameshughulikia uhamisho katika sentensi ya Kiswahili kwa kujikita katika vipengele mahususi vya sarufi kama viulizi na viwakilishi vinavyohusu upatanisho wa sarufi. Hii ni kwa sababu, inaaminika kuwa, wanafunzi wengi hurithi makosa ya ngeli kutoka katika shule za msingi na upili. Matokeo ya mitihani ya kitaifa nchini Kenya ya darasa la nane (KCPE) na kidato cha nne (KCSE) ya miaka ya 2006 hadi 2008, KNEC, (2006) yameonyesha bayana kushuka kwa alama wanazopata wanafunzi katika somo la Kiswahili. Sababu mahususi zilizotolewa na watahini ni kwamba wanafunzi huandika insha duni bila kuzingatia misingi ya ngeli na sarufi kwa jumla. Matatizo haya huwaandama wanapoenda katika viwango vya juu vya elimu.

Ambuyo (2007) ameshughulikia uhamisho dhima katika sentensi za Luloogoli huku vipengele vya ngeli vikidhihirika wazi kisintaksia. Mawazo haya ya Ambuyo (mtaje) yanawiana na ya Opunde (2010) ambaye ameshughulikia umuhimu wa kutumia Riwaya katika ufundishaji wa Ngeli za Kiswahili katika shule za upili nchini Kenya. Tahakiki za wataalam hawa zimeufaa utafiti huu. Mianya iliyoachwa na wataalam hawa ni kwamba hawakushughulikia makosa na changamoto zinazowakumba wanafunzi wa Kiswahili wa Vyuo Vikuu hususan Chuo Kikuu cha Maseno kama vile utafiti huu ulivyoniua kufanya. Ni muhimu kwa hivyo kujadili namna aina mbalimbali za uainishaji wa ngeli unavyozingatiwa kwa vile hali hii inachangia katika utata wa matumizi ya ngeli.



### 2.2.1 Uainishaji wa Ngeli

Sehemu hii inajadili uainishaji wa ngeli ambapo maoni ya wataalam mbalimbali kuuhusu yametolewa. Kulingana na TUKI (1981), kuainisha ni kupanga katika makundi mbalimbali. Katika muktadha huu, kuainisha ngeli ni kuweka nomino katika makundi mbalimbali kutegemea upatanisho wa kisarufi. Frawley (2003), akiyahusisha mawazo ya Mukuria (2002) anadai kuwa kila lugha huwa na njia yake ya kuainishia nomino ili kuweka wazi usarufi wa lugha husika. Frawley (mtaje) anaongezea kuwa nomino katika lugha za Kibantu kikiwemo Kiswahili huainishwa kwa kuzingatia mfumo wa ngeli.

Upangaji wa nomino katika ngeli umewahi kupitia katika mikondo tofauti, KIE (2006). Ngeli za Kiswahili zimeainishwa kutegemea maumbo ya nomino, matumizi ya nomino katika sentensi na maana na fahiwa tofauti za nomino. Lwidiko (2008) ameshughulikia dhana ya ngeli katika Kihehe lakini ametumia uainishaji wa Kimofolojia na Kisintaksia kwa pamoja. Amezichanganya mbinu zote mbili kwa kutumia mianzo ya nomino na pia matumizi ya viambishi vya ngeli pamoja. Amezigawa ngeli za Kihehe katika makundi kumi na manane. Uainishaji huu ni msingi muhimu kwa utafiti wetu kwa vile umetumia kigezo cha kisarufi katika (Mofu-sintaksia) kutafitia upatanisho wa ngeli katika lugha hiyo ya Kihehe. Alipata kuwa muumano wa viambishi ni muhimu katika kuangazia dhana ya ngeli. Hata hivyo, kule kuchanganya vigezo viwili ni tofauti na utafiti huu. Katika utafiti huu, tumejikita katika kigezo cha Sintaksia kwa vile kinatuelekeza katika kuzingatia ngeli na miundo ya sentensi ambapo tunazingatia upatanisho wa kisarufi. Gromova (2008) anachangia kwa kusema kuwa hadi sasa watumiaji wa Kiswahili hawajakubaliana kuhusu viambishi-patanishi vilivyo sawa na viambishi awali vya nomino (ling. Jicho jeusi jingine, nyumba nyeusi nyingine) ama viambishi-patanishi tofauti (ling. Jicho jeusi lingine, nyumba nyeusi zingine). Haya yanatudokezea tu utata wa suala la ngeli.

Emmanuel (2009) katika utafiti wake amechunguza ngeli za Kipangwa. Anadai kuwa dhana ya ngeli ni tata sana katika lugha za Kibantu. Anaendelea kusema kwamba hakujawahi kuwa na makubaliano kuhusu jinsi ngeli zinafaa kuainishwa. Anaongezea kuwa matumizi ya uainishaji wa kimofolojia, kisintaksia na kisemantiki katika upekee wa kila mojawapo umezua matatizo mengi. Madai haya ni msingi muhimu kwa utafiti wetu ambao utajikita katika kuchunguza makosa na changamoto zinazotokea wanafunzi wa kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno wanapotumia ngeli. Mtaalam huyo anaibuka na makundi kumi na manane ya ngeli za Kipangwa. Kulingana naye uainishaji wa kimofolojia na kisintaksia kwa pamoja ndio mwafaka zaidi. Madai yake yanakubaliana na yale ya Lwidiko. Uainishaji wao umeufaa utafiti huu, kwa vile utafiti wetu unaangazia upatanisho wa kisarufi ambao ni wa kisintaksia.

Uainishaji wa ngeli za nomino umegawanywa katika aina tatu kuu zifuatazo:

### **2.2.1.1 Uainishaji Kimofolojia**

Haya ni maelezo kuhusu uainishaji wa ngeli kwa kutegemea mianzo ya nomino. Hali hii ni muhimu kwa utafiti huu kwa vile inaangazia msingi wa utata wa matumizi ya ngeli. Kigezo hiki kimetumiwa na wataalam mbalimbali wakiwemo wale wa kimapokeo kama vile Krapf (1882), Burt (1917), Broomfield (1931), Ashton (1944) na Welmers (1973). Wanasarufi wanaozingatia kigezo hiki huyapanga makundi ya ngeli katika jozi za umoja na wingi. Mawazo ya wataalam hawa yanawiana na ya Guthrie (1967) ambaye anadai kuwa viambishi vya awali vya ngeli za majina ya Kibantu hudhihirika katika upatanisho wa kisarufi. Kwa mfano;

#### *Kiswahili*

M - wa mtu – watu

M - mi mti –miti

#### *Kikuyu*

m - a mundu - andu

m – mi muti -miti

Anaongezea kuwa sifa hii haipatikani katika lugha za Kiniloti kama inavyoonekana katika mifano hii:

Lugha za Kibantu

Kiswahili: Kitabu hiki ni kikubwa

Kikuria: Egetabo keno nekenene

Ekegusii: Egetabo eke nekenene

Lugha za Kiniloti

Dholuo: Buku ni duong'

Kimaasai: O kitabu ni

Kuna baadhi ya wataalam waliotafitia ngeli katika lugha za Kibantu ambao wamezingatia kigezo hiki. Kwa mfano, Mukuria (1987) alishughulikia ngeli za Kikuyu cha Kiambu kwa kutumia kigezo hiki na akapata ya kuwa kulikuwa na uwiano wa karibu sana baina ya lugha hii na Kiswahili Sanifu. Jambo hili ni muhimu kwa utafiti huu kwa vile huchangia katika kuivuruga sarufi ya lugha ya Kiswahili kwa vile huzua kutokea kwa makosa ya sarufi hususan ngeli kwa sababu ya athari ya lugha ya kwanza na ujumulishaji. Marani (1994) akiiunga mkono hoja hii ametafitia athari za Kikabarasi katika kujifunza Kiswahili Sanifu na vipengele vya uzingativu wa ngeli kimofolojia vimedhihirika katika utafiti wake.

Huu ndio uainishaji ulioendelezwa na Mgullu (1995, 1999). Akiyachangia mawazo ya wataalam hawa, Chomi (2001) anasema kuwa uainishaji huu umejikita katika viambishi vya mianzo ya nomino hizo. Mukuria (2002) akiongezea maoni haya anadai kwamba uchunguzi uliofanywa kuhusu matatizo ya kisarufi yanayowakumba wanafunzi wa Kiswahili umeonyesha baadhi ya athari zinazosababishwa na uzingativu wa viambishi vya nomino katika kufundisha ngeli (Ruo, 1991; Mazrui, 1991; Mukuria 1991 na Ipara 1999). Anatumia mfano wa Ruo aliyetoa mifano kuhusu baadhi ya majina ya wanyama kama vile, 'kiboko' na 'kifaru' iliyoza kosa lifuatalo:

- a) 'Kifaru kikubwa kimetokea mtoni.' Badala ya

b) ‘Kifaru mkubwa ametokea mtoni’.

Frawley (2003) anaongezea kuwa, mojawapo ya vikwazo vya kimofolojia katika lugha za Kibantu huhusu mpangilio wa nomino katika ngeli kwa kuzingatia mianzo ya nomino hizo.

Kigezo hiki huzua matatizo na changamoto kadhaa kwa watumizi wa Kiswahili kwa vile kuna nomino nyingine ambazo huwa na viambishi sawa lakini zinazua tungo tofauti zinapotumiwa katika sarufi kwa mfano, ‘kipepeo’, ‘kibogoyo’ na ‘kiongozi’ zina kiambishi ki- sawa na ‘kibeti’, ‘kiti’ na ‘kiambaza’. Uainishaji huu umependekezwa na wataalam kama Mgullu (mtaje), Habwe na Karanja (2004) pamoja na Obuchi na Mukhwana (2010). Uainishaji huu unadhihirisha ngeli zifuatazo:

- |            |          |                  |
|------------|----------|------------------|
| 1. MU – WA | Mu+tu    | Mtu-Watu         |
| 2. M – MI  | M+ti     | Mti-Miti         |
| 3. KI – VI | Ki+ti    | Kiti-Viti        |
| 4. JI – MA | Ji+cho   | Jicho-Macho      |
| 5. U – N   | U+devu   | Udevu-Ndevu      |
| 6. U – MA  | U+gonjwa | Ugonjwa-Magonjwa |
| 7. U-O     | U+kuta   | Ukuta-O+Kuta     |
| 8. O-MA    | O+debe   | Debe-Madebe      |
| 9. O-O     | Taa-Taa  |                  |

(Kutoka kwa *Mtalaa wa Isimu* ; Mgullu ,1995 :Uk. 153-156)

### **2.2.1.2 Uainishaji Kisintaksia**

Hiki ni kigezo cha kuainishia makundi ya ngeli kinachohusu uzingativu wa mofu zinazowakilisha nomino kwenye vitenzi. Mawazo ya wataalam anuwai yamejadiliwa ili kuonyesha uhusiano wa kazi zao na malengo ya utafiti huu. Wataalam kama Heine (1968),

Nkwera (1978) Kapinga (1983), Mbaabu (1985), Adewole (1986), Mohamed (1988), Mgullu (1999) na Mirikau (2008) wanakiita, ‘kigezo cha kisintaksia’. Uainishaji huu hujikita katika upangaji wa nomino katika makundi kwa kuzingatia upatanisho wa sarufi wa nomino hizo. Chomi (2001) akimnukuu Crystal (1985) anaeleza kuwa upatanisho wa kisarufi hutawaliwa na kiambishi patanishi na umefafanuliwa kama dhana ya kiisimu ambayo huelezea uhusiano uliopo baina ya neno na neno. Kiambishi hicho huonyesha upatanisho kati ya nomino na kitenzi au kati ya nomino na kivumishi. Baadhi ya hawa wataalam wamezianisha ngeli katika makundi tofautitofauti. Kipengele hiki kinahusiana na madhumuni ya kwanza ya utafiti huu kwa vile ni miongoni mwa mambo yanayozua changamoto na kuchanganyikiwa kwa watumizi wa lugha ya Kiswahili. Kwa mfano, Nkwera (1978) amezingatia ujozi katika uainishaji wa ngeli na anaibuka na ngeli nane. Uainishaji wake unatumia vipatanishi vya kisarufi ambavyo hupatikana katika mianzo ya viarifa au vitenzi. Ameziainisha ngeli za Kiswahili kama ifuatavyo;

- |              |                                       |                                                |
|--------------|---------------------------------------|------------------------------------------------|
| 1. A-WA      | Mpishi <b>a</b> – napika              | Wapishi <b>wa</b> – napika                     |
| 2. U-I       | Mji <b>u</b> – mevamiwa               | Miji <b>i</b> - mevamiwa                       |
| 3. KI-VI     | Kibeti <b>ki</b> – mepotea            | Vibeti <b>vi</b> – mepotea                     |
| 4. LI-YA     | Jina <b>li</b> – meitwa               | Majina <b>ya</b> - meitwa                      |
| 5. U-U       | Uzuri wake <b>u</b> – meonekena       | Uzuri wake <b>u</b> – meonekana                |
| 6. U-ZI      | Uso <b>u</b> – meng’ara               | Nyuso <b>zi</b> – meng’ara                     |
| 7. PA- KU-MU | Mahali <b>pa</b> – le ni pazuri au    | Mahali <b>ku</b> – le au Mahali <b>mu</b> – le |
| 8. KU – KU   | Kuimba kwake <b>ku</b> – nafurahisha  |                                                |
|              | Kuimba kwao <b>ku</b> – kunafurahisha |                                                |

Naye Adewole (1984) hazingatii ujozi katika uainishaji wake wa ngeli za Kiswahili. Anazianisha ngeli kutegemea upatanisho unaopatikana kwenye vitenzi vinavyotumiwa

pamoja na hizi nomino. Anatumia makundi kumi na matano. Upatanisho wake wa sarufi ni sawa na ule wa Nkwera (1978) katika matumizi ya sentensi.

1. KI Kibeti chake **ki**-mepatikana
2. VI vibeti vyao **vi**-mepatikana
3. A Mzee **a**-anaenda
4. WA Wazee **wa**-naenda
5. LI Jino **li**-meng'oka
6. YA Meno **ya**-meong'oka
7. U Mkoba **u**-menunuliwa
8. I Mikoba **i**-menunuliwa
9. U Ufagio **u**-mekatika
10. ZI Fagio **zi**-mepatikana
11. I Nguo yake **i**-meraruka
12. ZI Nguo zao **zi**-meraruka
13. PA-KU-MU Hapa **pa**-nafaa  
Huku **ku**-nafaa  
Humu **m**-nafaa

Mbaabu (1985) naye anaziainisha ngeli za Kiswahili kwa kutumia upatanisho uliopo baina ya nomino na vivumishi vionyeshi. Misingi ya upatanisho wake imo katika vivumishi vionyeshi kama ifuatavyo:

- |              |                                  |                                   |
|--------------|----------------------------------|-----------------------------------|
| 1. HUYU-HAWA | Mvulana <b>huyu</b> ni mkorofi.  | Wavulana <b>hawa</b> ni wakorofi. |
| 2. HUU-HII   | Mkeka <b>huu</b> umeraruka.      | Mikeka <b>hii</b> imeraruka.      |
| 3. HILI-HAYA | Jina <b>hili</b> limetajwa.      | Majina <b>haya</b> yametajwa.     |
| 4. HIKI-HIVI | Kijiko <b>hiki</b> kimenunuliwa. | Vijiko <b>hivi</b> vimenunuliwa.  |

5. HII-HIZI                      Nguo **hizi** zitashonwa.                      Nguo **hizi** zitashonwa.

6. HAPA-HUKU-HUMU              Mahali **hapa** pamechafuka.

                                         Mahali **huku** kumechafuka.

                                         Mahali **humu** mmechafuka.

Hizi ni nomino zinazoambatana na vionyesho au viashiria vya mahali. Pili, kuna nomino zitokanazo na vitenzi. Kwa mfano;

- Kuimba **huku** kunavutia.
- Kucheza **huku** kunavutia.

Kapinga (1983) akitofautiana na Mbaabu (1995) anaziainisha ngeli kwa kuzingatia upatanisho wa kisarufi unaojitokeza katika mianzo ya vitenzi vinavyoambatana na nomino.

Mfano;

1. YU-A-WA      Mtu **a**-takuja kesho.      Watu **wa**-takuja kesho.

                                         Mama **yu**-aja .              Akina mama **wa**-ja.

2. LI – YA              Jiwe **li**-metupwa.              Mawe **ya**-metupwa.

3. U – I                      Mti **u**-mekatwa.              Miti **i**-mekatwa.

Aidha, Kapinga (1983) anaziweka pia nomino zifuatazo katika ngeli ya YA-YA.

- Mafuta **ya**-limwagika.
- Maji **ya**-mechafuka.

4. I – ZI                      Nguo **i**-menunuliwa.              Nguo **zi**-menunuliwa.

5. U – ZI                      Uso **u**-mefura .              Nyuso **zi**-mefura.

6. U – YA                      Ugonjwa **u**-memmaliza.              Magonjwa **ya**-mewamaliza.

7. KU                      Kucheza **ku**-napendeza.              Kucheza **ku**-napendeza.

8. KI – VI                      Kisu **ki**-menolewa.              Visu **vi**-menolewa.

9. PA-KU-MU      Mahali hapa **pa**-navutia.

Mahali humu **m**-navutia.

Mahali huku **ku**-navutia.

Kulingana na kigezo cha kisintaksia, ni wazi kuwa hakuna mfumo mmoja unaotumiwa katika uainishaji wa ngeli. Hivyo basi, uainishaji wa ngeli kisintaksia huleta tofauti kubwa katika idadi ya ngeli anavyoshauri (Mgullu 1999). Anapendekeza kuongezwa kwa ngeli mbili kama ifuatavyo:

- |            |                                |                                      |
|------------|--------------------------------|--------------------------------------|
| 1. I – I   | Chai <b>i</b> -mepikwa na mama | Chai <b>i</b> -mepikwa na akina mama |
| 2. YA – YA | Mate <b>ya</b> -metemwa        | Mate <b>ya</b> -metemwa              |

Ngeli hii huhusisha nomino za vitu viowevu au majimaji. Nomino nyingine ni kama vile maji, mafuta, marashi, na kadhalika. Pia, Mgullu (1995) anapendekeza uainishaji wa ngeli kisintaksia ujitokeze kijozi au katika ujozi. Hali hii ni muhimu kwa vile husaidia katika kuziweka nomino katika umoja na wingi. Hivyo basi hurahisisha matumizi ya kila aina ya hizi nomino katika sentensi. Uainishaji huu wa ngeli ndio ambao unapendekezwa na kutumiwa katika silabasi ya shule za msingi na upili nchini Kenya (K.I.E, 2002). Uainishaji huu wa kisintaksia unajitokeza ifuatavyo:

- |            |                                 |                                    |
|------------|---------------------------------|------------------------------------|
| 1. YU-A-WA | Mtoto <b>a</b> -naenda shule    | Watoto <b>wa</b> -naenda shule     |
|            | Mtoto <b>yu</b> -aenda kwao     | Watoto <b>wa</b> -enda kwao        |
| 2. LI – YA | Jitu <b>li</b> -limvamia        | Majitu <b>ya</b> -liwavamia        |
| 3. U – I   | Mto <b>u</b> -livukwa.          | Mito <b>i</b> -livukwa.            |
| 4. KI – VI | Kiko <b>ki</b> -menunuliwa.     | Viko <b>vi</b> -menunuliwa.        |
| 5. I – ZI  | Nyumba <b>i</b> -mejengwa.      | Nyumba <b>zi</b> -mejengwa.        |
| 6. U – YA  | Ugonjwa huu <b>u</b> -natatiza. | Magonjwa haya <b>ya</b> -natatiza. |
| 7. U – U   | Uzuri wake <b>u</b> -limbariki. | Uzuri wao <b>u</b> -liwabariki.    |
| 8. U – ZI  | Uso wake <b>u</b> -mefura.      | Nyuso zao <b>zi</b> -mefura.       |



9. KU                    Kulia kwake **ku**-naudhi.
10. PA-KU-MU        Mahali hapa **pa**-napendeza.  
                               Mahali huku **ku**-napendeza.  
                               Mahali humu **m**-napendeza.
11. YA-YA            Maji **ya**-memwagika.            Maji **ya**-memwagika.
12. I – I                Sukari **i**-tanunuliwa.            Sukari **i**-tanunuliwa.

Kulingana na uainishaji huu, idadi halisi ya ngeli za Kiswahili ni kumi na mbili. Jambo la muhimu hapa ni kuwa, uainishaji huu unahakikisha kuwa kila kitenzi cha Kiswahili kinapata kiambishi cha ngeli katika vitenzi vyake. Hata hivyo, uainishaji huu ungali na changamoto kadhaa. Baadhi ya changamoto hizi ni kama vile kufanana kwa baadhi ya vipatanishi vya kisarufi kutoka ngeli moja hadi nyingine kwa mfano, Ngeli za U – YA, U – I na U –U zina vipatanishi vya U – vinavyofanana. Mifano ifuatayo inadhihirisha haya:

- Ugonjwa **u**-memponza (U – YA)
- Mkeka **u**-linunuliwa juzi (U – I)
- Uchoyo **u**-limletea dhiki (U – U)

Hapa, tunapata kuwa kuna matumizi ya vipatanishi vya kisarufi vinavyofanana katika hali ya umoja. Kwa hivyo hali hii huzua utata kwa matumizi ya kiswahili

Aidha, kuna ugumu katika kuainisha nomino zisizokuwa na ujozi katika uainishaji kwa mfano maiti, pua, shingo, giza, makala, jua n.k. Kwa mfano;

- Jasho **li**-namtiririka mfanyikazi
- Jua **li**-mewaka sana
- Giza **li**-litanda kote

Mifano hii ya sentensi inaonyesha kuwa hakuna ujozi bali sentensi hizi zimejikita katika ngeli ya LI. Mgullu (1995) anahitimisha kwa kueleza kuwa, kutokana na ugumu wa kubainisha idadi kamili ya ngeli kwa kuegemea katika kigezo cha kisintaksia, basi pamekuwepo na kujitokeza kwa idadi tofauti za ngeli katika vitabu tofauti kutegemea waandishi. Kwa hivyo, haya huleta utata kwa watumizi wa lugha ya Kiswahili hasa wanafunzi.

### **2.2.1.3 Uainishaji Kisemantiki**

Hiki ni kigezo cha kisemantiki cha kuyagawa majina katika makundi kwa kurejelea wataalam mbalimbali. Uainishaji huu umejikita katika uhusiano wa kimaana kati ya nomino za ngeli moja. Uainishaji huu umezigawa nomino za Kiswahili katika makundi kumi na manane. Uainishaji huu ni sawa na ule wa sintaksia unaopendekezwa na Mgullu (1995).

Mawazo ya Habwe na Karanja (2004) yanawiana na ya Obuchi na Mukhwana (2010) wanaposema kuwa mpango huu ulizingatia zaidi kuziainisha ngeli kwa kutumia mantiki, maana, asili na umbo la jina la kitu au kiumbe kilichotajwa na kuwekwa pamoja katika makundi au ngeli kwa mujibu wa matapo yao. Simala (2009) anayaunga mkono mawazo ya wataalam hawa anapodai kuwa maana na fahiwa katika lugha ndio msingi wa mawasiliano. Aidha, wataalam hawa wanadokeza kuwa uainishaji huo ni muhimu kwa sababu umesaidia katika kuzipanga nomino katika makundi kutegemea maana zinazotolewa na nomino hizo. Utafiti huo ukajikita katika msingi wa kutumia kiambishi cha upatanisho wa kisarufi kinachoambikwa kwenye kitenzi. Ndipo wanyama, wadudu, binadamu, nyuni, samaki na viumbe vyote kama hivyo, majina yao yakaorodheshwa katika ngeli moja ya a\_wa hivi:

1.Mtoto (A)\_ Mtoto anacheza a-

Watoto (WA) \_Watoto wanacheza wa-

2.Mti (U) \_ Mti ulianguka u-

Miti (I) \_ Miti ilianguka i-

3.Jiwe (LI) \_ Jiwe limepasuka li-

Mawe (YA) \_ Mawe yamepasuka ya-

4.Chuma (KI) \_ Chuma kimevunjika ki-

Vyuma (VI) \_ Vyuma vimevunjika vi-

5. Nguo (I) \_ Nguo imeraruka i-

Nguo (ZI) \_ Nguo zimeraruka zi-

6.Wimbo (U) \_ Wimbo umeanza u-

Nyimbo (ZI)\_ Nyimbo zimeanza zi-

Uainishaji huu ni kwa mujibu wa Habwe na Karanja (2004). Kila kigezo kina ubora na udhaifu wake. Kwa hivyo, kila mwanafunzi wa Kiswahili anafaa kumakinika katika matumizi mwafaka ya ngeli. Kwa hivyo uainishaji huweza kusababisha utata kwa wanafunzi hasa wasipo makinika.

Mgullu (1995) anadahili kuwa ni vigumu sana, katika lugha ya Kiswahili, kueleza kwa uhakika sifa za kimofolojia au kisintaksia zinazoweka pamoja nomino zenye maana moja ya jumla. Anaongezea kuwa ni vigumu kusema kwa mfano ngeli ya KI – VI ni ya nomino gani? Kwa hivyo, anahitimisha kwa kueleza kuwa kigezo cha kisemantiki kina uwezo mdogo sana wa kutumiwa kuainisha nomino za Kiswahili katika ngeli kwani kinaweza kutumiwa kuainishia ngeli moja tu – ile ya viumbe hai. Hata hivyo, anaeleza kuwa kigezo cha maana ni

muhimu kwa vile hutumiwa wakati wa kuzigawa nomino katika aina mbalimbali. Kwa mfano:

1. Nomino za pekee
2. Nomino za mguso
3. Nomino zinazohesabika
4. Nomino za jamii
5. Nomino za kawaida
6. Nomino za dhahania
7. Nomino zisizohesabika

Ni muhimu kuhitimisha kwa kusema kuwa, Mgullu (mtaje), anapendekeza vigezo viwili tu:

- a) Kigezo cha kimofolojia
- b) Kigezo cha kisintaksia
- c) Hii ni kwa sababu kigezo cha kisemantiki kinatuelekeza tu katika aina za nomino na wala si ngeli za nomino. Hata hivyo, Obuchi na Mukhwana (2010) wanapendekeza uainishaji wa kimofolojia na kisemantiki. Wakiunga mkono mawazo ya Simala (2009) wanapendekeza uzingativu wa kigezo cha maana anaposisitiza umuhimu wa maana fahiwa ambayo inajikita katika leksia ya maneno.

### **2.3 Namna makosa yanavyodhihirika katika matini**

Katika sehemu hii, utafiti huu unashughulikia dhana ya makosa, nadharia ya Uchanganuzi wa Makosa na uhakiki wa kazi mbalimbali kwa kutumia nadharia ya Uchanganuzi wa Makosa.

### 2.3.1 Dhana ya Makosa

Katika sehemu hii, utafiti huu umeshughulikia dhana ya makosa kama njia ya kuelewa chanzo cha matumizi ya makosa. French (1949) kwa mfano anatoa utafiti wa kina kuhusu makosa ambayo wanafunzi wamezoea kufanya. Naye Lee (1957) anatoa uchanganuzi wa baadhi ya makosa 2000 ambayo yanapatikana katika kazi iliyoandikwa na wanafunzi wa Kislovaki. Kazi hiyo inajumuisha makosa ya uakifishaji, kuongezea au kuondoa vibainishi, hijai, sentensi au tungo zisizo sahihi na matumizi mabaya ya nyakati au njeo. Mtaalam huyo alidai kuwa uchanganuzi huo wa makosa ulikuwa muhimu kwa vile ulimweka mwalimu katika hali bora na kuamua jinsi muda wa kufundisha ungeweza kutumiwa. Kwa hivyo, maelezo haya yanachangia utafiti huu kwa vile madhumuni ya kwanza yalikuwa na nia ya kubaini makosa ya matumizi ya ngeli miongoni mwa wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno. Kwa hivyo makosa ya ngeli yanaweza kuonyesha iwapo mwanafunzi amemakinika katika matumizi ya lugha kisarufi au la.

Kulingana na wataalam wengi, ili kuweza kuwa na muumano fulani katika sentensi kisarufi, ni sharti sheria fulani zitiliwe maanani ambazo kulingana na Chomsky (1965), ni sifa bia zinazotokea katika lugha yoyote ile. Kwa mfano, Ferguson (1984) na Barlow (1986) katika nakala yao ya *Agreement in Natural Language: Approaches, Theories, Descriptions* (eds.) (1988), uk.3, wanachangia dhana ya muumano katika sentensi ifuatayo;

Wa-toto    wa-nakula    samaki.

CL2-child    CL2-eat    fish.

‘The children are eating fish’.

Katika mfano huu, kiima **watoto** kina muumano na wingi wa viumbe hai unaowakilishwa na **wa** na kwa hivyo kitenzi **wa-nakula** hupatanishwa na wingi huo. Mawazo haya yanaungwa

mkono na TUKI (2004), wanapoelezea kuwa kosa ni wazo, tendo au jambo lililo kinyume na kanuni, taratibu au sheria. Ni hali ya kufanya lisilo sahihi au lisilokubalika. Dhana hii ni muhimu katika utafiti huu kwa vile uliazimia kutambua iwapo kuna makosa yoyote yanayodhihirika wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno wanapotumia ngeli. Kimsingi, wanafunzi wenye asili isiyo ya Kibantu wasipopata uelekezaji mwafaka huenda wakawa na makosa mengi kwa ajili ya ujumlishaji na athari ya lugha ya kwanza kama wanavyodai Selinker (1972) na Ligami (2002).

Utafiti huu unanua kuchunguza makosa ikiwa yapo, ambayo wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno hufanya kwa kurejelea matumizi yao ya ngeli mintaarafu upatanisho wa kisarufi. Kanuni hii itausaidia utafiti huu kutambua sentensi zilizo sahihi kisarufi na zisizo sahihi kisarufi kwa kuzingatia muumano kama uliodhihirika katika mfano huu.

Uainishaji huu unaopendekezwa na Mgullu huziainisha nomino kwa kuzingatia maana za nomino. Akimnukuu Loogman (1965) anasema kuwa ngeli ya MU – WA ambayo hudaiwa kuwa ni ngeli ya kwanza huwa ni ngeli ya viumbe vyenye uhai. Hata hivyo, hoja hii haitoshelezi na inaweza kupotosha kwa sababu si nomino zote za viumbe vyenye uhai huanzia na Mu (katika umoja) na Wa (katika wingi). Kwa mfano kuna nomino kama kijana/vijana, siafu/siafu, mbu/mbu, jambazi /majambazi na kadhalika.

Kulingana na Selinker (1972), dhana ya kufanya makosa ni ya Kisaikolojia na imo akilini mwa mwanafunzi husika. Anahusisha chanzo cha makosa ya lugha husika au ya pili na lugha ya mama ya mwanafunzi, kuhamisha lugha na lugha lengwa (Kiswahili-katika muktadha huu). Wakiongezea mawazo hayo, Richards na Rodgers (1986) wanadai kuwa kosa hufanywa na mwanafunzi anapoandika au kuzungumza kwa ajili ya kukosa makini, uchovu na kutozingatia yaliyomo miongoni mwa sababu nyingine.

Naye Johnson (1988) anaeleza kuwa makosa yanaweza kurekebisha na mwanafunzi, lakini katika mazoezi, kutambua iwapo mwanafunzi huyo hawezi kukosoa makosa yake ni tatizo, pengine akosolewe tu. Hali hii hutokea iwapo mwanafunzi yuyo huyo haelewi misingi na kaida muhimu za sarufi katika lugha husika.

Kwa mujibu wa Michaelides, (1990:30), anaeleza kuwa uchanganuzi ulioratibiwa makosa ya wanafunzi huweza kuwa na umuhimu mkubwa sana kwa wote wanaohusika kama vile walimu, wanafunzi na watafiti. Kwa walimu, makosa hudhihirisha bayana na kutoa taswira ya uelewa wa wanafunzi wa lugha husika.

Hobson (1990) akiunga mkono mawazo ya Michaelides (mtaje), anasema kuwa kosa moja huweza kusababisha msururu wa makosa katika matini. Isitoshe, anadahili kuwa, wataalam wengine huhesabu kosa linapotokea mara moja hata ikiwa limejiradidi ilhali wengine huhesabu kila kosa katika matini hata ikiwa limejirudia mara ngapi, na kadhalika. Hoja hii inaafikiana na ya (Lennon 1991). Ligami (2002) anaafikiana na mawazo haya anapoelezea kwamba makosa mengine ya kisarufi hupatikana kwa sababu ya kutofautiana kwa miundo ya lugha ya kwanza na lugha ya Kiswahili. Anachangia kauli hii kwa kusema kuwa, katika lugha ya Kiswahili kuna viambishi vya ngeli ambavyo huambishwa kwenye maneno yaliyomo katika sentensi. Kwa mfano:-

-paka mkubwa                      -kiti kkubwa

Ligami (2002) anaendelea kueleza kuwa hali hii ni tofauti katika lugha ya Dholuo kwa vile kivumishi hakibadiliki; kwa mfano:-

-*pus maduong'*                      -paka mkubwa

-*kom maduong'*                      -kiti kikubwa

*Maduong'* ina maana ya ukubwa.

Katika muktadha huu, hali kama hii huweza kumfanya mtumizi wa lugha ya Kiswahili kuenda kosa la sarufi mintaarafu ngeli. Ugunduzi huu ni muhimu kwa utafiti huu kwa vile linaweka msingi bora wa kulijibu swali la pili kuhusu makosa ya ngeli yanayofanywa na wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno.

### **2.3.2 Nadharia ya Uchanganuzi wa Makosa**

Sehemu hii inajadili nadharia ya Uchanganuzi wa Makosa. Nadharia hii iliasisiwa na Corder (1967) na kuendelezwa naye mnamo mwaka wa (1974). Nadharia hii ilitumika kutokana na uhusiano wake wa karibu na mada ya utafiti huu. Lengo la kutumia nadharia hii lilitokana na swali kwamba; Ni makosa yapi yanayotokea katika matumizi ya ngeli miongoni mwa wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno? Kwa kuitumia nadharia hii, utafiti huu ulichunguza makosa na changamoto za matumizi ya ngeli kwa njia tofauti miongoni mwa wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno. Kimsingi, historia ya nadharia hii ni ndefu ila kimatumizi kama chombo kuhusu kujifunza lugha, ilianza kutumiwa mnamo miaka ya sitini. Ellis (1994) anadai kuwa nadharia hii haikuwa ngeni kimaendeleo kwa vile uchanganuzi wa makosa ya wanafunzi ulikuwa ukitumika katika mbinu za ufundishaji.

Ni mnamo miaka ya sabini ambapo nadharia hii ilianza kutambuliwa kama sehemu ya Isimu tumizi – maendeleo yaliyotokana na kazi za Corder (1981a) katika mkusanyiko wa makala yake. Hapo awali katika makala yake ya semina, Corder (1967), aliandika kuwa makosa yanaweza kudhihirishwa katika njia tatu zifuatazo:

- 1) Makosa yalimpa mwalimu kutambua kiasi ambacho mwanafunzi alikuwa amejifunza.
- 2) Makosa yalimwezesha mtafiti kutambua jinsi lugha ilivyokuwa ikifundishwa.



- 3) Makosa yalitumika kama vyombo ambavyo mwanafunzi alitumia kutambua sheria za lugha lengwa.

Haya yalikuwa muhimu kwa utafiti huu uliolenga kutambua jinsi wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno wanavyotumia ngeli.

Corder (1974) anapendekeza hatua zifuatazo kama mihimili ya nadharia hii:

- 1) Kukusanya sampuli ya lugha ya wanafunzi.
- 2) Kutambua Makosa
- 3) Kuainisha Makosa
- 4) Kueleza Makosa
- 5) Kutathmini Makosa

Utathmini wa makosa ni muhimu kwa vile unaonyesha jinsi nadharia hii ya Uchanganuzi wa Makosa iliendelea miaka ya 1970 na 1980. Mhimili wa kwanza wa Corder (1974) unahusu kukusanya sampuli ya lugha ya wanafunzi. Hii ndiyo hatua ya kwanza katika Uchanganuzi wa Makosa. Nadharia hii huhitaji kuamua ni sampuli zipi za lugha ya wanafunzi zitakazotumiwa katika uchanganuzi na jinsi ya kuzikusanya sampuli hizi. Sampuli huweza kuwa kubwa, kadri au ndogo kutegemea idadi ya watafitiwa.

Mawazo ya Ellis (1994) yanakubaliana na ya Corder anapoeleza kuwa makosa yanayofanywa na wanafunzi huwa na sababu tofauti. Kwa mfano wanaweza kufanya makosa katika maongezi, ila hawafanyi katika uandishi kutegemea njia mbalimbali zinazohusika. Corder (1973) anapendekeza njia mbalimbali za ukusanyaji wa data kutoka kwa lugha ya wanafunzi, kwa mfano, watafitiwa wanaweza kuhojiwa, usaili au kuandika insha. Kipengele hiki ni

muhimu katika utafiti huu kwa vile kinahusiana na mbinu za kukusanya data katika utafiti huu.

Kulingana na Corder (1974) mhimili wa pili unapendekeza utambuzi wa makosa. Mhimili huu unaeleza kuwa, lugha ya wanafunzi ikishakusakusanywa, makosa katika lugha yanafaa kutambuliwa. Ni muhimu kutambua kosa ni lipi na ni mbinu gani inayotumiwa kutambua mojawapo. Katika utafiti huu mhimili wa utambuzi wa makosa umezingatiwa, kwa kubainisha makosa ya ngeli na Kiswahili sanifu.

Corder (1974), anasema kuwa mhimili wa tatu unahusu kuainisha makosa ya wanafunzi. Mhimili huu hujikita katika kulinganisha umilisi wa kiisimu wa wanafunzi. Njia sahihi ya kufanya hivyo ni kuanzia kategoria za kijumla kama vile: Mofolojia, sintaksia, semantiki na msamiati, Politzer na Ramirez (1973). Kanuni hii ni muhimu katika utafiti huu kwa vile dhana ya ngeli haipatikani katika ombwe tupu. Aidha, vijenzi vya sarufi (ngeli) ni mofolojia, sintaksia na semantiki.

Mhimili wa nne kulingana na Corder (1974), ni kuelezea makosa. Mhimili huu unadai kuwa baada ya kutambua na kuainisha makosa, ni bora kujaribu kuyaelezea kwa kutambua asili yake na kwa nini kosa hilo linafanywa. Katika utafiti huu, makosa ya ngeli yameelezwa na kujaribu kutambua asili yake.

Mhimili wa tano kwa mujibu wa Corder (mtaje) ni kutathmini makosa. Mhimili huu hujikita katika kutathmini na kutambua makosa na athari zake kwa watu husika. Katika utafiti huu, kutathmini makosa kunachangia pakubwa katika kuweza kutambua umilisi na utendaji wa kiisimu wa wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno. Mhimili mitano ya nadharia ya uchanganuzi wa makosa imetambulishwa katika utafiti huu kama njia ya kuweka wazi vile ngeli inavyotumiwa katika Chuo Kikuu cha Maseno, miongoni mwa wanafunzi wa

Kiswahili. Utafiti huu umetumia mihimili hii kwa kutambulisha na kuchunguza jinsi wanafunzi hao wanavyotumia ngeli kama itakavyojitokeza katika sura ya nne.

### **2.3.3 Uhakiki wa kazi mbalimbali zilizotumia nadharia ya Uchanganuzi wa Makosa**

Katika sehemu hii, utafiti ulijadili kazi mbalimbali zilizotafitiwa kwa kutumia nadharia ya Uchanganuzi wa Makosa. Hii ni njia ya kuweza kubaini ufaulifu au upungufu wa nadharia hii pamoja na mchango wake kwa utafiti huu. Kwa mujibu wa Ellis (1994) nadharia ya Uchanganuzi wa Makosa ilikuwa mojawapo ya nadharia za awali zilizotumiwa katika kuchunguza lugha ya wanafunzi ili kuweza kubaini jinsi walivyojifunza lugha ya pili. Anadai kuwa nadharia hii ilipata mashiko mnamo miaka ya sitini na sabini, hata hivyo, kwa ajili ya kuyaangazia makosa, ilisutwa na kupigwa vita na wataalam wachache kama vile, Bell (1974) na Long pamoja na Sato (1984). Ingawa hivyo, hivi karibuni imeanza kuthaminiwa na kutumiwa katika uwanda wa Isimu –tumizi (Taylor, 1986; Lennon, 1991).

Nadharia ya Uchanganuzi wa Makosa imetumiwa na wataalam kama Felix (1981) na Pavesi (1986) walipolinganisha lugha iliyosemwa na wanafunzi walioelekezwa na wale asilia. Bardovi-Harlig na Bofman (1989) walichunguza tofauti baina ya kundi la wanafunzi waliopita mtihani wa kuajiriwa katika Chuo Kikuu cha Indiana na wale waliofeli. Walitathmini na kuyaainisha makosa yaliyofanywa na makundi hayo mawili katika sehemu moja ya mtihani -insha na matokeo yalikuwa kwamba kundi lililofaulu lilifanya makosa machache kijumla kuliko kundi lililofeli. Isitoshe, mengi ya makosa hayo yalikuwa ya kileksia na kimofolojia kuliko yale ya kisintaksia. Tafiti hizi ni muhimu kwa utafiti huu kwa vile zinadhihirisha ushahidi wa mbinu ya usayansi katika utafiti. Hivyo basi, zimesaidia katika kuunga mkono madai ya Corder (1974), Selinker (1972), Dulay na Burt (1974b) pamoja na wengine mathalan utafiti huu.

## **2.4 Changamoto za matumizi ya Ngeli katika lugha mbalimbali**

Katika sehemu hii, utafiti huu umeshughulikia changamoto za matumizi ya ngeli katika lugha nyingine barani Afrika hasa lugha za KiBantu. Hali hii ni njia ya kutaka kuelewa chanzo cha utata wa dhana ya ngeli. Hali kama hii inadokeza chimbuko la utata wa dhana ya ngeli na changamoto zake.

Mbaabu (1995) anahusisha umuhimu wa ujuzi wa ngeli na umilisi na utendaji uliotajwa na Chomsky (1965). Mukuria (2002) akiunga mkono madai haya anaongezea kuwa kila lugha huwa na njia yake ya kuainishia nomino. Kuna lugha zinazozingatia uana ambapo nomino hupangwa katika kundi la kiume na kike kama Kiingereza, Kifaransa na Kimaasai. Migawanyiko ya nomino kiuana huathiri miundo ya nomino husika na hata vipashio vingine kwenye tungo. Haya huweza kuzua changamoto kwa mtumizi wa lugha husika, hasa akikosa kumakinika.

Kwa upande mwingine nomino katika lugha za Kibantu, kikiwemo Kiswahili huainishwa kwa kuzingatia mfumo wa ngeli. Kwa mujibu wa Frawley (2003), lugha za Kibantu hutegemea mfanano wa vikwazo vingi vya kifonolojia na kisintaksia. Hata hivyo, Chomi (2001) akichangia mawazo ya Mukuria (mtaje) anaongezea kusema kuwa huwezi kushughulikia sarufi katika lugha za Kibantu hasa Kiswahili bila kurejelea suala la ngeli.

Utata na changamoto katika matumizi ya ngeli ni jinsi maneno yanavyoundwa, sentensi zinavyopatanishwa, viwakilishi na vivumishi vinavyopatana kisarufi miongoni mwa mengine. Mawazo ya Choge (2006) na Gromova (2008) kuhusu utata wa ngeli yanawiana wanapodai kuwa hakujawahi kuwa na makubaliano kuhusu jinsi ngeli zinafaa kuainishwa, ingawa hivyo, utafiti huu unawania kutoa mikakati ya kukabiliana na matatizo hayo ya kisarufi na kuchanganua utata huo kwa kuangazia wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno.

Jambo kuu linalozua changamoto katika matumizi ya ngeli kwa lugha nyingi za KiBantu ni hali ya uainishaji wa maumbo ya ngeli. Hali hii huweza kutokea kwa vile wataalam mbalimbali wameweka maumbo ya ngeli tofauti. Mathalan mtaalam kama Lidwiko (2008), ametafitia ngeli za Kihehe na ametumia kigezo cha Mofo- Sintaksia na kuibuka na makundi kumi na manane ya ngeli. Vilevile, wataalam wengine kama vile Mirikau (2008) na Obuchi na Mukhwana (2010) wametumia vigezo vingine kama vile uzingativu wa viambishi kwenye nomino na viwakilishi vya vitenzi pamoja na uzingativu wa kigezo cha maana. Emmanuel (2008) anamuunga mkono Lidwiko kwa kuitafitia lugha ya Kipangwa kwa kutumia uainishaji huo huo wa Mofo- Sintaksia na kupata makundi kumi na manane. Haya huzua changamoto zaidi miongoni mwa wanafunzi wa taasisi mbalimbali kote ulimwenguni kwa sababu ya ukosefu wa kigezo kimoja maalum cha kupimia ngeli kwa jumla.

Vilevile, katika lugha ya Kiswahili, wataalam anuwai wametoa fasili mbalimbali za ngeli na kutumia vigezo mbalimbali kuainisha ngeli. Kwa mfano kuna wanaozingatia kigezo cha kimofolojia, kisintaksia na kisemantiki au hata vigezo viwili kwa pamoja. Jambo linalowakanganya watumizi wengi wa lugha ya Kiswahili wakiwemo wanafunzi. Kwa hivyo, dhana ya ngeli ni changamoto kwa vile watumizi wengine wa Kiswahili hawaelewi msingi wake. Hivyo basi, ingawa kuna changamoto nyingi zinazoizingira dhana hii ya ngeli, vipengele vinavyozua changamoto ni sawa na ndivyo vinavyochunguzwa katika utafiti huu. Ndiposa utafiti huu umezingatia matumizi ya ngeli miongoni mwa wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno.

## **2.5 Mikakati ya kukabiliana na matatizo ya kisarufi**

Mikakati mbalimbali imetolewa na wataalam mbalimbali ili kuweza kutatua utata wa ngeli na matatizo ya sarufi kwa jumla.

### 2.5.1 Uzingativu wa Sarufi

Sarufi ni ule utaratibu wa kanuni zinazomwezesha mtumiaji wa lugha kutoa tungo sahihi zinazoeleweka na pia kuelewa tungo zinapotolewa na mtu mwingine (Kapinga, 1983). Ni mpangilio maalum wa maneno kwa ufasaha kulingana na kanuni za lugha. Kwa hivyo, ni kupanga na kutumia maneno vizuri kulingana na mipango au taratibu zilizokubaliwa kuwa ni sahihi. Anaongezea kuwa lugha ya Kiswahili imejengwa kwa misingi ya ngeli. Hata hivyo, asemavyo Echessa (1990), watu wengi hushindwa kutofautisha maneno ya Sheng' na Kiswahili Sanifu, jambo linalotatiza sana maendeleo ya lugha hii. Kama anavyosema (Momanyi 2001: 187)

“...lugha ya Kiswahili imefika kwenye njia panda kwani idadi kubwa ya watu hawawezi kupambanua matumizi bora ya lugha ni yapi”.

Ng'ong'a (2002) akiongezea maoni haya na ya Miguda (2002) anaelezea kuwa wanafunzi wengi Chuoni hutumia Sheng' kuliko lugha nyingine. Mukuria (2002) anachangia madai haya anaposema kuwa sarufi ni sehemu muhimu sana katika Kiswahili, hasa sehemu ya ngeli ambayo ni uti wa mgongo wa lugha ya Kiswahili. Ni lazima mwanafunzi azielewe ngeli za nomino katika umoja na wingi pamoja na viambishi vyake ili kumwezesha kutumia ngeli na viambishi hivyo kwa usahihi. Sarufi vilevile, inahusisha vipengele muhimu kama vile vitenzi, majina, uakifishaji na matamshi mbalimbali. Ndiposa Diane na Jeanette (2002) wanaeleza kuwa masuala ya sarufi kwa wanaisimu hujikita katika kuangazia fonetiki, fonolojia, semantiki na leksia na wala si sintaksia na mofolojia pekee. Hali hii ni muhimu kwa utafiti huu kwa vile dhana ya ngeli haipatikani katika ombwe tupu. Hivyo basi, ni lazima mwanafunzi aelewe sarufi kwa ndani, kwa mapana na marefu ndipo aweze kujieleza kwa ufasaha na kuandika insha bora. Ngeli zina umuhimu mkubwa zaidi katika kuisarifu lugha. Vilevile, ngeli ndizo nguzo za sarufi na ufasaha wa lugha ya Kiswahili (Chomi, 2001).

Ndiposa utafiti huu unapendekeza uzingativu wa sarufi pamoja na mikakati mingine ili kukabiliana na matatizo ya kisarufi yanayotokana na kutozingatia matumizi sahihi ya ngeli.

### **2.5.2 Mkakati wa kutambua nomino ambazo hupatikana katika ngeli husika**

Utafiti huu unapendekeza kwamba nomino zigawanywe katika umoja na wingi kama mbinu msingi ya kuorodhesha nomino katika makundi. Haya mawazo yametolewa na TUKI (1981). Hali hii itamwezesha mtumizi wa lugha ya Kiswahili kutambua nomino husika. Chomi (2001) na Mukuria (2002) wanachangia mkakati huu kwa kufafanua kuwa nomino katika Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu huainishwa kwa kuzingatia mfumo wa ngeli. Kwa kuongezea hoja hii Frawley (2003) anasema kwamba lugha za Kibantu hutegemea mpangilio wa vikwazo vya kimofolojia vinavyohusu mpangilio wa nomino katika ngeli kwa kuzingatia mianzo ya nomino hizo. Kwa hivyo, mkakati huu ni muhimu kwa vile utamwezesha mtumizi wa lugha ya Kiswahili kutambua nomino inapatikana katika ngeli gani.

### **2.5.3 Mkakati wa kuzingatia maana ya nomino husika**

Michango ya baadhi ya wataalam wanaopendekeza mbinu hii ni kama Habwe na Karanja (2004) wanaoeleza ni mwafaka kwa vile husaidia katika kuziainisha nomino katika makundi kutegemea maana na fahiwa zilizotolewa na nomino hizo. Akiyachangia madai haya, Simala (2009) anasema kuwa ugumu wa maana ya lugha unatokana na mbinu za uchanganuzi zilizoasisiwa na wanasarufi mapokeo waliozingatia muundo na nafasi ya vipashio katika lugha badala ya kutilia mkazo fahiwa ambayo ni msingi wa maana. Kwa hivyo, ni muhimu kutambua maana ya nomino kileksia ambayo ndio maana kisarufi. Hata hivyo, maana katika lugha hukua na kubadilika kutegemea utamaduni. Katika muktadha huu, maana ya nomino ni muhimu hasa kwa utafiti huu kwa maana kuna maneno mengine yanayopatikana katika nomino tofauti ilhali yana muundo mmoja. Kwa hivyo, ili kuepukana na makosa ya kisarufi ni muhimu kuzingatia fahiwa ili kuleta maana ya msingi ya nomino husika.

#### **2.5.4 Mkakati wa kubaini kikundi cha nomino pamoja na sheria zake**

Katika sehemu hii, wataalam wengi kama vile, Heine (1968), Nkwera (1978), Kapinga (1983), Crystal (1985), Mbaabu (1985), Mgullu (1995) na Chomi (2001) wanapendekeza kuwa nomino ziainishwe kwa kuzingatia upatanisho wa sarufi wa nomino hizo. Wanaongezea kuwa kiambishi patanishi huonyesha upatanisho kati ya nomino na kitenzi au kati ya nomino na kivumishi. Mkakati huu ni muhimu kwa mtumizi wa lugha ya Kiswahili kwa sababu ataweza kutambua kwa haraka urari wa vipatanishi vya sarufi katika sentensi. Hata hivyo wakati mwingine mtumizi wa lugha ya Kiswahili hutatizika asipoweza kutambua maana ya nomino husika. Kwa hivyo, mkakati wa uzingativu wa maana huweza kumfaa katika hali hii.

#### **2.5.5 Mkakati wa kuzingatia wingi wa maneno ya ngeli tofautitofauti.**

Wataalam wengine wanapendekeza sheria za ngeli tofautitofauti zinapotumika kwa mfano Schmitt (2002) anasema kuwa nomino hizi zitumiwe kwa ujumla. Mifano kama vikombe, watu, mawe (zili, yali au vili) huweza kutumika. Yaani; vikombe, watu na mawe yalikuwepo. Anapendekeza kuwa ngeli ya nomino ya mwisho katika orodha itumiwe katika kuikamilisha sentensi. Hali kama hii huweza kumsaidia mtumizi wa lugha ya Kiswahili kufanya maamuzi ya haraka bila kusababisha makosa ya kisarufi. Kwa hivyo, hali hii huweza kuchangia katika kuepukana na makosa ya ngeli yanayochangia katika kuboronga sarufi.

#### **2.6 Nafasi ya Ngeli katika kuonyesha umilisi wa kiisimu wa lugha ya Kiswahili.**

Sehemu hii imeshughulikia mawazo ya wataalam mbalimbali kuhusu umilisi na utendaji wa kiisimu. Haya ni muhimu kwa utafiti huu kwa vile huathiri watumizi wa lugha ya Kiswahili. Hali hii hutokea katika matumizi kama ifuatavyo:



### **2.6.1 Umilisi na utendaji wa kiisimu**

Umilisi na utendaji wa kiisimu ni dhana mbili ambazo hutumika kuelezea hali ya viwango mbalimbali vya lugha. Kulingana na Chomsky (1995), aliipa dhana ya umilisi wa lugha umuhimu. Kulingana naye, wanajamii lugha huwa na ujuzi wa kuelewa mpango wa matumizi ya sentensi hizo katika lugha husika. Ndiposa aliuita ujuzi huu umilisi na ule wa matumizi ya lugha akauita utendaji. Hivyo basi, kuna viwango vinne vya umilisi na utendaji kiisimu ambavyo viliufaa utafiti huu. Navyo ni; kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika.

Kwanza kabisa, kusikiliza ni stadi ya lugha ambayo humtaka mwanafunzi kuipata fahiwa na mantiki ya yale anayosikiliza au kuyasoma, na kwa kawaida huambatana na sauti nyingine pamoja na kutazama kutegemea muktadha (Mendelson, 1994). Kuna njia mbili za kusikiliza. Kusikiliza kwa njia moja kama katika mhadhara ni kusikiliza ili kujifunza. Pia kuna kusikiliza kwa njia ya pili kunakohusu mjadala au mazungumzo. Hivyo basi, msikilizaji shupavu hutumia kusikiliza huku ili aweze kufahamu lugha zungumzi na msikilizaji husika kuweza kupata umilisi kupitia kwa utendaji unaostahiki.

Pili, ni kuzungumza. Stadi hii ni muhimu, ingawa hupuuzwa sana kwa vile hutumika kila mara kwa maisha ya kila siku. Kuzungumza humhitaji mmoja aweze kutambua ni kwa nini, vipi na ni wapi anawasiliana. Kuzungumza hutofautiana na kuandika. Stadi ya kuzungumza hudhihirisha umilisi kwa vile mtumizi wa lugha anaweza kutamka maneno kwa kutumia, mfano; toni na shadda ili kuweza kuzua tofauti ya kimaana.

Tatu, ni stadi ya kusoma. Kusoma huhusu kuelewa na kujifunza. Hivyo basi, kusoma ni njia ya kupokea na kutafsiri ujumbe kutoka kwa lugha moja kupitia kwa njia ya kurudufisha nakala (Urquhart na Weir, 1998). Kwa hivyo, kusoma huhusisha viwango vya fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki. Stadi ya nne ni ya kuandika. Stadi ya kuandika haitendeki tu katika ombwe tupu. Kuandika husaidia mtumizi wa lugha yoyote ile kuweza kuweka

fahiwa kwa karatasi au daftari. Uandishi ni mbinu inayohusisha kuandika insha, imla na makala tofauti tofauti.

Stadi hizi nne za lugha ndizo hudhihirisha viwango vinne vya kiisimu ambazo ni kusikiza, kusoma, kuzungumza na kuandika kama ilivyotambuliwa awali. Haya yanahusiana na utafiti huu kwa vile wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno walichunguzwa walivyotumia ngeli kwa kusikiza waliposailiwa, kuzungumza walipojadiliana katika mihadhara ya Kiswahili na kuandika insha na kuzisahihisha. Haya yaliazimia kuupima umilisi na utendaji wao wa kutumia ngeli za Kiswahili, na hivyo umilisi wa lugha ya Kiswahili kwa jumla.

Umilisi hupatikana katika matumizi ya lugha, asemavyo Chomsky (1986). Aidha, anadai kuwa umilisi wa kisarufi ni kule kujua umbo la lugha na maana katika matumizi yake. Aidha, mtu huongeza umilisi wa kiisimu katika maisha anapozidi kukua na hufikia viwango tofauti kwa watu tofauti (Coseriu, 1988). Mawazo yake yalituongoza sana tulipokuwa tukiulinganisha umilisi wa ngeli kuanzia wanafunzi wa mwaka wa kwanza hadi wa mwaka wa nne.

Umilisi wa kiisimu wa lugha ya Kiswahili hutegemea mambo kama vile mazingira anamokulia mtu (Habwe na Karanja, 2004). Ukiwa na umilisi wa kiisimu wa lugha, basi wewe una umilisi wa lugha hiyo (Lehmann, 2007). Hivyo basi ufasaha wako utakuwa wa hali ya juu. Kwa hivyo, dhana ya umilisi ni muhimu kwa utafiti huu kwa vile ulitusaidia kutambua jinsi ngeli za Kiswahili ziliweza kusaidia katika kudhihirisha umilisi wa kiisimu wa ngeli wa wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno. Hassan (2008) anasema kuwa ni sharti mtu aelewe sheria za utunzi wa lugha ndipo aweze kuwa na umilisi katika usemi, uandishi na isimu jamii.

Sehemu hizi tatu ndizo zinazompa mtu umilisi wa kiisimu katika lugha husika. Hivyo basi, kwa kujikita katika ngeli, utafiti huu ulidhamiria kuchunguza namna umilisi wa kiisimu wa lugha ya Kiswahili ulivyodhihirika wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu Cha Maseno walipotumia ngeli kama kipengele muhimu cha sarufi ya Kiswahili. Kwa hivyo, ni bayana kuwa dhana ya ngeli ina nafasi pana katika kudhihirisha umilisi na utendaji wa kiisimu wa lugha ya Kiswahili.

Chomsky (1965) alisisitiza umilisi na utendaji. Kulingana naye umilisi ni ujuzi ambao wanajamii lugha huwa nao wa kuelewa mpango wa lugha husika ilhali utendaji ni ule ujuzi wa matumizi ya lugha hiyo. Ngeli ni utaratibu wa taaluma ya sarufi ya lugha katika kupanga aina za majina (nomino) katika makundi kutegemea sifa fulani mahsusi kwa mfano, Ki – Vi, Ji – Ma na kadhalika (TUKI, 1981). Katika muktadha huu, ngeli katika lugha ya Kiswahili huweza kutambulishwa kwa viambishi vinavyounda mianzo ya nomino (kimofolojia), upatanisho wa sarufi (kisintaksia) na maana ya nomino hizi (kisemantiki). Kwa hivyo, ujuzi wa ngeli ni muhimu kwa mwanafunzi yeyote yule wa lugha ya Kiswahili kwa vile ni nguzo kuu katika kutambua umilisi na utendaji wa maneno katika lugha husika (Mbaabu, 1995). Kule kuwepo kwa idadi tofauti za ngeli katika vitabu tofauti hutegemea waandishi (Mgullu, 1995).

Musumeci (1997) anadokeza kuwa kuna haja kubwa ya mwanafunzi kutambua miundo na maana zinazojitokeza katika lugha husika. Ujuzi wa sheria za lugha ni muhimu katika kudhihirisha ufasaha wa lugha. Kwa hivyo, dhana ya ngeli ni muhimu katika kutekeleza majukumu haya. Asiyeelewa ngeli hawezi kutunga sentensi zilizo sahihi kisarufi kwa vile dhana ya ngeli hurejelea makundi ambamo nomino za Kiswahili hugawanywa (Chomi, 2001).

Frawley (2003) anadai kuwa lugha za Kibantu hutegemea mfanano wa vikwazo vingi vya kimofolojia na kisintaksia. Haya huathiri ngeli kwa sababu kuna maneno mengine ambayo huwa na mianzo na viambishi vinavyotofautiana ilhali hujumuishwa katika kundi moja la nomino. Habwe na Karanja (2004) wanashauri kuwa usarufi wa lugha ya Kiswahili umejengwa katika misingi ya ngeli. Mawazo haya yanawiana na Obuchi na Mukhwana (2010). Hivyo basi, ngeli isipokuwepo katika sarufi ya lugha ya Kiswahili huenda kukawa na dosari fulani itakayosababisha kuboronga kwa sarufi hiyo.

Silabasi ya Taasisi ya Elimu ya Kenya (KIE, 2002) ilionyesha wazi kuwa uainishaji wa mada ya ngeli katika shule za upili ulizingatia mfumo wa kimofolojia hapo awali lakini mfumo huo ulibadilishwa na ukaanza kufuata ule wa kisintaksia. Haya yaliwaathiri wanafunzi hasa waliouzoa mfumo wa kimofolojia kwa vile mfumo huo uliziweka nomino katika makundi kutegemea mianzo ya nomino hizo. KIE (2006) inadai kuwa kigezo cha sintaksia ni nanga kuu katika kuimarisha ufasaha wa mawasiliano baina ya wanafunzi. Jambo muhimu la kutambua hapa ni kwamba wanafunzi huweza kutambulishwa kwa miundo tofauti ya sentensi. Isitoshe, hali hii humweka mwanafunzi katika kuweza kutumia nomino kutegemea muktadha wa sentensi. Haya hupelekea mawasiliano mwafaka miongoni mwa wanafunzi hao. Kwa hivyo, mawasiliano hayo huweza kudhihirisha umilisi na utendaji wa lugha ya Kiswahili. Changamoto kadhaa zilijitokeza kama inavyodai KIE (2006). Kwa mfano mfumo huo ulizigawa nomino za viumbe wenye uhai katika ngeli tofauti.

Kwa mfano.

Ng'ombe – Ng'ombe (Ngeli ya N-N)

Mtu – Watu (Ngeli ya M-WA)

Mtume – Mitume (Ngeli ya M-MI)

Kiboko – Viboko (Mnyama – Ngeli ya KI-VI)

Kiboko – Viboko (Mjeledi – Ngeli ya KI-VI)

Kiziwi – Viziwi (Ngeli ya KI-VI)

Dereva – Madereva (Ngeli ya JI-MA)

Kijana – Vijana (Ngeli ya KI-VI) na kadhalika.

Ingawa nomino hizi ziliwakilisha viumbe wenye uhai (kisemantiki), ziliorodheshwa katika makundi ya nomino tofautitofauti. Jambo hili lilidhihirika wazi miongoni mwa baadhi ya wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno hususan wa mwaka wa kwanza. Wengi wao walitatizika katika kuyaainisha maneno katika ngeli husika. Hili lilitudhihirishia kuwa huenda baadhi yao waliyarithi matatizo hayo kutoka katika shule za upili. Huu ni uhamishaji wa matumizi na athari ya lugha ya kwanza. Hali hii imefafanuliwa zaidi na Henderson (2005). Gromova (2008) anachangia kwa kueleza kuwa, ingawa ngeli ni kipengele muhimu katika lugha ya Kiswahili, hakujawahi kuwa na makubaliano jinsi ngeli za Kiswahili zinavyofaa kuainishwa.

Hata hivyo, uainishaji wa kimofolojia ni tofauti na uainishaji wa kisintaksia ambao uliziweka nomino hizi katika ngeli moja. Utafiti wetu ulituelekeza katika kuufuata uainishaji wa kisintaksia kwa vile ulihusu upatanisho wa kisarufi. Ndiposa akronimu hii huenda ikawawezesha wanafunzi wengi kupata kumakinika. Viumbe wenye uhai. Kwa mfano;

#### **Ngeli ya (A-WA)**

BI – Binadamu  $\left( \begin{array}{l} \text{Kijana – Vijana} \\ \text{Mtu - Watu} \end{array} \right)$  Ngeli ya A-WA

WA - Wanyama –  $\left( \begin{array}{l} \text{Punda – Punda} \\ \text{Ng'ombe – Ng'ombe} \end{array} \right)$  Ngeli ya A-WA

WA – Wadudu (Siafu – Siafu) – Ngeli ya A-WA

N – Ndege (Kasuku - Kasuku) – Ngeli ya A-WA

SA- Samaki (Dagaa - Dagaa) – Ngeli ya A-WA

V – Vilema (Kiziwi - Viziwi) – Ngeli ya A-WA

**(Wazo la mtafiti)**

Hili linaonyesha kwamba, ingawa nomino nyingi katika ngeli ya A-WA zina viambishi tofauti, hiyo si sababu ya kuziweka katika makundi ya ngeli tofauti kwa vile yanapatana kisarufi (kuna upatanisho wa kisarufi) na hivyo basi katika kutunga sentensi, ‘a’ huweza kupachikwa kwa kitenzi au kivumishi katika umoja na ‘wa’ katika wingi. Kwa mfano;

Kijana **anakula** – Vijana **wanakula**.

Ng’ombe **anakula** – Ng’ombe **wanakula**.

Siafu **anakula** – Siafu **wanakula**.

Kasuku **anakula** – Kasuku **wanakula**.

Dagaa **anakula** – Dagaa **wanakula**.

Kiziwi **anakula** – Viziwi **wanakula**.

Isitoshe, baadhi ya nomino hazikuwa na viambishi vilivyofuata mianzo ya nomino (kimofolojia). Hii ina maana kuwa hakukuwa na viambishi awali vilivyoongoza mwanafunzi katika uainishaji wa ngeli kimofolojia. Hebu tazama mifano hii.

- a. **Kalamu**.
- b. **Karatasi** .
- c. **Baiskeli**.
- d. **Chupa**, na kadhalika.

Pia, kulikuwa na baadhi ya nomino ambazo huwa tu na viambishi pekee. Kwa mfano ngeli ya

JI – MA.

- a. Darasa – Madarasa

- b. Duka – Maduka
- c. Ua – Maua

Ule ukosefu wa viambishi ngeli katika hali ya umoja ulizua utata katika kutambua nomino hizo zilipatikana katika ngeli zipi. Hii ni mifano ya mambo yaliyozua utata katika matumizi ya ngeli.

## **2.7 Hitimisho**

Katika kutalii vitabu ambavyo vilitumiwa katika shule za upili, utafiti ulibainisha yafuatayo kwamba idadi ya ngeli katika vitabu hivyo haikuwa sawa kwa mfano katika Mgullu (1999). Ameerodhesha uainishaji wa kisintaksia kwa kuzingatia upatanisho wa sarufi ilhali Habwe na Karanja (2004) na Obuchi na Mukhwana (2010) wametumia uainishaji wa kimofolojia ambapo ngeli zimeainishwa kutegemea mfanano wa viambishi vya mianzo ya nomino. Kwa hivyo, mwanafunzi wa somo la Kiswahili ameachwa na jukumu la kujifunza ngeli kwa mwelekeo mseto bila ya kuwepo kwa mfumo maalum wa kuweza kumudu ngeli barabara. Tahakiki za wataalam hawa ni msingi muhimu kwa utafiti huu kwa vile unauongoza kutambua matatizo yanayotokana na matumizi ya ngeli yanayoathiri umilisi, ujuzi na utendaji wa lugha ya Kiswahili.

Utafiti huu umejikita katika nadharia ya Uchanganuzi wa makosa wa Corder (1974) kwa vile mwanafunzi wa Kiswahili huweza kujifunza ngeli kwa kuyatambua na kuyakosoa makosa y

## SURA YA TATU

### NJIA NA MBINU ZA UTAFITI

#### **3.1 Utangulizi**

Sura hii inajadili muundo wa utafiti, njia za utafiti, eneo la utafiti, kundi lengwa, usampulishaji, uchanganuzi na uwasilishaji wa data. Data iliyokusanywa ilihusu matumizi ya *Ngeli* miongoni mwa wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno, nchini Kenya.

Utafiti huu unazingatia muundo mseto. Mbinu zilizotumiwa zilikuwa kurekodi majadiliano katika vikundi maalum vya Kiswahili na usaili pamoja na uandishi wa insha kwa wanafunzi wa mwaka wa kwanza hadi wa nne, mwaka wa 2013. Pia, changamoto za utafiti zilifafanuliwa.

#### **3.2 Muundo wa Utafiti**

Utafiti unazingatia muundo mseto ambapo muundo wa kitathmini na kitakwimu imetumiwa. Utafiti wa kitathmini humsaidia mtafiti kuelewa namna matukio mbalimbali yanavyoathiriana na hali halisi ya kawaida (Strauss na Corbin, 1990). Akiunga mkono hoja hii, Mugenda, (2003) anasema kuwa muundo wa kitathmini huegemea katika uzoefu wa wahusika. Kwa kuzingatia muundo huu, utafiti huu uliweza kupata majibu mwafaka kwa maswali ya utafiti. Aidha, maswali mengi ya utafiti huweza kujibiwa kwa ukamilifu (Johnson na Onwuegbuzie, 2004).

Utafiti huu ulitumia muundo wa kitathmini uliojumuisha ukadiriaji wa umilisi wa kiisimu wa wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno kupitia; kuwarekodi kwa tepurekoda wakiwa wanajadiliana katika vikundi maalum vya Kiswahili na usaili, kisha kuwapa mada za insha kuandikia. Kwa hivyo, utafiti wa kitathmini ni bora kwa vile mtafiti anaweza kutumia tukio muhimu kudhibitisha wazi tukio lilo hilo kwa wasomaji kupitia kwa kukiangalia kitu kwa undani kisha kukadiria ubora wake au thamani yake (TUKI, 2013).



Utafiti huu ulitumia muundo wa kitakwimu kwa sababu hutumiwa kuelewa tukio ambalo halijulikani. Vilevile, husaidia katika upatikanaji wa ufahamu mpya ulio tofauti na hali inayojulikana (Strauss na Corbin, 1990). Muundo wa kitakwimu uliwezesha utafiti huu kubaini kiwango cha umilisi na utendaji wa kiisimu wa wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno kwa kuangazia idadi ya makosa mintaarafu ngeli.

Tafiti zilizojikita katika uchanganuzi wa matini, Eggins (2004) na Fairclough (2004) zilitumia uchanganuzi wa kitakwimu kufidia uchanganuzi wa kitathmini. Katika utafiti huu, uchanganuzi wa kitathmini ulijikita katika kuyatathmini makosa ili kutoa thamani yake ilhali uchanganuzi wa kitakwimu uliweza kutumiwa kusesitiza vipimo pamoja na uhusiano wa vipengele vilivyokuwa vikitafitiwa.

Kwa hivyo, insha zilichanganuliwa kitakwimu kwa kutumia vipengele vya kisarufi kimofolojia, kisintaksia na kisémantiki hususan ngeli ambapo makosa ya wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno yalitumiwa kubaini umilisi na utendaji wao wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili.

### **3.3 Eneo la utafiti**

Utafiti ulifanywa katika Chuo Kikuu cha Maseno katika jimbo la Kisumu nchini Kenya. Aidha, Chuo Kikuu cha Maseno kiliteuliwa kama mpangilio wa kifani cha kuwa kiwakilishi cha ngazi ya juu ya elimu. Chuo hiki kilikuwa na jumla ya wanafunzi 540 waliokuwa wakifanya somo la Kiswahili, mwaka wa 2013. Wanafunzi hao walikuwa wakichukua digrii ya kwanza. Haya ni kutokana na takwimu kutoka kwa mkuu wa Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Maseno.

Aidha, utafiti ulijumuisha wanafunzi wa miaka yote kuanzia mwaka wa kwanza hadi wa nne ili kuweza kupata fursa ya kulinganisha na kulinganua umilisi na utendaji wao wa lugha ya

Kiswahili. Uteuzi wa eneo hili ulitokana na baadhi ya maswali yaliyoulizwa na wanafunzi hao na mijadala ya warsha za walimu na wanafunzi kuhusiana na suala la ngeli. Kwa hivyo, uteuzi wa eneo hili ulisababishwa na mshawasha wa mtafiti kutaka kubainisha iwapo wanafunzi wa Chuo Kikuu walikuwa wametambua mchango wa dhana ya ngeli katika kuweza kuonyesha umilisi na utendaji wa kiisimu wa lugha ya Kiswahili. Hivyo basi, ilitarajiwa kuwa matokeo ya utafiti katika Chuo Kikuu cha Maseno yangetumiwa kuelezea hali ilivyokuwa katika Vyuo Vikuu vingine nchini Kenya. Sababu hasa zilizochangia katika kuchagua Chuo Kikuu cha Maseno ni kuwa hakujawahi kuwa na utafiti wa aina hii katika Chuo Kikuu hiki tangu kuanzishwa kwake. Kwa hivyo, kuchaguliwa kwake ni kwa kimaksudi.

### **3.4 Kundi Lengwa**

Utafiti huu ulilenga kazi za wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno wanaofanya shahada ya kwanza. Wanafunzi hao waliteuliwa kutoka mwaka wa kwanza hadi mwaka wa nne. Jumla ya wanafunzi hao ni 540 idadi ya kila mwaka ikiwa: mwaka wa kwanza – 250, mwaka wa pili – 80, mwaka wa tatu – 80 na mwaka wa nne ikiwa 130.

### **3.5 Usampulishaji**

Uteuzi sampuli wa mtabakisho kulingana na Kombo na Tromp (2006) huhitaji kwamba idadi ya watafitiwa igawanywe katika vijisehemu kisha uteuzi sampuli ulioratibiwa utumiwe. Katika utafiti huu, idadi ya jumla ya wanafunzi wa Kiswahili wa behewa la Maseno ilikuwa 540. Waligawanywa kulingana na mwaka kuanzia mwaka wa kwanza hadi wa nne (tazama jedwali 1). Mtafiti aliteua sampuli 54 ya wanafunzi hao kwa mujibu wa Mugenda (2003). Mugenda (mtaje) anapendekeza ushuru wa jumla ya idadi. Kwa hivyo, katika muktadha huu, kwa vile jumla ya wanafunzi wa Kiswahili ni 540, 1/10 ya idadi hiyo iliweza kuleta sampuli ya 54 ya wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno. Idadi hiyo ndiyo

iliyohusishwa katika kurekodiwa ikijadiliana, kusailiwa pamoja na kuandika insha. Mada za insha zilisampuliwa kimaksudi kutegemea kozi walizozifanya na dodoso zilihusu matumizi ya ngeli katika kuonyesha umilisi na utendaji wa kiisimu wa lugha ya Kiswahili. Kimukhtasari, sampuli hizo zilikuwa kama ifuatavyo; mwaka wa kwanza 25, mwaka wa pili 8, mwaka wa tatu 8 na mwaka wa nne 13. Uteuzi sahili usioratibiwa ulitekelezwa kwa wanafunzi wote. Wanafunzi walihitajika kuvichagua vijikaratasi vya ndio na **la** vilivyoandikwa kutegemea idadi.

Tazama jedwali hili:

<b>IDADI YA WANAFUNZI</b>	<b>MWAKA</b>	<b>USHURI YA IDADI YA JUMLA</b>	<b>SAMPULI</b>
i) 250	1	$\frac{1}{10} \times 250$	25
ii) 80	2	$\frac{1}{10} \times 80$	8
iii) 80	3	$\frac{1}{10} \times 80$	8
iv) 130	4	$\frac{1}{10} \times 130$	13
<b>SAMPULI JUMLA</b>			<b>54</b>

#### **Jedwali 1: Uteuzi sampuli wa mtabakisho**

Aidha, usampulishaji maksudi ulitumika ili kupata sampuli kumi na mbili za insha zilizoambatishwa katika kazi hii. Insha tatu zilitumiwa kwa kila mwaka a, b na c (tazama kiambatisho 4). Usampulishaji maksudi ulitekelezwa hivi:

<b>Kwanza</b>	<b>Pili</b>	<b>Tatu</b>	<b>Nne</b>
25	8	8	13
8	(3)	(3)	5
8	3	3	5
(3)	2	2	(3)
3			
3			

## **Jedwali 2: Usampulishaji maksudi**

### **(Ubunifu wa mtafiti)**

Kwa hivyo, kulingana na Patton (1990), usampulishaji maksudi hutegemea uchaguzi wa sampuli zisizoratibiwa kutokana na sampuli wakilishi za idadi ya jumla. Utafiti huu uliweza kupata insha tatu kutoka kwa kila mwaka na kuwa na jumla ya insha kumi na mbili ambazo ziliwekwa kama viambatisho vya kuyawakilisha makosa ya ngeli yaliyofanywa na wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno kuanzia mwaka wa kwanza hadi wa nne.

### **3.6 Ukusanyaji data**

Utafiti huu umetumia njia na hatua anuwai kukusanya data. Hali hii imeuwezesha utafiti huu kutimiza madhumuni yake. Aidha, njia hizi zimeuwezesha utafiti huu kukusanya data inayofaa na inayolenga matumizi ya ngeli katika Chuo Kikuu cha Maseno.

#### **3.6.1 Muda wa ukusanyaji data**

Ukusanyaji data ulitekelezwa kwa muda wa miezi mitatu; baina ya mwezi wa Februari na Aprili, 2013. Kipindi hiki kilikuwa muhimu kwa utafiti huu kwa maana utafiti huu kwa maana huo ndio wakati ambao mtafiti aliweza kuwapata wanafunzi wote kuanzia mwaka wa kwanza hadi wa nne.

### **3.6.2 Utaratibu wa ukusanyaji data**

Hatua ya kimsingi ilikuwa kupata kibali kutoka kwa Mkuu wa Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Maseno, idhini ipo kwenye kiambatisho 1 uk. 101. Aidha, mtafiti alihitajika kupata stakabadhi ya idhini kutoka kwa kamati ya maadili ya Chuo Kikuu cha Maseno, tazama kiambatisho 2 uk. 102. Vibali hivi vilikuwa muhimu kwa sababu vilimpa mtafiti fursa ya kujitambulisha kwa watafitiwa. Mtafiti akisaidiwa na wahadhiri husika kutoka idara ya Kiswahili alipanga muda wa kuwapata watafitiwa. Hii ilimwezesha mtafiti kunasa majadiliano na usaili pamoja na kuwahusisha watafitiwa katika uandishi wa insha. Watafitiwa walijibu maswali ya usaili na kujadiliana katika vikundi maalum vya Kiswahili huku wakirekodiwa. Azma na madhumuni ya utafiti yalibainishwa wazi kwa watafitiwa.

### **3.6.3 Uthabiti na utegemezi wa vifaa vya utafiti.**

Majaribio awali yalifanywa kwa lengo la kupata uthabiti na uhakikishaji wa vifaa vya utafiti. Haya yalikuwa na lengo la kupata data madhubuti ama isiyokuwa na shaka kwa utafiti huu.

Kwanza kabisa, ili kupata uhakika wa vifaa vya utafiti (kiambatisho 4 na 5), vilipewa wataalam katika Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Maseno ili kuvichunguza na kutathmini ubora wa kila kifaa na ufaafu wake pamoja na uwiano na malengo ya utafiti. Haya ni kwa mujibu wa Mugenda (2003). Wataalam hao walivipima kwa mizani ya kisayansi na mapendekezo yao yalitumika hatimaye katika kuunda na kuyachuja maswali ya usaili, mada za mijadala na mada za insha zilizokuwa na uwezo wa kuzua data faafu. Wanafunzi wa Kiswahili wa shahada ya kwanza ndio waliolengwa katika usaili, majadiliano na uandishi wa insha.

Majaribio awali yalitekelezwa baada ya kubaini uhakikishaji wa vifaa. Watafitiwa 20 wa Kiswahili kutoka Chuo Kikuu cha Maseno walishirikishwa katika majaribio awali ili kujibu

maswali ya usaili huku wakirekodiwa pamoja na majadiliano na uandishi wa insha. Sampuli hii ya wanafunzi haikutumiwa kwa utafiti huu, haya ni kwa mujibu wa Kombo na Tromp (2006). Majibu yao yalipimwa kwa mizani ya wataalam katika idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Maseno.

### **3.7 Mbinu za ukusanyaji data**

Ili kuweza kuchunguza matumizi ya ngeli miongoni mwa wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno, utafiti huu ulitumia njia mbalimbali kukusanya data.

Aidha, utafiti huu ulitumia mbinu ya uhakiki katika kufafanua maoni, mielekeo na mitazamo ya wataalam kuhusu mada ya utafiti.

#### **3.7.1 Utafiti wa Maktabani**

Utafiti huu ulifanywa kwa kuyadurusu na kuyachunguza maandishi kuhusu mada ya utafiti. Maandishi haya yalikuwa muhimu kwa vile yaliweza kuweka wazi misingi ya mada ya utafiti. Vilevile, yalitumika katika kuonyesha uhusiano baina ya tafiti za awali na mada ya utafiti. Jambo hili liliupa utafiti huu fursa ya kuweza kutambua hali iliyokuwa imewekwa na tafiti nyingine za awali zilizohusiana na utafiti huu.

Hivyo basi, hali hii iliweza kubainisha pengo la kujaliza kwa kuzingatia mwanya uliokuwa umeachwa na tafiti hizo. Maktaba za Vyuo Vikuu nchini kama vile Chuo Kikuu cha Maseno na Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro zilitumika pamoja na mtandao. Hali hii ilimwezesha mtafiti kuchanganua kwa mapana na marefu mada ya utafiti na hivyo kupata fursa ya kuweza kudhihirisha mianya iliyokuwepo katika kazi anuwai za wataalam mbalimbali.

### **3.7.2 Utafiti wa Nyanjani**

Utafiti huu ulifanywa katika Chuo Kikuu cha Maseno. Mtafiti alijihusisha na kuhudhuria majadiliano ya vikundi maalum vya Kiswahili. Hivyo basi, mtafiti alipata fursa ya kuwarekodi kwa tepurekoda wanafunzi hao wakijadiliana na pia aliwarekodi huku akiwasaili kisha akawapa mada za insha kuandikia kuanzia mwaka wa kwanza hadi wa nne. Utafiti huu ulifanywa baada ya mtafiti kufanya majaribio ya awali kwa kutumia sampuli ndogo ya wanafunzi ishirini akiwa na lengo la kupata uthabiti na ufaafu wa vifaa. Utafiti hasa ulifanywa katika kipindi cha mwezi wa pili hadi wa nne (2013).

#### **3.7.2.1 Majadiliano katika vikundi maalum vya Kiswahili**

Mbinu hii imehusisha kupanga wanafunzi katika vikundi maalum kwa kusikiza na kuwarekodi wakijadiliana kuhusu mada walizopewa za kozi mbalimbali kutegemea mwaka, (taz. kiambatisho 6 uk.109). Majadiliano ya wanafunzi wa kila mwaka yalirekodiwa kwa vile mtafiti alikuwa na nia ya kutambua jinsi wanafunzi hao walivyotumia ngeli katika mawasiliano yao.

#### **3.7.2.2 Usaili / Dodoso**

Mbinu hii ilihusisha maswali huru yaliyokuwa na nia ya kujibu maswali ya utafiti huu. Kwa hivyo, usaili ulikuwa na maswali yaliyohusu mada ya utafiti, (taz. kiambatisho 5 uk.106). Kulingana na Kothari (2004), ubora wa kifaa hiki mathalan humpa mtafiti nafasi ya kudadisi zaidi kwa kutunga maswali ya ziada na kumpa mtafiti majibu anayotarajia. Wanafunzi wa Kiswahili waliosampuliwa wa kila mwaka kuanzia mwaka wa kwanza hadi wa nne walirekodiwa wakisailiwa na mtafiti. Wasailiwa (ishirini na watano) 25 wa mwaka wa kwanza waliwakilisha wanafunzi 250, wasailiwa 8 (wanane) wa mwaka wa pili waliwakilisha wanafunzi 80, wasailiwa 8 (wanane) wa mwaka wa tatu waliwakilisha wanafunzi 80 ilhali wasailiwa 13 (kumi na watatu) wa mwaka wa nne waliwakilisha wanafunzi 130 wa Kiswahili

mtawalia. Walisailiwa kuhusu uelewa wao wa dhana ya ngeli pamoja na mielekeo na changamoto zilizowakumba walipotumia ngeli katika mawasiliano yao, kijumla, maswali yalilenga kuchunguza umilisi wao wa kiisimu wa lugha ya Kiswahili.

Aidha, makosa waliyoyafanya katika harakati zao za kutumia ngeli katika mawasiliano yalichunguzwa na kunakiliwa. Isitoshe, mtafiti alichunguza changamoto zilizowakumba walipotumia ngeli. Maswali hayo yaliandaliwa kwa lengo la kupata data kuhusu matumizi ya ngeli katika kudhihirisha umilisi na utendaji wao wa kiisimu wa lugha ya Kiswahili.

Wasailiwa wa kila mwaka walipewa muda wa kutosha kushiriki huku wakirekodiwa kwa tepurekoda. Maswali ya usaili yaliandaliwa vyema na yalikuwa yaleyale kwa wanafunzi wa mwaka wa kwanza hadi wa nne. Mbinu hii ya usaili ilikuwa njia bora ya kuweza kupima ukweli wa majibu ya wasailiwa kuhusu suala la ngeli. Kama wanavyoshauri Mugenda na Mugenda (2003) njia hii ya mahojiano hutoa maelezo ya ndani ambayo hayangepatikana iwapo mtafiti angetumia njia nyingine.

Mbinu hii ilitumika kwa kuwasaili wanafunzi kwa makundi tofauti ya wanafunzi katika vikao pekee (kwa kuwarekodi). Wanafunzi wa kila mwaka walishughulikiwa peke yao.

Utafiti huu ulirekodi wanafunzi wa kila mwaka kuanzia wa kwanza hadi wa nne kwa kuwasaili. Tulikuwa na sababu ya kulinganisha umilisi wao wa ngeli za Kiswahili kwa jumla.

### **3.7.2.3 Uandishi wa Insha**

Mbinu hii ilitumiwa ili kuweza kuzikimu mbinu nyingine za utafiti zilizotumiwa. Mtafiti aliandaa mada za insha kwa kila mwaka kuanzia mwaka wa kwanza hadi wa nne kwa kuongozwa na wahadhiri husika, mtafiti alipata fursa ya kuwapa wanafunzi walioteuliwa insha na wakaziandika kwa muda wa dakika arobaini. Urefu wa insha ulifaa kuwa kati ya maneno 200 – 300. Watafitiwa wa kila mwaka walishirikishwa kama ifuatavyo; Wanafunzi 25 (ishirini na watano) wa mwaka wa kwanza waliandika insha kuhusu; *mazingira ya Chuo*



*Kikuu na ya shule ya upili; Wanafunzi 8 (wanane) wa mwaka wa pili waliandika insha kuhusu; lugha ya Sheng' inatinga vipi maendeleo ya Kiswahili sanifu?; wanafunzi 8 (wanane) wa mwaka wa tatu waliandika insha kuhusu; jadili matatizo yanayokikumba kiswahili nchini Kenya na upendekeze namna tunaweza kuyasuluhisha; na wanafunzi 13 (kumi na watatu) wa mwaka wa nne waliandika insha kuhusu; namna utandawazi umesaidia katika mawasiliano. Jumla ya insha 54 ziliandikwa na wanafunzi hao. Insha zote zilisahihishwa na makosa ya ngeli kudondolewa. Tulitumia orodha ya uchunzaji kutambua makosa, tazama kiambatisho 8 uk.134 Hata hivyo, insha kumi na mbili (12) pekee ndizo zilizosampuliwa kwa kutumia usampulishaji kimfumo na kuwekwa kama viambatishi katika kazi hii, (tazama Kiambatisho 4 ).*

Lengo la uandishi wa insha lilikuwa kubaini na kudondoa makosa ya kisarufi kwa kuegemea kwa ngeli na kukadiria kiwango cha umilisi wao wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili. Tazama kiambatisho 4 kuhusu **mifano ya insha ya kila mwaka inayodhihirisha makosa** ya kisarufi kwa kurejelea kipengele cha ngeli. Uandishi wa insha uliteuliwa kwa vile ndiyo njia mwafaka iliyoweza kutumiwa kupata maandishi ya nathari kutoka kwa wanafunzi (Omondi, 1993).Utaratibu huu unaenda sambamba na mapendekezo ya Bachman& Palmer (1996) kuwa wanafunzi watoe majibu yanayoweza kutuzwa kwa kukadiria ustadi wa lugha husika. Kozi walizofaa kujifunza kulingana na mwaka zilizingatiwa. Mada za insha ziliteuliwa kutegemea kozi zao za Kiswahili na tajriba zao. Mada hizo ziliwasilishwa kwa baadhi ya wahadhiri wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno katika Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika na maoni yao kuhusu mbinu hii kutiliwa maanani. Ni muhimu kutilia maanani maoni kama hayo kwa kuwa uandishi wa insha una athari katika maisha ya watu (Messick, 1995).

Bachman & Palmer (1996) wanaeleza kuwa, ili insha iweze kuwa na uthabiti na ufaafu unaostahiki ni sharti itungwe ili kulenga madhumuni mahususi yanayolenga kundi la wanafunzi. Katika utafiti huu, insha zililenga kubaini makosa ya sarufi hususan ngeli pamoja na kupima umilisi wa kiisimu wa lugha ya Kiswahili kwa kuangazia wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno.

### **3.8 Uchanganuzi na uwasilishaji wa data**

Sehemu hii imetoa mwelekeo wa kuchanganua na kuwasilisha data tuliyokusanya nyanjani. Data zilizokusanywa kwa kurekodiwa ambazo zilihusisha mijadala na usaili zilinukuliwa na kusikizwa kwa muda wa takribani dakika 20 kutegemea kila mwaka kwa wiki tatu. Mtafiti alizirejelea data hizo kila mara ili kuweza kulinganisha na kulinganua matumizi ya ngeli kwa kuzingatia wanafunzi wa kila mwaka kuanzia mwaka wa kwanza hadi wa nne. Aidha, data zilizotokana na uandishi wa insha zilisahihishwa na kupangwa kulingana na kila mwaka wa wanafunzi ili kutambua umilisi na utendaji wa kiisimu wa wanafunzi hao katika lugha ya Kiswahili.

#### **3.8.1 Uchanganuzi wa kitathmini**

Uchanganuzi wa kitathmini husaidia katika ufahamu na utoaji maelezo ya kina kuhusu namna watu wanavyokabiliana na hali halisi (Johnson & Onwuegbuzie, 2004). Kwa hivyo, insha za wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno zilichanganuliwa kitathmini kwa kuzingatia uchanganuzi wa yaliyomo hususan makosa ya ngeli (sarufi). Uchanganuzi huo ulianza kwa kubaini ngeli sahihi na zisizo sahihi (Mgullu, 1995; 1999; Habwe na Karanja, 2004). Kisha kwa kuegemea katika nadharia ya Uchanganuzi wa Makosa (Corder, 1974), mtafiti aliweza kuzitambua hatua muhimu zilizohusu kuyadondoa makosa baada ya kupata sampuli ya wanafunzi miongoni mwa nyingine. Makosa yalidondolewa katika insha, vikundi maalum vya majadiliano ya Kiswahili na usaili kuanzia mwaka wa kwanza hadi wa nne.

Makosa hayo yaliwasilishwa kijedwali. Hatimaye tathmini ya makosa hayo ilitolewa. Maelezo ya kina yalitolewa kuhusu makosa ya ngeli tofauti tofauti na kutathminiwa vilivyo kwa mujibu wa mhimili wa tano wa Corder (1974) kuhusu kutathmini makosa na kutambua makosa yana athari zipi kwa watu husika.

### **3.8.2 Uchanganuzi wa kitakwimu**

Muundo wa utafiti ulikuwa kitathmini na kitakwimu. Uchanganuzi wa kitakwimu ulifanyiwa data iliyotokana na vikundi maalum vya majadiliano ya Kiswahili, usaili na insha. Lengo la kufanya hivyo lilikuwa kuweza kutoa muhtasari na ruwaza ya umilisi na utendaji wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili. Vile vile, umilisi wa kuandika, kupitia kwa insha ulikadiriwa kitakwimu kupitia kwa mwongozo. Tazama kiambatisho 3. Utafiti huu ulitumia viwango vya idadi ya makosa na alama wiano. Idadi ya utukiaji ni muhimu kwa vile inaweza kutumiwa kutoa muhtasari wa kiasi cha alama anazopata wanafunzi wasiomilisi matumizi ya vipashio vya sarufi (Brown, 1990). Takwimu zilikuwa muhimu kwa vile zilitusaidia katika kuyadondoa na kuyatathmini makosa. Aidha, zilisaidia utafiti huu kubaini matumizi ya kipengele cha ngeli kilichokuwa kikitafitiwa kwa kukadiria umilisi wa juu na wa chini kutegemea makosa yao.

Data za kitathmini zinabainisha utokeaji wa hali hizi katika Chuo Kikuu cha Maseno. Data hizo zinawekwa pamoja na kuorodheshwa katika sehemu kuu husika kutegemea maswali na madhumuni ya utafiti. Hivyo basi, sehemu ya kwanza inarejelea changamoto zinazotokea wanafunzi hao wa Kiswahili walipotumia ngeli. Sehemu ya pili nayo ilihusu makosa ya ngeli. Sehemu ya tatu inazichunguza na kupendekeza mikakati ya kukabiliana na makosa hayo ya kisarufi. Kila sehemu ilichunguzwa na kuchanganuliwa ili kuweza kubainisha data za kitakwimu. Kila mojawapo ya sehemu hizo ilichanganuliwa na idadi kuwekwa pamoja na kuwasilishwa kwa mfumo wa asilimia. Data ziliweza kuwasilishwa kwa kutumia majedwali.

Hatimaye, mtafiti aliweza kutoa matokeo na mapendekezo kutegemea data zilizokuwa zimechanganuliwa.

Aidha, mtafiti alizisahihisha insha za wanafunzi hao ili kutambua iwapo kulikuwa na makosa yoyote ya ngeli (upatanisho wa kisarufi) yaliyojitokeza. Aidha, changamoto zimedhihirika wazi na kuweza kuusaidia utafiti huu kuweza kujibu maswali yote ya utafiti.

### **3.9 Changamoto za utafiti**

Changamoto tulizokumbana nazo tulipokuwa tukifanya utafiti wetu zilikuwa nyingi. Kwanza kabisa, chombo cha kunasa sauti kilikuwa na hitilafu ya kimitambo. Haya yalitulazimu kujiandaa mapema na kutafuta fundi wa mitambo. Aidha, baaadhi ya wanafunzi waliokuwa wameteuliwa walikuwa wanafaa kufanya mitihani yao ya mwisho wa muhula. Jambo hili lilimlazimu mtafiti kuweza kuahirisha shughuli za usaili na uandishi wa insha. Isitoshe, kulikuwa na utata katika kuweza kuainisha maneno fulani katika ngeli kwa mfano maiti, miungu, ua na kadhalika. Ilimlazimu mtafiti kuweza kufafanua. Jambo hili lilifaa sana kwa vile liliwasaidia wasailiwa katika kuyajibu maswali ya usaili kwa njia huru na wazi. Ingawa hivyo, mtafiti alilazimika kutumia muda mrefu akishughulikia wanafunzi wa kila mwaka ili kuweza kupata data faafu. Hata hivyo, changamoto hizo zilimpa mtafiti motisha na ari ya kuendelea na utafiti hadi akafaulu katika kupata data kamilifu iliyofidia na kufanikisha utafiti huu.

### **3.10 Maadili ya utafiti**

Utafiti ulizingatia maadili kwa vile utafiti huu uliegemea katika kuwachunguza binadamu kama watafitiwa. Kulingana na *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* Toleo la Tatu , (2013), maadili ni matendo ya haki. Katika utafiti, dhana ya maadili inarejelea ile hali ya kupata kibali na kuweza kuwa na siri wakati wa kufanya utafiti. Kwa hivyo, hatua ya kimsingi ilikuwa kupata kibali kutoka katika Idara ya Kiswahili Na Lugha Nyingine za Kiafrika, Chuo Kikuu cha

Maseno (tazama kiambatisho 1). Kisha, mtafiti alitafuta idhini kutoka kwa Kamati ya Maadili ya Chuo Kikuu cha Maseno (tazama kiambatisho 2). Mtafiti alichukua jukumu la kuhakikisha kuwa kila mtafitiwa aliyehusika katika utafiti huu alipata heshima na staha aliyostahili. Kwa hivyo, waliohusika katika utafiti huu walipewa nakala za kupeana idhini (tazama kiambatisho 7) ili wamruhusu mtafiti kuwarekodi na kuwapa mada za kuandikia insha. Hayo yalihusu kutojitambulisha wakati wa kuandika insha na kutotoa habari kuhusu utafiti kwa yeyote ambaye hakuufurahia utafiti huu. Hivyo basi, mtafiti hakuweza kudanganya au kubadili data iliyotolewa na watafitiwa wakati wa kurudufisha nakala za kazi hii. Kwa hivyo iwapo kuna makosa yoyote yaliyoweza kujitokeza, hayakukusudiwa na mtafiti. Kwa upande wa kurekodi, mtafiti alizinasa sauti zao kwa hiari yao na wala hakuwashurutisha.

### **3.11 Hitimisho**

Sura hii imejikita katika kujadili muundo wa utafiti uliokuwa wa mseto; wa kitathmini na kitakwimu. Nalo eneo la utafiti limeelezwa wazi pamoja na kundi lengwa. Usampulishaji na ukusanyaji data umebainishwa. Njia na mbinu za utafiti zilizohusu utafiti maktabani na nyanjani zimeelezwa. Nao uchanganuzi na uwasilishaji wa data umeonyeshwa. Aidha, changamoto na maadili ya utafiti yameelezwa bayana katika sehemu hii.

## SURA YA NNE

### UCHANGANUZI NA UWASILISHAJI WA DATA

#### 4.1 Utangulizi

Sura hii imechanganua na kuwasilisha data kuhusu matumizi ya ngeli miongoni mwa wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno. Azma kuu ya sura hii ilikuwa kuweka wazi majibu kwa maswali na madhumuni ya utafiti huu. Haya yalidhamiria kufafanua mchango wa ngeli za Kiswahili katika kudhihirisha umilisi na utendaji wa kiisimu wa lugha ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Maseno nchini Kenya.

Vilevile, sura hii imejikita katika kujadili matokeo kuhusu matumizi ya ngeli miongoni mwa wanafunzi wa Kiswahili wa Vyuho Vikuu nchini kama ilivyobainika katika Chuo Kikuu cha Maseno. Data iliyokusanywa ilihusu kurekodi vikundi maalum vya mijadala ya Kiswahili, vilevile kurekodi usaili pamoja na uandishi insha. Aidha, data imechanganuliwa na kuwasilishwa kinaelezo, kijedwali na kwa kupitia kwa viwango vya asilimia.

#### 4.2 Makosa yaliyodhihirika wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno walipotumia ngeli

Madhumuni ya kwanza katika utafiti huu yalikuwa kutambua makosa yaliyodhihirika katika matumizi ya ngeli miongoni mwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Maseno.

Hivyo basi, katika muktadha huu, mtafiti analenga kuchunguza umilisi na utendaji wa watafitiwa kuhusu uelewa wao wa dhana ya ngeli kimatumizi. Haya yanadhihirika wazi kutokana na kule kunukuu na kusikiza rekodi za mijadala ya mihadhara ya kawaida ya Kiswahili na usaili pamoja na kuwapa na kusahihisha insha zao zilizoandikwa. Katika kuchanganua data, matumizi ya nadharia ya Uchanganuzi wa Makosa (Corder 1974) yaliuongoza utafiti huu.

#### 4.2.1 Data iliyotokana na mijadala iliyoleta kosa

Mwaka	Kosa	Sahihi
1	*lahaja la	Lahaja ya
2	*miundo za	Miundo ya
3	*uundaji ya	Uundaji wa
4	*Maana wa	Maana ya

#### Jedwali 3: Makosa kutokana na mijadala (Uorodheshaji nyanjani)

Makosa haya yalidondolewa kwa mujibu wa mhimili wa tatu wa Corder (1974) wa kuainisha makosa na Selinker (1972) anayezungumzia kuhusu ujumlishaji na athari ya lugha ya kwanza. Aidha, makosa ya mijadala yalikuwa machache kwa sababu wanafunzi walikuwa wamemakinika baada ya kurekodiwa wakisailiwa na kuandika insha.

Chomsky (1957) anadokeza kuwa umilisi wa kiisimu huhusu utendaji katika lugha na uwezo wa kuwasiliana kisahihhi. Aidha, umilisi wa kiisimu ni utaratibu wa kielimu katika isimu ya lugha inayomilikiwa na wanajamii lugha husika kama anavyoshauri Chomsky (1965). Kimsingi, umilisi ni dhana inayorejelea umahiri katika taaluma mbalimbali.

Hymes (1972) anadokeza kuwa umilisi wa mawasiliano huwa lengo kuu la elimu hasa katika mazingira ya darasani. Umilisi wa kiisimu huhusu utambuzi wa utamkaji wa sauti katika lugha, ufahamu wa maumbo ya maneno, miundo ya sentensi, maana zinazojitokeza katika maneno na sentensi na matumizi ya maneno, katika miktadha tofauti katika maisha ya kila siku. Ujuzi wa ngeli ni muhimu kwa mwanafunzi wa Kiswahili kwa sababu ni nguzo kuu katika kutambua umilisi na utendaji wa maneno katika lugha husika kama anavyodokeza

Mbaabu (1995). Haya yanatudhihirishia kuwa ngeli na umilisi ni mambo mawili yanayoathiriana kwa kiasi kikubwa. Kwa mujibu wa Chomi (2001), dhana ya ngeli inarejelea makundi ambamo nomino za Kiswahili hugawanywa. Ngeli katika lugha ya Kiswahili huweza kutambulishwa kwa viambishi vinavyounda mianzo ya nomino, upatanisho wa sarufi wa nomino hizi katika sentensi na maana ya nomino hizi.

Upatanisho wa kiisimu umefafanuliwa kama dhana ya kiisimu ambayo huelezea uhusiano wa kisintaksia uliopo baina ya neno na neno asemavyo Crystal (1980). Madai haya ya Crystal yameungwa mkono na Chomi (2001), anayeeleza kuwa upatanisho wa kisarufi hutawaliwa na kiambishi patanishi. Kimsingi, Ferguson na Barlow (1988) wanakubaliana na Crystal (1980) kwa kutoa ufafanuzi wa kina kuhusu muumano au upatanisho wa kiisimu. Wanaeleza kuwa ni sharti kuwe na upatanisho kati ya nomino, kitenzi na kivumishi ili kuleta muumano mwafaka katika sentensi husika. Kiambishi patanishi ndicho kinachoonyesha upatanisho kati ya nomino na kitenzi au kati ya nomino na kivumishi. Wanaongezea kuwa, muumano huu ukizingatiwa, basi mtumizi wa lugha husika ataweza kuepukana na makosa ya sarufi. Katika muktadha huu, hayo ndiyo makosa ya ngeli. Aidha, kwa mujibu wa Mgullu (1995), Habwe na Karanja (2004) na Obuchi na Mukhwana (2010), upatanisho ni muhimu sana katika lugha yoyote ile kwani hupunguza makosa.

Hivyo basi, kuna uhusiano mkubwa sana kati ya ngeli za Kiswahili na viambishi patanisho. Nomino zote zinazoakisiwa na viambishi patanishi sawa katika vivumishi au vitenzi huunda ngeli moja. Katika sehemu hii mtafiti alitaka kuchunguza uelewa wa watafitiwa kuhusu umilisi wao wa lugha ya Kiswahili. Jumla ya wanafunzi 54 wa Kiswahili walihusishwa katika mijadala, usaili na uandishi wa insha. Katika majibu yao, watafitiwa 48 (88.88%) walidhihirisha kuwa walifahamu dhana ya ngeli katika kudhihirisha umilisi wa lugha ya Kiswahili. Hata hivyo, idadi iliyosalia ya watafitiwa 6 (11.11%) ambao walijumuisha



wanafunzi wa Kiswahili wa mwaka wa kwanza walikuwa na utata katika kufahamu dhana ya ngeli na umuhimu wake katika umilisi wa lugha ya Kiswahii. Haya yalitokana na kusikiza na kunukuu rekodi za usaili na kuzisahihisha na kuchanganua insha zao. Hali hii ilidhihirisha bayana kuwa, licha ya dhana ya ngeli kuwa pana na tata, baadhi ya wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno walionyesha kwamba walitumia ngeli ipasavyo. (Tazama kielelezo cha 1 uk. 83).

#### 4.2.2 Makosa ya ngeli kutokana na insha

MWA KA	MADA	KOSA	SAHIHI	IDADI	ASILIMIA %
1a	<i>Mazingira ya Chuo na shule za upili</i>	Kengele <b>ambacho</b>	Kengele <b>ambayo</b>	10	47.62
1b	“	Vyumba <b>za</b>	Vyumba <b>vya</b>	06	28.57
1c	“	Mazingira <b>inayomzingira</b>	Mazingira <b>yanayomzingira</b>	05	23.81
<b>JUMLA</b>				<b>21</b>	<b>100</b>
2a	<i>Sheng'inavyotinga Kiswahili Sanifu</i>	Lugha <b>huu</b>	Lugha <b>hii</b>	08	30.77
2b	“	Soko <b>ya</b>	Soko <b>la</b>	13	50.00
2c	“	Jambo <b>hii</b>	Jambo <b>hili</b>	05	19.23
<b>JUMLA</b>				<b>14</b>	<b>100</b>
3a	<i>Matatizo yanayokikumba Kiswahili</i>	Tatizo kubwa <b>inayokumba</b>	Tatizo kubwa <b>linalokumba</b>	04	28.57
3b	“	Lugha ya Kiswahili <b>umekumbana</b>	Lugha ya Kiswahili <b>imekumbana</b>	02	14.29
3c	“	Matatizo haya <b>yanaifanya</b> Kiswahili	Matatizo haya <b>yanakifanya</b> Kiswahili	08	57.14
<b>JUMLA</b>				<b>14</b>	<b>100</b>
4a	<i>Utandawazi na mawasiliano</i>	Mawasiliano <b>wa</b> watu	Mawasiliano <b>ya</b> watu	03	27.30
4b	“	Faida moja <b>vya</b> utandawazi ni kwamba	Faida moja <b>ya</b> utandawazi ni kwamba	05	45.40
4c	“	Utandawazi umefanya nchi kuwa <b>dogo</b>	Utandawazi umefanya nchi kuwa <b>ndogo</b>	03	27.30
<b>JUMLA</b>					<b>100</b>

#### Jedwali la 4: Makosa kutokana na insha

Jedwali 4 linaonyesha makosa ya wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno kutokana na mbinu ya uandishi wa insha. Data hii ililenga kulijibu swali la pili kuhusu makosa yanayofanywa na wanafunzi hao. Jedwali hili limegawanywa katika sehemu nne kuu ambazo zinaonyesha sehemu ya mwaka, sehemu ya mada, sehemu ya kosa na majibu sahihi. Idadi ya makosa katika kila sehemu na asilimia yake imeonyeshwa.

Mtafiti alitumia jumla ya mada nne kutegemea kozi zilizofunzwa kwa kila mwaka. Insha za wanafunzi 54 zilisahihishwa na kutuzwa alama kutegemea idadi ya makosa kwa mujibu wa nadharia ya Uchanganuzi wa Makosa (Corder, 1974). Mhimili wa tano unahitaji mtafiti aweze kutathmini makosa na kuweza kukadiria umilisi kutegemea idadi ya makosa husika. Kwa kuegemea katika mhimili huu, jedwali hili linaonyesha kuwa wanafunzi wa mwaka wa kwanza na wa pili walikuwa na makosa mengi ya ngeli ikilinganishwa na wale wa mwaka wa tatu na wa nne. Kwa mfano; ni wazi kuwa wanafunzi wa mwaka wa kwanza(1a) walikuwa na asilimia 47.62% ya makosa; mwaka wa pili (2a) 30.77%; mwaka wa tatu (3a) 28.57% na mwaka wa nne (4a) 27.30% . Makosa haya ya uandishi wa insha yalifaribiana na yale ya usaili na majadiliano. Kwa mfano katika sentensi ifuatayo, kuna kosa linaloashiria utata wa vivumishi:

i) Uhuru\*yoyote badala ya uhuru wowote. (taz. uk. 108).

ii) Shughuli \*zingine badala ya shughuli ya shughuli nyingine.

(tazama uk. 109).

Vilevile katika sentensi ifuatayo, kuna makosa ya ukosefu wa upatanisho mwafaka wa kisarufi. Kwa mfano mienendo \*bovu badala ya mienendo mibovu (taz. uk. 121) kwa hivyo kosa hili ni la kisintaksia. Kwa kutumia usampulishaji kimfumo (Kombo & Tromp, 2006),

mtafiti alipata insha tatu tatu zilizoordheshwa kama; a, b na c kwa kila mwaka na kuweza kuziambatisha kwa utafiti huu ( tazama kiambatisho 4 uk.104) .

Kutokana na data hii, kimsingi ilionekana wazi kuwa kulikuwa na shida katika matumizi ya nomino na viwakilishi. Wanafunzi wachache walitumia nomino bila kuzingatia upatanisho wa kisarufi. Hawakutilia maanani muumano na makubaliano katika sentensi. Haya huenda yakawa yanatokana na athari ya lugha zao za kwanza au ile hali ya ujumlishi inayotokana na kuzingatia mianzo ya nomino kimofolojia kwa mfano: **\*Kengele ambacho kinawaambia,** kama ilivyodhihirika miongoni mwa wanafunzi wa Kiswahili wa mwaka wa kwanza. Katika muktadha huu, huenda wanafunzi hao walihusisha ngeli KI-VI na mwanzo wa nomino K-Kengele. Selinker (1969, 1972) anayahusisha makosa haya na ujumlishi na pia uhamishaji kutoka lugha ya kwanza hadi ya pili.

Ingawa wanafunzi hao wanatoka katika lugha za kwanza mbalimbali, ilikuwa wazi kuwa wanafunzi wengine walikosa kuzingatia sheria za sarufi. Wanafunzi huweza kutumia sheria visivyofaa (Richard, 1974). Ilikuwa dhahiri kuwa wanafunzi wengine walitumia ujumlishi kusababisha makosa ya ngeli. Ligami (2002) anachangia kuwa makosa ya aina hii huenda yakatokea kwa sababu ya ukosefu wa viambishi vya ngeli katika lugha ya kwanza ya mtumizi wa lugha husika.

Hata hivyo, utafiti huu ulibaini kuwa kulikuwa na wanafunzi wengine wa mwaka wa kwanza ambao walikuwa na makosa machache;(1c) 23.81% na mwaka wa pili (2c) 19.23% ambao walionyesha umilisi wa hali ya juu (tazama kiambatisho 4 uk. 104) Mifano yote iliyotolewa inadhihirisha hali ya umuhimu wa ngeli kama kipengele muhimu cha kupimia umilisi na utendaji wa lugha ya Kiswahili.

Hata hivyo, kwa kutumia nadharia ya Uchanganuzi wa makosa (Corder 1974) ili kudhihirisha matumizi ya ngeli miongoni mwa wanafunzi hao, mtafiti alisikiza na kunukuu rekodi za

majadiliano katika vikundi maalum vya Kiswahili na usaili pamoja na kuzisahihisha insha zao na kuorodhesha aina za sentensi zilizokuwa zikijitokeza. Sentensi hizi zilikuwa na aina tofauti ya vipatanishi vya sarufi na hali hiyo iliweza kudhihirisha ngeli mbalimbali.

Mtafiti alibainisha ngeli kwa kurejelea upatanisho wa sarufi (K.I.E 2002; Mgullu 1995, 1999; Habwe na Karanja 2004 na Obuchi na Mukhwana 2010). Ngeli zilizoorodheshwa ni kumi na mbili na zinaegemea katika upatanisho wa sarufi kisintaksia, ambao ni mwelekeo unaozingatiwa na wataalam wengi kama nilivyotaja hapo awali. Ngeli hizi zimeorodheshwa ifuatavyo;

1. Ngeli ya YU – A – WA
2. Ngeli ya U – I
3. Ngeli ya LI – YA
4. Ngeli ya KI – VI
5. Ngeli ya I – ZI
6. Ngeli ya U – U
7. Ngeli ya U – YA
8. Ngeli ya U – ZI
9. Ngeli ya YA – YA
10. Ngeli ya I – I
11. Ngeli ya KU –
12. Ngeli ya PA – KU – MU (Mahali)

Hata hivyo, Chesebe na Ndegwa (2010) wanaorodhesha ngeli kumi na nne wanaongezea ngeli za KI – Ø na LI – Ø kwa hizi zilizo hapo juu. Kwa mfano:

Ngeli ya {LI - Ø} – Jua

Ngeli ya {KI - Ø} – Kiswahili

### 4.3 Changamoto za matumizi ya ngeli

Kuna changamoto zilizotokea wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno walipotumia ngeli kimawasiliano. Data ilikusanywa kwa kutumia usaili uliorekodiwa.

Zifuatazo ni changamoto zilizojiri wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno walipotumia ngeli:

#### 4.3.1 Athari ya lugha ya Sheng'

MWA KA	SHENG'	NGELI	KISWAHILI	NGELI	KIINGER EZA	IDA DI	ASILI MIA (%)
1	a) Hedi b) Mboch c) Kiruru	Ø-MA Ø-MA KI-VI	Mwalimu mkuu – walimu wakuu Kijakazi/vijakazi Pombe/Tembo	A-WA A - WA I - I	Headmaster/ Headteacher Househelp Beer	12 6 7	48.00 24.00 28.00
<b>Jumla</b>						<b>25</b>	<b>100</b>
2	a)Daro b)Makopa c) Kushut	I-YA WA-WA WA KU	Darasa/madarasa Polisi/Polisi Kupiga risasi	LI – YA A – WA KU – KU	Classroom Policeman To shoot	3 3 2	37.50 37.50 25.00
<b>Jumla</b>						<b>8</b>	<b>100</b>
3	a) Hosi b)Maspidi c) Manzi	I-YA YA-YA Ø-MA	Hospitali/Hospitali Mbio/haraka Msichana/Wasichana	I – ZI I – ZI A - WA	Hospital Hurry/Rush Girl	2 3 3	25.00 37.50 37.50
<b>Jumla</b>						<b>8</b>	<b>100</b>
4	a)Gava b)Buda c)Ngovo, Kobole	I-YA Ø-MA I-YA	Serikali Baba Sarafu ya shilingi tano	I – ZI A – WA I – ZI	Government Father Five shilling Coin	5 4 4	38.46 30.77 30.77
<b>Jumla</b>						<b>13</b>	<b>100</b>

Jedwali 5: Sheng' katika Chuo Kikuu cha Maseno

Data hii ilitafitiwa kwa kutumia mbinu ya usaili (taz kiambatisho 5, swali la 5 uk 123). Jedwali hili limegawanywa katika sehemu nne kuu. Sehemu ya kwanza ni ya mwaka, ya pili ni ya Sheng', ya tatu ni ya Kiswahili sanifu na ya nne ni ya Kiingereza. Idadi ya watafitiwa walioshiriki katika usaili na asilimia yake imeonyeshwa. Kimsingi, jedwali hili linaonyesha kuwa lugha ya Sheng' inaathiri sarufi ya Kiswahili kwa vile maneno yake hayawezi kupangwa kwa makundi ya nomino yaani ngeli kama ilivyo lugha ya Kiswahili. Kwa mfano tukitazama mwaka wa kwanza (Ø-MA) katika sentensi: Hedi amekam – Mahedi wamekam badala ya mwalimu mkuu amekuja – Walimu wakuu wamekuja (A – WA). Hali hii husababisha ngeli za ziada kimofologia yaani Ø-MA. Mfano mwingine ni ule wa tatu: mwaka hosi imejengwa – Mahosi yamejengwa badala ya Hospitali imejengwa – Hospitali zimejengwa (I – ZI).

Kutokana na jedwali hili, tunapata kwamba wanafunzi wa mwaka wa kwanza (1a) waliochangia usaili walikuwa 12 ambao waliwakilisha asilimia 48.00%. Hii ina maana kuwa walitumia Sheng' kwa wingi. Katika mwaka wa pili (2a), idadi ya wasiliwa ilikuwa 3 iliyowakilisha asilimia 37.50%. Hali hii inaonyesha kwamba wanatumia Sheng' kwa kiasi kidogo kuliko wale wa mwaka wa kwanza. Jedwali hili pia linaonyesha ya kwamba, katika mwaka wa tatu (3a), wasailiwa 2 waliwakilisha asilimia 25.00%. Hii inamaanisha ya kuwa wanafunzi hao walitumia Sheng' kwa kiasi cha chini zaidi. Hali hii huweza kutokea kulingana na ile hali ya kwamba sasa wameanza kuwa na umilisi wa hali ya juu wa lugha ya Kiswahili. Aidha, katika mwaka wa nne (4a), wasailiwa 5 waliwakilisha asilimia 38.46% ya matumizi ya Sheng'. Hii ina maana kwamba wanafunzi wa mwaka wa nne wanatumia Sheng' kwa kiwango cha chini kiasi kuliko wa mwaka wa kwanza lakini juu ya mwaka wa pili na wa tatu. Hata hivyo, utafiti wetu unabaini kuwa wanafunzi hao wa mwaka wa nne wanatumia Sheng' kwa kiasi hicho wakiwa katika mawasiliano ya kawaida kando na mawasiliano maalum ya darasani au ya kujibu maswali ya mtihani. Kwa hivyo, mhimili wa kwanza wa

kwanza wa Corder (1974) unaosema mtafiti atambue sampuli ya lugha ya wanafunzi unaidia utafiti kuipata data hii ya Sheng' huku mhimili wake wa tano unaopendekeza makosa yatathminiwe unaidia utafiti huu kuyatathmini matumizi ya Sheng' kama changamoto inayowakumba wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno.

Kulingana na Momanyi (2001) lugha ya Kiswahili imefika kwenye njia panda kwa vile watu hawawezi kupambanua matumizi bora ya lugha ni yapi. Kwa hivyo, haya yanaonyesha kuwa Sheng' ni mojawapo ya changamoto zinazochangia katika kuvuruga sarufi ya lugha ya Kiswahili.

Jedwali lifuatalo linaonyesha data nyingine ya usaili kuhusu changamoto za matumizi ya ngeli ili kudhibitisha hali ilivyo katika Chuo Kikuu cha Maseno:



### 4.3.2 Changamoto ya vivumishi vinavyotatanisha

		VIVUMISHI TATANISHI					
Mwaka		Nomino	Ngeli	Kivumishi	Sahihi	Idadi	Asilimia (%)
1		Nguo Nguo	I – ZI	a).Ingingine b).Nyingine c).Zingine	Nguo nyingine	09 08 08	36 32 32
	<b>Jumla</b>					<b>25</b>	<b>100</b>
2		Jambo	LI – YA	a).Jingine b).Lingine c).Nyingine	Jambo jingine	03 03 02	37.5 37.5 25
	<b>Jumla</b>					<b>08</b>	<b>100</b>
3		Taifa	LI – YA	a).Nyingine b).Lingine c).Jingine	Taifa jingine	02 03 03	25 37.5 37.5
	<b>Jumla</b>					<b>08</b>	<b>100</b>
4		Nyumba	I – ZI	a).Nyingine au b).Zingine  c).Ingingine	Nyumba nyingine	03 03 07	23.08 23.08 56.16
	<b>Jumla</b>					<b>13</b>	<b>100</b>

#### Jedwali 6: Matumizi ya vivumishi vinavyotatanisha

Jedwali 6 linawakilisha matumizi ya ngeli katika Chuo Kikuu cha Maseno. Mtafiti alitumia mwelekeo mmoja wa maswali ya usaili kwa wanafunzi wote wa Kiswahili kuanzia mwaka wa kwanza hadi wa nne lakini katika vikao tofauti. Wanafunzi wa mwaka wa kwanza walikuwa wengi kwa idadi. Wanafunzi 25 ambayo ni asilimia 46.30% ya 54 iliyokuwa idadi ya jumla walihusishwa katika utafiti. Miongoni mwa wanafunzi hao, kwa mfano (1a) ambao walikuwa 9 na ambayo ni asilimia 36% walitatizika na vivumishi vya ngeli ya I-ZI. Kwa mfano, walichanganyikiwa ikiwa ni sawa kusema:

a) *Nguo 'nyingine' zinunuliwe. Au*

b) *Nguo 'zingine' zinunuliwe. Ama*

c) *Nyumba 'ingine' inunuliwe.*

Hali hii inaonyesha kuwa kuna baadhi yao; 1b na 1c waliowakilishwa na idadi ya 8(32%) na 8(32%) ama walitatizika kwa kiwango cha kadri au hawakutatizika mtawalia.

Jedwali hili la 7 pia linaonyesha jinsi wanafunzi wa mwaka wa pili walikumbwa na changamoto ya vivumishi tofauti. Wanafunzi wa mwaka wa pili waliosailiwa walikuwa(8) ambayo ni asilimia 14.81% ya idadi ya jumla ya 54. Miongoni mwa wanafunzi hao, wanafunzi 2a (3) ambao ni asilimia 37% walitatizika na matumizi ya vivumishi vya ngeli ya LI –YA kwa vile walikosa kubaini ikiwa watumie ‘ lingine’ au ‘jingine’ ama ‘nyingine’katika umoja. Hali hii inadhihirisha uchangamano wa dhana ya ngeli. Aidha, wanafunzi wa mwaka wa tatu pia walikuwa 8 na waliwakilisha 14.81% ya idadi ya jumla ya 54. Baadhi ya wanafunzi wa mwaka wa tatu kwa mfano, 3a ambao walikuwa 2 ni asilimia 25% iliyowakilisha wale waliokuwa na shida na vivumishi vya ngeli ya LI-YA. Walishindwa ikiwa sentensi iwe:

1) Taifa ‘nyingine’. Au

2) Taifa ‘lingine’. Ama

3) Taifa ‘jingine’.

Hali hii huzua kukanganyikiwa zaidi kwa watumizi wa lugha ya Kiswahili. Vilevile, kulingana na jedwali 3, wanafunzi wa mwaka wa nne walikuwa 13, idadi ambayo ilijumuisha asilimia 24.08% ya idadi ya jumla ya watafitiwa 54. Idadi ya wanafunzi 4a (3) inawakilisha asilimia 23.08% ya wanafunzi wa mwaka wa nne waliokuwa na matatizo ya

vivumishi vya ngeli ya I-ZI. Walishindwa kubaini kivumishi sahihi kati ya; Nyumba ‘nyingine’ na ‘zingine’.

Kwa hivyo, kutokana na jedwali hili, ni wazi kuwa wanafunzi hao walikuwa na tatizo la kubainisha vivumishi vya ngeli ya I-ZI na LI-YA. Kulingana na Choge(2006), yale yanayozua utata na changamoto katika matumizi ya ngeli ni jinsi maneno yanavyoundwa, sentensi, viwakilishi na vivumishi miongoni mwa mengine. Mawazo yake yanawiana na ya Gromova (2008) anapodahili kuwa hakujawahi kuwa na makubaliano kuhusu jinsi ngeli za Kiswahili zinafaa kuainishwa. Mawazo Gromova (mtaje) yanaafikiana na mawazo ya wanafunzi hawa anapotoa changamoto kati ya **jingine** na **lingine** na kuuliza ni kivumishi kipi kinafaa kutumiwa katika ngeli ya LI-YA. Kwa mfano;

- a) Gari ‘jingine’ limewasili? Au
- b) Gari ‘lingine’ limewasili.

Obuchi na Mukhwana (2010) wanachangia kwa kutoa suluhisho wakielezea kuwa, katika ngeli ya LI-YA;

Kiambishi Ji + ngine huongezwa na kupata **Jingine** kwa umoja na katika wingi kiambishi Me + ngine huongezwa na kupata **Mengine**. Kwa mfano;

- a) Gari **jingine** limenunuliwa.
- b) Magari **mengine** yamenunuliwa.

Anaongezea kuwa, chanzo cha matumizi ya kivumishi –ngine ni –ngi kwa mfano katika ngeli ya I-ZI, nomino **nguo** itakuwa **nguo nyingi** na kwa hivyo kivumishi –ngine kitakuwa **nguo nyingine** katika umoja na wingi na wala si nguo ‘zingine’

au nguo ‘ingine’, kama walivyodai baadhi ya wanafunzi hao. Hii ni kwa sababu hakuna, nguo ‘zingi’ wala nguo ‘ingi’ katika Kiswahili.

Kwa hivyo, mhimili wa tano wa Corder (1974) wa kutathmini makosa uliuwezesha utafiti huu kutathmini hali hii na kupata majibu ya swali la kwanza la utafiti kuhusu changamoto zinazowakumba wanafunzi hao.

Katika kutamatisha, changamoto za matumizi ya ngeli hudhihirika kwa njia mbalimbali. Changamoto hizo zilimshinikiza mtafiti pamoja na wasailiwa kutambua njia zilizoambatana na utambuzi mwafaka wa ngeli. Hivyo basi, mtafiti aliorodhesha njia nne ambazo zilikuwa kama mikakati ambayo ingeweza kutumiwa ili kutambua kipengele cha upatanisho wa sarufi mintaarafu ngeli. Njia hizo zilikuwa matumizi ya vikundi, maswali na majibu, maelezo pamoja na mifano (Tazama kiambatisho 5 nambari ya 6 uk. 129). Baadhi ya watafitiwa walidai kuwa hatuwezi kuutumia mkakati mmoja bali njia tofauti tofauti hata zikiwemo maigizo, nyimbo, kusoma makala mbalimbali kuhusu ngeli na kadhalika. Kwa hivyo, tuliafikiana katika usaili kuwa mbinu hizo zingetumiwa mradi tu zingeweza kusaidia katika utambuzi wa ngeli iliyofaa ili kuzua upatanisho mwafaka wa kisarufi.

#### **4.4 Mikakati ya kukabiliana na makosa ya kisarufi**

Tukirejelea malengo mahususi ya utafiti huu, lengo la tatu lilikuwa na azma ya kupendekeza mikakati au mbinu mwafaka za kukabiliana na makosa hayo ya kisarufi. Wakati wa kufanya utafiti wetu, mtafiti alikuwa na jukumu la kuyaandaa maswali ya usaili ambayo aliweza kuwauliza wanafunzi hao huku wakirekodiwa. Rekodi hizo zilisikizwa na kuhaririwa (tazama kiambatisho 5 swali la nambari 6).

<b>MWAKA</b>	<b>MIKAKATI/MAONI YA WANAFUNZI</b>	<b>IDADI YA WASAILIWA</b>	<b>ASILIMIA (%)</b>
1	Uzingativu wa maana Uzingativu wa sarufi Wingi wa nomino Nomino na sheria	07 06 06 06	28 24 24 24
<b>JUMLA</b>		<b>25</b>	<b>100</b>
2	Uzingativu wa maana Uzingativu wa sarufi Wingi wa nomino Nomino na sheria	03 03 01 01	37.50 37.50 12.50 12.50
<b>JUMLA</b>		<b>08</b>	<b>100</b>
3	Uzingativu wa maana Uzingativu wa sarufi Wingi wa nomino Nomino na sheria	03 02 02 01	37.50 25.00 25.00 12.50
<b>JUMLA</b>		<b>08</b>	<b>100</b>
4	Uzingativu wa maana Uzingativu wa sarufi Wingi wa nomino Nomino na sheria	04 04 03 02	30.77 30.77 23.08 23.08
<b>JUMLA</b>		<b>13</b>	<b>100</b>

#### **Jedwali 7: Mikakati kulingana na maoni ya wanafunzi**

Kulingana na jedwali hili, mikakati ifuatayo ilitolewa na na utafiti huu na kupewa wanafunzi ili watoe maoni kuhusu mikakati mwafaka:

##### 1. Uzingativu wa maana

Mbinu iliyotumiwa ilikuwa usaili. Idadi kubwa ya wanafunzi walipigia upatu mkakati huu kama mbinu faafu ya kutambua matumizi ya ngeli. Hali hii ilidhihirika hivi:

Kwa mfano, katika mwaka wa kwanza sentensi hii ilibainik: \* Kiboko kimekufa – Mwanafunzi wa mwaka wa kwanza alisema. Badala ya Kiboko amekufa

Mwaka wa kwanza 28%; mwaka wa pili, 37.50%; mwaka wa tatu, 37.50% na mwaka wa nne 30.77%. Mhimili wa tano wa Corder (1974) uliufaa sana utafiti huu kwa vile unaangazia kutathmini makosa. Jambo ambalo linamwezesha mtumizi wa lugha ya Kiswahili kuweza kutambua maana ya nomino kabla ya kuziainisha katika ngeli husika. Habwe na Karanja (2004) wanadai kuwa mbinu hii ni mwafaka kwa vile husaidia katika kuzianisha nomino katika makundi kutegemea maana na fahiwa zao. Isitoshe, Simala (2009) anaeleza kuwa, maana ni dhana ya kimsingi katika mawasiliano maana pia ni kipengele muhimu katika kazi hii.

## 2. Uzingativu wa sarufi

Mbinu iliyotumiwa ni usaili na insha. Baadhi ya wanafunzi waliunga mkono mkakati huu. Mwaka wa kwanza (24%), mwaka wa pili (37.50%), mwaka wa tatu (25%) na mwaka wa nne (30.77%). Kwa mfano katika uk. 105 (kiambatisho 4,1a) kuna kosa la sarufi “**mazingira hii**” badala ya **mazingira haya**. Hii inadhihirisha umuhimu wa wa kuzingatia sarufi ili kuepukana na makosa ya kisarufi. Mhimili wa kwanza wa Corder (1974) unaelezea kuhusu kukusanya sampuli ya lugha ya wanafunzi. Hali hii ilikuwa muhimu kwa utafiti huu kwa vile sampuli ya lugha ya wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno ilitathminiwa kwa mujibu wa mhimili wa tano wa Corder wa kutathmini makosa ili kutambua sarufi faafu kwa mujibu wa ngeli mintaarafu upatanisho wa kisarufi. Mengi ambayo yanajitokeza yanadhihirika katika kazi ya Mukuria (2002) kuwa sarufi ni sehemu muhimu sana katika Kiswahili, hasa sehemu ya ngeli. Nao Habwe na Karanja(2004) pamoja na Obuchi na Mukhwana(2010) wanadai kuwa asiyelewa ngeli, haimudu sarufi ya Kiswahili.

## 3. Wingi wa nomino

Mbinu iliyotumiwa ilikuwa ya uandishi wa insha. Wanafunzi wachache walipigia upatu mkakati huu. Mwaka wa kwanza (24%) mwaka wa pili (12.50%) mwaka tatu

(25.00%) na mwaka wa nne (23.08%). Kwa kuegemea katika nadharia ya Corder (1974), sampuli ya lugha ya wanafunzi katika uandishi wa insha iliufaa sana utafiti huu. Hali hii ilijitokeza katika baadhi ya insha za wanafunzi, taz. kiambatisho 4, mwaka wa pili 2(a) uk. 111; \*vitabu, majarida na magazeti inayoandikwa, badala ya; vitabu, majarida na magazeti yanayoandikwa. Mtaalam Schmitt ( 2002) anaeleza kuwa ujumla wa ngeli uzingatiwe kwa makini. Anatoa suluhu kuwa, nomino zikichanganywa, basi ngeli ya mwisho katika orodha hiyo ndiyo hutumika kuikamilisha sentensi.


#### 4. Nomino na sheria

Mbinu iliyotumiwa ni uandishi wa insha na usaili. Wanafunzi wachache walionelea mkakati huu ulikuwa mwafaka. Mwaka wa kwanza (24%), mwaka wa pili (12.50%), mwaka wa tatu (25%) na mwaka wa nne (23.08%). Kulingana na Corder ( 1974), mhimili wa pili unaelezea kuhusu kutambua makosa. Hivyo basi, uzingativu wa mhimili huu uliwezesha utafiti huu kuweza kutambua makosa ya sarufi. Kwa mfano, tazama kiambatisho 4, 5 na 6. Wataalam kama Mgullu (1995,1999), Chomi (2001), Habwe na Karanja( 2004) miongoni mwa wataalam wengine wanapendekeza matumizi ya nomino na sheria kama mkakati ili kutambua upatanisho wa sarufi mwafaka.

Ingawa mikakati hii ilitolewa maoni na wanafunzi, mikakati yote huweza kutumiwa katika kusuluhisha matatizo hayo ya kisarufi. Mikakati mingine mingi ipo ambayo inaweza kusaidia kama vile kutambua mianzo ya nomino na kuweka katika kikundi husika ila tu ni muhimu pia maana yake izingatiwe.

#### 4.5 Umilisi.

**Kielelezo cha 1: Umilisi wa ngeli za Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Maseno.**



#### **Ukokotezi nyanjani**

Data hii ilitokana na usaili na insha (tazama Kiambatisho 4 na 5). Jedwali hili linatupa taswira kuwa wanafunzi sita (6) miongoni mwa watafitiwa 54 ambayo ni asilimia 11 ya wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno walikosa umilisi kuhusu dhana ya ngeli. Kwa upande mwingine, wanafunzi arobaini na nane (48), idadi inayowakilisha asilimia 89 ya wanafunzi hao walikuwa na umilisi mkubwa kuhusu dhana ya ngeli. Kauli hii inatupa kigezo cha kubaini kuwa kuna pengo kubwa kati ya wale wanaomilisi dhana ya ngeli na wale wasioimilisi. Hivyo basi, kwa kutumia nadharia ya Corder (1974), mhimili wa tano wa kutathmini makosa unaidia utafiti huu kupima umilisi wa wanafunzi hao.

Kauli hii imeungwa mkono na Tewes (1991), anayetoa kigezo kuwa mtu anapozungumza, umilisi wake hufahamika kwa namna anavyojieleza na kuweza kuendeleza mazungumzo haya. Mtaalamu huyo anaendelea kudokeza kuwa ufasaha wa mtu ukiwa zaidi ya asilimia thelathini hadi arubaini na tano, huwa na umilisi wa hali ya wastani, na akiwa na ufasaha wa



zaidi ya asilimia sabini na tano, huwa na umilisi wa juu zaidi, akiwa na ufasaha wa asilimia chini ya thelathini, yeye huwa na umilisi wa kiisimu wa hali ya chini. Hivyo basi, swali letu la pili limeweza kujibiwa kwani utafiti wetu umedhihirisha kuwa kulikuwa na uwezekano wa ngeli za Kiswahili kuweza kuonyesha umilisi na utendaji wa kiisimu wa lugha ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Maseno.

Matumizi mazuri ya ngeli za Kiswahili huashiria umilisi wa juu wa lugha ya Kiswahili ilhali matumizi mabaya ya ngeli huashiria umilisi wa chini wa lugha ya Kiswahili, Mbaabu (1999) na Chomi (2001). Utafiti huu ulikuwa na lengo kuu la kuchunguza jinsi wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno walivyotumia ngeli kimawasiliano. Malengo mahsusi yalitalii makosa yaliyotokea, changamoto zilizojiri na mikakati ili kuonyesha umilisi uliodhihirika katika utendaji wao, hivyo basi, kuonyesha hali ya umilisi wao wa lugha ya Kiswahili. Baadhi ya wataalam kama vile Chomi (2001) na Mukuria (2003) wanasisitiza kuwa usarufi wa lugha ya Kiswahili umejengwa kwa misingi ya ngeli. Hivyo basi, anayeifahamu ngeli, anaimudu na kuwa na umilisi wa lugha ya Kiswahili. Utafiti huu ulijikita katika kuwapa wanafunzi mada za insha kutegemea mwaka ili kutambua matumizi yao ya ngeli. Tazama kiambatisho cha 4. Wanafunzi wa miaka ya juu (tatu na nne) walidhihirisha umilisi na utendaji wa hali ya juu kuliko wanafunzi wa miaka ya chini (kwanza na pili). Hata hivyo, ingawa nadharia tete ilikuwa kwamba wanafunzi wa viwango vya juu walikuwa na umilisi wa hali ya juu, utafiti huu ulibaini kuwa kulikuwa na wanafunzi wengine wa viwango vya chini waliokuwa na makosa machache na kwa hivyo walidhihirisha umilisi na utendaji wa hali ya juu.

#### **4.6 Hitimisho**

Katika sura hii, data ilihusu matumizi ya ngeli miongoni mwa wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno. Hivyo basi utafiti iliwania kuchunguza lugha halisi ya wanafunzi

hao katika mawasiliano yao. Mambo hayo yaliweza kujadiliwa kwa kina, nayo ni, makosa yaliyodhihirika wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno walipotumia ngeli kupitia kwa njia ya usaili, majadiliano na uandishi wa insha, changamoto zilizowakumba wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno walipotumia ngeli, na mikakati ya kukabiliana na makosa hayo ya kisarufi ili kuinua umilisi wao wa kiisimu katika Kiswahili na isimu kwa jumla.

## **SURA YA TANO**

### **MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO**

#### **5.1 Utangulizi**

Sura hii inatoa muhtasari, mahitimisho na mapendekezo ya utafiti huu. Inatoa muhtasari kwa kurejelea suala la utafiti, maswali ya utafiti, madhumuni ya utafiti na nadharia ya utafiti. Kimsingi, sehemu hii imetoa matokeo ya utafiti yaliyotokana na data iliyochanganuliwa kwa minajili ya kuonyesha na kuweka wazi matumizi ya ngeli miongoni mwa wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno. Aidha, sehemu hii inatoa mapendekezo ambayo yanaweza kutumiwa na watafiti wengine katika kushughulikia vipengele vingine vya sarufi na masuala mengine ya isimu kwa jumla.

#### **5.2 Muhtasari wa Utafiti**

Tumeigawa tasnifu yetu katika sura tano. Kwanza kabisa, katika sura ya kwanza, tulitoa dokezo kuhusu usuli wa utafiti, suala la utafiti, maswali ya utafiti, madhumuni ya utafiti, upeo wa utafiti, msingi wa utafiti, nadharia na umuhimu wa utafiti. Nayo sura ya pili ilijikita katika tahakiki ya maandishi yaliyohusiana na mada yetu ya utafiti. Sura ya tatu ilishughulikia njia na mbinu za utafiti. Sura ya nne ilijikita katika kuwasilisha na kuchanganua data kuhusu matumizi ya ngeli kama ilivyobainika katika Chuo Kikuu cha Maseno.

Suala la utafiti lilisababishwa na msukumo wa mtafiti kuwa dhana ya ngeli ilikuwa pana na tata kiasi cha kuzua changamoto nyingi mno na kuwakanganya watumizi wengi wa lugha ya Kiswahili. Kwa vile kulikuwa na ushahidi mkubwa wa matini ya ngeli za Kiswahili kuwa na changamoto katika matumizi na vilevile kuweza kutumiwa kuonyesha umilisi wa lugha ya Kiswahili, utafiti ulionyesha ule uwezekano wa ngeli kama kipengele muhimu cha sarufi kilivyoweza kuonyesha umilisi na utendaji wa lugha ya Kiswahili. Chuo Kikuu cha Maseno

kiliteuliwa kimaksudi na utafiti ukahusisha wanafunzi wa Kiswahili wa mwaka wa kwanza hadi wa nne wa mwaka wa 2013. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Corder (1974) . Utafiti ulikuwa na umuhimu wa kuweza kubainisha ngeli zinazotatiza na changamoto zake.

Utafiti ulifanywa katika Chuo Kikuu cha Maseno katika jimbo la Kisumu nchini Kenya. Wanafunzi 54 wa Kiswahili kuanzia mwaka wa kwanza hadi wa nne walihusishwa katika utafiti. Muundo mseto wa kitathmini na kitakwimu iliwanishwa. Sampuli ya 54 iliteuliwa kutoka kwa sampuli ya jumla ya 540 kwa kutumia uteuzi wa vikoja pamoja na uteuzi usioratibiwa. Mbinu ya ukusanyaji data ilikuwa ya kunasa sauti kwa tepurekoda majadiliano ya vikundi maalum vya Kiswahili na kurekodi usaili pamoja na uandishi wa insha ambapo wanafunzi walipewa mada kutegemea mwaka wao wa usajili katika Chuo Kikuu. Data iliyokusanywa nyanyani iliwekwa pamoja, ikasikizwa na kunukuliwa, ikahaririwa na programu ya Tarakilishi ya Kitakwimu kwa Sayansi Jamii [SPSS]. Data hiyo iliweza kuwasilishwa kimaelezo na kijedwali. Data hizi zilibainisha bayana uhalisia wa hali hizi kama zilivyotolewa nyanjani. Matokeo ya utafiti huu yalionyesha kuwa, wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu walikumbwa na changamoto za matumizi ya ngeli kama vile athari ya Sheng' na vivumishi tatanishi. Aidha, wanafunzi wa viwango vya juu kama mwaka wa tatu na wa nne walikuwa na makosa machache ya matumizi ya ngeli, jambo lililoashiria umilisi wao wa lugha ya Kiswahili. Kwa upande mwingine, wanafunzi wa viwango vya chini kama vile mwaka wa kwanza na wa pili walikuwa na makosa mengi, jambo lililoashiria umilisi wao wa chini wa lugha ya Kiswahili. Hata hivyo, utafiti huu ulibaini kuwa kulikuwa na wanafunzi wengine wa viwango vya chini waliokuwa na makosa machache, jambo lililopelekea utafiti huu kuhitimisha kuwa wanafunzi hao vilevile walikuwa na umilisi wa hali ya juu ya lugha ya Kiswahili kama wenzao wa viwango vya juu. Wanafunzi hao walipendekeza mikakati ya kukabiliana na matatizo hayo ya kisarufi kama vile uzingativu wa maana za nomino na sarufi.

### 5.3 Hitimisho la utafiti

Ilibainika wazi kuwa kuna makosa mengi ya ngeli yanayotokana na madhumuni yote matatu. Kwanza kabisa, ngeli zilizoleta utata ni ngeli zilizohusu maneno kama vile **maiti**. Wanafunzi wa miaka yote minne walishindwa kubainisha ikiwa neno hili liwekwe katika ngeli ya **A-WA** au **I - ZI**. Tazama kiambatisho 5, nambari ya 3 iv.

Pili, madhumuni ya kwanza ya makosa ya ngeli yalidhihirika kupitia kwa mbinu zote za utafiti: Majadiliano, usaili na uandishi wa insha. Makosa hayo yalihusu athari ya lugha ya kwanza, hijai na kutopatanisha maneno kisarufi. Mifano ya makosa ni kama vile, **magazeti inayoandikwa** badala ya **magazeti yanayoandikwa**. Tazama insha ya mwaka wa pili (2a), kiambatisho 4.

Isitoshe, kwa mujibu ya madhumuni ya pili ya changamoto, ni wazi kuwa lugha ya Sheng' inaathiri kwa kiasi kikubwa lugha ya Kiswahili kwani maneno ya Sheng' hayawezi kuwekwa katika makundi ya nomino mahsusi kama zilivyo nomino za Kiswahili sanifu. Badala yake, ngeli za ziada huibuka.

Tatu, vivumishi vinavyotatanisha vilizua maswali mengi miongoni mwao kwani walishindwa kubaini kwa mfano watumie 'gari lingine' au 'gari jingine' katika ngeli ya {li-ya} na ni hali ipi iliyokuwa sahihi.

Nne, wanafunzi walitoa maoni kuhusu mikakati ambayo ilitolewa na utafiti huu. Kwa mfano, asilimia 28% ya wanafunzi wa mwaka wa kwanza, asilimia 37.5% ya wale wa mwaka wa pili, asilimia 37.5% ya wale wa mwaka wa tatu na asilimia 30.7% ya wanafunzi wa mwaka wa nne walionelea kuwa mkakati wa uzingativu wa maana ulikuwa muhimu zaidi katika kuwasaidia kusuluhisha matatizo hayo ya kisarufi. Wengine wao walidai kuwa uzingativu wa sarufi ndio uliokua mkakati mwafaka ilhali wachache walionelea mikakati ya wingi wa

nomino na ule wa kuzingatia nomino na sheria zake. Hata hivyo, mikakati hiyo yote ikitumiwa kwa umakini huenda ikasaidia katika kutoa suluhisho kwa matatizo hayo ya sarufi na kuinua umilisi na utendaji wao wa kiisimu katika lugha ya Kiswahili.

Tano, wanafunzi hao walikanganyikiwa kuhusu nomino fulani zilizokuwa katika ngeli zaidi ya moja. Haya yalijitokeza wakati wa usaili (Tazama Dodoso, kiambatisho 5, nambari ya 3). Utafiti huu ulitambua kuwa wanafunzi hao walihitaji ujuzi wa kufanya utafiti zaidi na kutumia kamusi na mtandao katika kuweza kubainisha maana ya maneno kwa vile uainishaji huo wa kisemantiki ni muhimu. Iliaminika kuwa uainishaji huo wa kisemantiki ungeweza kuwasaidia katika kuainisha nomino katika makundi kutegemea maana na fahiwa zilizotolewa na nomino hizo. Ingawa hivyo, njia zote za uainishaji ni muhimu ila wataalam wa hapo awali walipendekeza ule wa kimofolojia ulioweka msingi na uliopendekezwa na mtaala wa ufundishaji katika shule za msingi na za upili nchini Kenya ni ule wa kisintaksia.

Kwa muhtasari, utafiti huu ulibaini kuwa ujuzi wa ngeli ni muhimu kwa mwanafunzi wa Kiswahili kwa vile ni nguzo kuu katika kutambua umilisi na utendaji wa maneno katika lugha ya Kiswahili. Hata hivyo, utafiti huu ulijikita katika uainishaji wa kisintaksia kwa vile huzingatia muktadha wa sentensi huku viambishi vya upatanisho wa sarufi vikiwekwa katika mianzo ya vitenzi na vivumishi katika sentensi husika.

#### **5.4 Mapendekezo ya utafiti**

Mapendekezo yafuatayo yametolewa ili kuweza kutambua matumizi mwafaka ya ngeli. Kwanza kabisa, makosa ya sarufi yatatuliwe kwa mkakati wa uzingativu wa sarufi sahihi, kusoma makala sanifu na ufahamu ili kukuza umilisi wa usikivu.

Pili, ili kuepukana na changamoto za ngeli, wanafunzi wazingatie mikakati iliyotolewa na utafiti huu kwa mfano, uzingativu wa maana na uzingativu wa sarufi. Aidha, vivumishi tata

vizingatiwe kwa kusoma vitabu sahihi. Pia, wanafunzi wahimizwe kuepukana na matumizi ya Sheng' kwani hutunga maendeleo ya Kiswahili sanifu.

Tatu, mikakati zaidi ibuniwe ya kuinua umilisi wa lugha ya Kiswahili.

Mwisho, wazo la Gromova (2008) laweza kutatuliwa na mapendekezo haya kwa vile utafiti huu umefafanua wazi jinsi kivumishi cha pekee –**ingine** miongoni mwa vivumishi tata kinafaa kuainishwa.

### **5.5 Mawanda mapya ya utafiti.**

Ngeli zitafitiwe katika lugha nyingine za Kiafrika kwa vile si zote zilizo na muundo unaofanana na lugha ya Kiswahili. Isitoshe, hali hii itachangia katika kuvumbua vipengele vingine vilivyo nguzo na msingi wa lugha hizi.

Makundi zaidi ya ngeli yabuniwe na kutafitiwa. Pia, ngeli za Sheng' zitafitiwe katika muktadha wa ulinganisho na Kiswahili sanifu. Vilevile, vipengele vingine vya sarufi kama vile vielezi vitafitiwe katika muktadha wa ngeli.

### **5.6 Taamuli**

Ngeli ni kipengele cha sarufi kilicho hai na bado kinakua.

## MAREJELEO

- Adewole, S.M. (1984). *'Agreement as a Cohesive Device in Kiswahili,'* M.A thesis, (Unpublished), Dar es Salaam : University of Dar es Salaam.
- Ambuyo, B. A. (2007). *Uhamisho Dhima* katika sentensi za Luloogoli:Tasnifu ya Uzamili, (Haijachapishwa) Kenyatta University.
- Ashton, E. (1944). *Swahili Grammar*, London, Longman Bleek, W.H.I. (1869),Comparative Grammar of South African Languages, London,Tubingen and Company.
- Bachman, L.F. & Palmer, A.S. (1996). *Language Testing in Practice*. New York: Oxford University Press.
- Bardovi – Harlig, K. & T. Bofman (1989). 'Attainment of Syntactic and morphological accuracy by advanced language learners.' *Studies in Second Language Acquisition* 11:17-34.
- Barlow, M. (1986). *Unification and agreement*. Paper presented at the Linguistic Society of America Winter Meeting, New York.
- Bloomfield, L. (1933). *Language*. New York: Holt, Rinehart and Winston.
- Broomfield, G.W.( 1931). *Sarufi ya Kiswahili*, London :The Sheldon Press.
- Burt, F. ( 1917). *Swahili Grammar and Vocabulary*, London: Society for Promoting Christian Knowledge.
- Canale, M. & Swain, M. (1980). 'Theoretical bases of communicative approaches to second language teaching and testing.' *Applied Linguistics* 1: 1 – 47.
- Chamot, A. , J. O'Malley, L. Kupper & M.Impink-Hernandez. (1987). *A Study Of Learning Strategies in Foreign Language Instruction: First Year Report*. Rosslyn, Va: Interstate Research Associates.
- Chesebe, M. & Ndegwa, D. (2010). *Secondary Breakthrough Workbook Kiswahili*: Nairobi: Moran Publishers Ltd.
- Choge, S. C. (2006). *Kusanifisha Kiswahili Sanifu*:Hitaji katika karne ya 21.SS. Sewangi & J.S Madumulla (Eds) Makala ya Kongamano la Kimataifa la Jubilei ya TUKI 2005, Dar es Salaam: TUKI uk. 25-35



- Chomi, W. E. (2001). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*, Sebha: African Studies Research Center.
- Chomsky, N. (2001). *Post Chomsky*. Cambridge: Massachusetts Institute of Technology Press.
- Chomsky, N. (1996). 'Some Observations on the Economy' in *Generative Grammar*: Cambridge: Massachusette Institute of Technology Press.
- Chomsky, N. (1995). *The Minimalist Program*: Cambridge: Massachusette Institute of Technology Press.
- Chomsky, N. (1993). 'A minimalist program for linguistic theory'. In *Hale and Keyser* 1993b.
- Chomsky, N. (1986). *Knowledges of language, its nature and use* Cambridge: M. I.T Press.
- Chomsky, N. (1965). *Aspects of the theory of Syntax*. Cambridge: Massachusette Institute of Technology Press.
- Chomsky, N. (1957). *Syntactic Structures*, The Hague: Mouton.
- Cohen, L. & Manion, L. (1994). *Research Methods in Education*. London Rontledge.
- Cohen, A. (1987) . 'Student processing of feedback on their compositions' in Wenden and Rubin eds
- Constitution of Kenya (2010). Nairobi: Government Printers.
- Cook, V.J. & Newson, M. (1996). *Chomsky's Universal Grammar*, 2nd edition Oxford: Basil Blackwell.
- Cook, V.J. (1988). *Chomsky's Universal Grammar*, Oxford: Basil Blackwell.
- Corder, S.P (1981). *Error Analysis and Interlanguage*. Oxford: Oxford University Press.
- Corder, S. P. (1974). 'Error analysis' in *Allen and Corder* (eds.) 1974.
- Corder, S. P. (1967). 'The significance of learners' errors'. *International Review of Applied Linguistics* 5:161-9.
- Coseriu, E. (1985). Linguistic competence: What is it really? *The Modern Language Review*. Cambridge: Cambridge University Press.

- Crystal, D. (1985). *A Dictionary of Linguistics and Phonetics*, (2<sup>nd</sup> Edition), London: Basic Blackwell Ltd.
- Diane, L.& Jeanette, D.( 2002). ‘An article on Introduction: Grammar and Grammars’ in *An Introduction to Applied Linguistics*. London: Holder Education.
- Dulay, H. & M. Burt. (1974b). Errors and strategies in child second language acquisition; *TESOL Quarterly* 8: 1 29 – 36.
- Echessa, P. (1990). “A Study of the Word Structure and Processes involved in Word Formation in Sheng’: A Case Study of Eastlands Area of Nairobi”. M.A. Thesis, Kenyatta University.
- Eggs, S. (2004). *An Introduction to Systemic Functional Linguistics 2<sup>nd</sup> Edition* London: Continuum.
- Ellis, R. (1994). *The Study of second Language Acquisition*. New York: Oxford University Press.
- Emmanuel, H. (2009). *The Kipangwa noun Class System*, Dar es Salaam: University of Dar es Salaam.
- Fairclough, N. (2004) *Discourse Analysis*. London: Routledge.
- Felix, S. ( 1981). “The effect of formal instruction and second learning language acquisition”. *Language Learning* 31:87-118.
- Ferguson, E. A. (1984). *Grammatical agreement in Classical Arabic and the colloquial dialects*. Paper presented at the meeting of the Middle Eastern Studies Association of North America.
- Fergusson, C.A, & Barlow, M. (eds.). (1988). *Agreement in Natural Languages: Approaches Theories, Descriptions*, United States. Stanford University.
- Fillmore, C., D. Kempler & W. Wang. (eds.). (1979). *Individual Differences in Language Ability and Language Behaviour*. New York. Academic Press.
- Frawley, W. J. (2003). *International Encyclopaedia of Linguistics*, New York: Oxford University.
- French, F. (1949). *Common Errors in English*. London: Oxford University Press.

- Gromova, V. N. (2008). 'Maswali Machache ya Usanifishaji wa Kiswahili' (Jingine au Lingine?) *Swahili Forum* 15, uk.115-120.
- Guthrie, M. (1967). *The Classification of The Bantu Languages*. London ; Dawsons of Pall.
- Habwe, J. & Karanja, P. (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*, Nairobi: Phoenix Publishers.
- Heine, B. (1976). *A Typology of African Languages based on the order of meaningful elements*, Berlin.
- Howart, A.P.R.(1999). History of Second Language Teaching. In Spolsky, B.(ed.). *Concise Eyclopaedia of Educational Linguistics*. Amsterdam: Elsevier.
- Hymes, D. H. (1972). *On Communicative Competence*, Philadelphia : University of Pennsylvania Press.
- Jespersen, O. (1922). *Language. Its Nature, Development and Origin*. New York: Macmillan.
- Johnson, R.B. & Onwuegbuzie, A.J. (2004). *Mixed Methods Research: A Research Paradigm who's time has come*. *Educational Researcher*, Vol. 33, No. 7. Pp. 14 – 26.
- Kapinga, M. C. (1983). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu*, Dar es Salaam: TUKI.
- Kawa, A. N. (2003). *The Syntax of Noun Phrase Movement in Kiswahili*, M.A Thesis, (Unpublished) Kenyatta University.
- Kerlinger, F. N. (1973). *Foundation of Behavioural Research*, New York : Holt Renchartand Winston
- King'ori, A.(2005). Movement in Kiswahili Sentence: A minimalist Approach: M.A.Thesis (Haijachapishwa), Kenyatta University.
- Kothari, C. R. (2008). *Research Methodology: Methods and Techniques. Qualitative and Quantitative*. 2<sup>nd</sup> edition.New Delhi: New Age Ltd. International Publishers Ltd.
- Kombo, D.K. & Tromp, D.L.A. (2006). *Proposal and Thesis writing: An Introduction*. Nairobi: Pauline Publications Africa. *Linguistics* 12:180-95.
- Krapf, J. (1882). *A Dictionary of Swahili Language*. London: Tübingen and Company.

- Lee, W. (1957). 'The Linguistics Context of language learning'. *English Language teaching journal* 11:77-85.
- Lehman, W.P. (1973). *Descriptive Linguistics*. New York: Random House.
